

**KIKUNDI NOMINO CHA KISWAHILI:  
MTAZAMO WA SINTAKSIA YA 'X-BAR'**

NA

**TOM MBOYA OLALI**


Tasnifu hii imetolewa kwa  
Madhumuni ya kutosheleza  
baadhi ya mahitaji ya

**Digrii ya Master of Arts (M.A)**  
katika **Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

**JUNI, 1997**

# IKIRARI


Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa na mtu yeyote kutosheleza mahitaji ya digrii katika chuo kikuu kingine.



---


**TOM MBOYA OLALI**

Tasnifu hii imetolewa Kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo kikuu cha Nairobi.



---

**DKT. BURENG G.V. NYOMBE**



---

**MWALIMU AGGREY K.WASIKE**

# FAHARASA

Ukurasa

Ikirari

Faharasa .....	(ii)
Tabaruku .....	(vii)
Shukrani .....	(x)
Orodha ya vifupisho na Ishara .....	(xiv)
Dibaji .....	(xvi)

<b>1.0 SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0.0 Utangulizi .....	1
1.1.0 Somo la utafiti .....	6
1.2.0 Madhumuni ya utafiti .....	13
1.3.0 Upeo wa tasnifu .....	14
1.4.0 Sababu ya kulichagua somo .....	15
1.5.0 Nadharia tete .....	16
1.6.0 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili .....	17
1.7.0 Msingi wa nadharia .....	24
1.7.1 Utangulizi wa nadharia ya umilikifu na masharti .....	36
1.7.2 Nadharia ya $\theta$ (theta).....	39
1.7.3 Nadharia ya uhusika .....	40
1.7.4 Nadharia ya masharti .....	40

1.7.5	Nadharia ya umilikifu .....	41
1.7.6	Nadharia ya umipaka .....	43
1.7.7	Nadharia ya ufafanuzi wa kiima cha kishazi kisoukomo .....	43
1.8	Njia za utafiti .....	44
	Tanbihi .....	46
2.0	<b>SURA YA PILI</b> .....	48
2.0.0	Mofolojia ya nomino .....	48
2.1	Ngeli za nomino .....	49
2.2	Uambishaji .....	53
2.2.1	Kundi la 1/2 .....	53
2.2.2	Kundi la 3/4 .....	55
2.2.3	Kundi la 5/6 .....	58
2.2.4	Kundi la 7/8 .....	62
2.2.5	Kundi la 9/10 .....	64
2.2.6	Kundi la 11/12 .....	66
2.2.7	Kundi la 15 .....	68
2.2.8	Kundi la 16, 17, na 18 .....	69
2.3	Unyambuaji .....	71
2.3.1	Kiishio -i .....	72
2.3.2	Kiishio -ji .....	73
2.3.3	Kiishio -E .....	74
2.3.4	Kiishio -O .....	76

2.3.5	Kiambishawali U-.....	79
2.3.6	Kiishio -U .....	80
2.3.7	Kiishio -A .....	81
2.3.8	Nomino kutokana na vivumishi .....	86
2.4	Muundo wa kimsingi wa nomino .....	87
2.4.1	Udogo wa nomino .....	89
2.4.1.1	Kundi la 1/2 .....	91
2.4.1.2	Kundi la 3/4 .....	93
2.4.1.3	Kundi la 5/6 .....	94
2.4.1.4	Kundi la 7/8 .....	95
2.4.1.5	Kundi la 9/10 .....	96
2.4.2	Ukubwa wa nomino .....	97
	Tanbihi .....	101
3.0	<b>SURA YA TATU</b> .....	102
3.0.0	Uvumishaji wa nomino .....	102
3.1	Vivumishi .....	104
3.1.1	Vivumishi vya sifa .....	105
3.1.2	Vivumishi vya idadi .....	111
3.2	Vielezi kiasi .....	119
3.2.1	Matumizi ya -enye .....	121
3.2.2	Matumizi ya -ingine .....	124
3.2.3	Matumizi ya -enyewe .....	126

3.2.4	Matumizi ya -ote .....	128
3.2.5	Matumizi ya o -ote .....	130
3.3	Vimilikishi .....	130
3.4	-A Unganifu .....	134
3.5	Vionyeshi .....	135
3.5.1	Vionyeshi vya ujirani .....	136
3.5.2	Vionyeshi vya ujirani wa mbali .....	137
3.6	Kishazi rejeshi .....	139
3.7	Amba -.....	140
3.8	-O rejeshi .....	142
3.9	Viwakilishi .....	146
3.9.1	Viwakilishi nafsi .....	147
3.9.2	Viwakilishi nafsi-huru .....	149
	Tanbihi .....	152
4.0	<b>SURA YA NNE</b> .....	154
4.0.0	Mtazamo wa sintaksia ya 'X-bar' .....	154
4.1	Kiunzi cha muundo virai .....	154
4.1.1	Muundo wa KN sahili .....	158
4.1.2	Kn .....→ N .....	159
4.1.3	Kn .....→ Kiw .....	159
4.1.4	Kn .....→ N (Kiv).....	161
4.1.5	Kn .....→ N (K.KIV).....	161

4.2	Kaida ya X-bar .....	162
	Tanbihi.....	188
5.0	<b>SURA YA TANO</b> .....	190
5.0.0	Hitimisho .....	190
5.1	Mapendekezo .....	193
	Marejeleo .....	195

# TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia mke wangu mpenzi Pauline Nkatha Olali, mtoto wangu Bill, Wazazi wangu Noah Olali Awino na Caren Anyango Olali. Wao ni wazazi wajuao uchungu wa mwana.

## Huba kwa Wazee Wangu

Mama, mpendwa mwenye huruma, mchungu wa roho yangu

Mama, ukikeshwa kwa lazima, amani iweko kwangu

Mama, ukae ukisimama, kwa kuhofu chozi langu

Nitakulipaje wema, ikubali twaa yangu

Mama, kinichombeza kwa hima, nitulize ari zangu

Mama, ukiimba na kusema, kunipoza roho yangu

Mama, unilaze na mapema, pale kitandani pangu

Nitakulipaje wema, ikubali twaa yangu

Mama, na usiku nigutuke, maziwa yako nataka

Mama, nitupe vitekete, nawe ukishughulika

Mama, na kinyesi kinitoke, hakika ukisumbuka

Nitakulipaje wema, ikubali twaa yangu



Mama, mikono yako himaya, mimi nilihifadhika  
Mama, na joto likininginya, hadi nikiburudika  
Mama, nawe kinikumbatiya, kwa imani iso shaka  
Sina la kukulipiya, mamangu muhibaka

Mama, na kitako uniweke, nilipotimu miaka  
Mama, kwa miguu nisoteke, napita nikianguka  
Mama, dede miguu nitake, na viambaza kushika  
Na wewe ushughulike, nisije nikavunjika

Mama, nikue nikaramke, unitie na chuoni  
Mama, nisome nielimike, niwe mtu duniani  
Mama, upowe ufurahikike, ili upate amani  
Hakuna wa kuipita, hadhi yako duniani

Mama, bado ninakuhitaji, kwa furaha na simanzi  
Mama, leo ninakutaraji, nizidishie mapenzi  
Mama, nipate njema siraji, mamangu nakuenzi  
Jambo lako silivunji, natenda bila upinzi

Baba, wewe sijakusahau, uli huko Asemboni,

Baba, wala sifanyi dharau, usinitie kosani,

Baba, mimi hukuweka juu, mlezi wa utotoni

Msaada wako mkuu, sijasahau abadani

Baba, na wewe msaidizi, sikutoi shukurani

Baba, rohoyo ina mbawazi, wende urudi kazini

Baba kunikumbuka kizazi, mote mwangu utotoni

Chakula pia mavazi, daima uli mbioni

Baba, unibebe kwa ulezi, unapokuwa nyumbani

Baba, unipanguse machozi, unisuke mikononi

Baba, unipe na uongozi, niongoke ukubwani

Sinacho cha kukujazi, pokea yangu imani

Mama, sitosahau faraji, na wema wako ulinzi

Baba, na damu haiwi maji, sitojitia kisunzi

Nyote, imani yenu saruji, ni msingi wa mapenzi

Radhi zenu nalitaji, dunia ina simanzi

S.A Mohamed (1980:46)

# SHUKRANI

Bila shaka, magambera na wakereketwa waliowahi kuandika tasnifu kama hii ikasomwa, wataniunga mkono nikisema kuwa kuhitimisha kazi hii si masihara bali ni sulubu haswa kama si kondo. Aidha, ni kazi ya ujima inayoundwa kwa mawaidha na mchango wa fikira kutoka kwa jamaa na jamii--Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kwa mintarafu hii, ningependa kuwashukuru wafuatao walioniwezesha kufika hapa nilipofika pa jivu la bongo kuzaa moto.

Sina namna ila kuwataja baadhi yao. Hata hivyo, kwa wale ambao sitawataja kwa sababu ya wakati na nafasi, nawaomba waelewe kuwa usaidizi wao ulinifaa zaidi. Sina budi kuwashukuru. Msaada wao si haba ingawa baadhi yao walinisabilia pasipo wao kujua kwamba wananikuza.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Bureng G.

Nyombe na mwalimu Aggrey K. Wasike ambao waliniongoza kwa kunipa mashauri si haba ambayo yalinisaidia. Mapendekezo yao ndiyo ambayo yameniwezesha kujitokeza na kazi kama hii. Lazima niongeze kusema kuwa, wao, asilani hawalaumiwi kwa kosa lolote lililojitokeza kwenye tasnifu hii.

Kama kuna dosari, nakiri litakuwa kosa langu wala si lao.

Aidha nawashukuru watu wafuatao kwa msaada wao wa makala, vitabu, miswada, vitabu na mashauri mema; Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz, Profesa Duncan Okoth-Okombo, Profesa Marzouk, Profesa Lucia Omondi na

Profesa Mohamed Bakari. Wengine ni Dkt. Kithaka wa Mberia aliyeifungulia ukurasa mpya katika kipengele cha sintaksia, Dkt. Marete, Dkt. Kineene wa Mutiso, na Dkt. Nyagah. Siwezi kuwasahau wahadhiri wengine katika idara ya isimu na lugha za kiasia kwa kushirikiana nami nilipowauliza maswali mengi mno, hususan, Ndg. Richard Songelaeli Mgullu, Ndg. Mwenda Mbatiah, Ndg. John Hamu Habwe, Ndg. Gichobi Mungania, Ndg. Muaka Lisanza na Ndg. Zachary Mumbo Mosoti. Sitamsahau daima dawamu.

Nawashukuru wazazi wangu mzee Noah Olali Awino na Mama Caren Anyango Olali kwa kuamua kujitesa na kujinyima ili wagharamie masomo yangu ya digirii ya pili. Ndugu zangu na dada zangu, ninawashukuru kwa kuvumilia shida wakati matumizi karibu yote ya nyumbani yametumiwa kugharamia elimu yangu. Shukrani za dhati kwa ndugu yangu Godfrey Otieno (Chot Apel) ambaye daima hakuchoka kunitembelea chuoni kunijulia hali na kunitia shime, yeye akifahamu maisha chuoni hayakuwa mepesi kama ambavyo wengine walivyofikiria.

Ninawashukuru wanadarasa wenzangu Kathoki Mutie, Nyamberi Magoma, Kariuki Waithira, Omwoyo Osiemo, Kilelu Mwailengo na Omondi Osano tulioabiria pamoja kwenye merikebu ya usomi na kwa kunipa fursa ya kutaalamika kutokana na mijadala tulioahiriki pamoja na ambayo ilinifaa sana. Wengi wao walikuwa marafiki ambao walirahisisha maisha chuoni. Pia

sitamsahau mwanadarasa mwenzangu kutoka China Du Shun Fang ambaye mwanzoni tulitiana moyo kuendelea na safari hii naye akavunja ahadi yake akajiuzulu njiani. Upande wa isimu, kulikuwa na Mbugua Getingo na Wambui Njagi. Bila wao kungekuwa na upweke usioelezeka.

Namshukuru Beatrice Wambugu ambaye alichukua muda wake kutatua tatizo la kutoleweshwa nakala za sura kadhaa za kazi hii kabla ya kupelekwa kwa wasimamizi.

Shukrani tele kwa Dkt. Francis Eshun wa chuo kikuu cha Wisconsin, Madison kule Marekani kwa kuchukua muda wake mwingi usiku na mchana akichora vielelezo tungo kwa mtambo wa kompiuta. Namwomba awe na moyo huo huo daima dawama.

Asilani si nia yangu kusahau upendo wa Bi. Illuminata Kimeu ambaye alijitoa mhanga kuipiga chapa kazi hii kwa weledi mwingi na moyo mkunjufu.

Juhu di zake hizo zilichangia vikubwa kufanikisha na hatimaye kukamilika kwa tasnifu hii kwa wakati ufaao.

Shukrani maalum ni kwa mke wangu mpenzi Pauline Nkatha Olali kwa kuwa mshirika mwema wa shida na ugumu wote niliopitia, na kwa kunikubalia kutotangamana nao wakati nilipokuwa nimechukuliwa na andao la kuiandika kazi hii. Sitamsahau mtoto wangu Bill ambaye kila mara aliponitembelea

chuoni na kunipata ninapumzika sisomi, atasema, "Baba, mbona unapumzika tu hausomi ! "Ushauri wake kila mara unanikumbusha mwito wa Dkt. May Lenna Balisidya:

Kama Ukiamua kutenda  
jambo si vizuri kuliachia  
katikati sharti ulifanye  
na ulikamilishe.

( Mulika na 19 uk.vi)

Naogopa kosa la kumsahau Bw. Bob Okoth, mhariri msimamizi wa gazeti la 'Taifa' linalochapishwa na kampuni ya 'Nation Newspapers Limited' Kwa kunitengea ukurasa wa 12 kila Jumamosi kuchapisha makala yangu ya isimu na hivyo kunipa moyo wa kuutalii zaidi ulimwengu wa isimu. Hiyo kwangu mimi, ni heshima kubwa.

Natoa shukrani kwa chuo kikuu cha Nairobi kwa kunipa nafasi ya kufanya shahada ya Master of Arts (M.A) licha ya nafasi chache zilizoko.

Namshukuru Mungu mweza vyote kwa kunipa uzima ili nifikie kiwango hiki. Kwenu nyote, nasema:

*Nyasaye Nyakalaga ogwedhu duto.*

# ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA

E.....	Kielezi
KBN .....	Kibainishi
KIH .....	Kihusishi
KIO .....	Kionyeshi
KIU .....	Kiunganishi
KIV .....	Kivumishi
KIW .....	Kiwakilishi
KL .....	Kikundi Leksika
KMK.....	Kiambishi Kitangulizi
KMV.....	Kanuni Muundo Virai
KE .....	Kikundi Kielezi
K.KIH .....	Kikundi kihusishi
K.KIV .....	Kikundi kivumishi
K.N .....	Kikundi nomino
KT .....	Kikundi Kitenzi
MN.....	Miundo nje
MZ.....	Mzizi
N.....	Nomino
n.k.....	na kadhalika
N̄.....	'N-bar'
S.....	Sentensi
SB .....	Sarufi bia
SH .....	Shamirisho

SMV .....	Sarufi Muundo Virai
SPEC .....	'Specifier'
SZGM .....	Sarufi zalishi Geuzamaumbo
T .....	Kitenzi
UD .....	Umbo ndani
UF .....	Umbo kifonetiki
UM .....	Umilikifu na Masharti
UMT .....	Umbo kimantiki
VN .....	Vikundi nomino
WG .....	wingi
$\bar{X}$ .....	'X-bar'
$\alpha$ .....	Alpha, ikiashiria idadi
$\beta$ .....	Beta, ikiashiria jinsiya
$\theta$ .....	Theta, ikiashiria 'agiumenti ya'
$\gamma$ .....	Gamma, ikiashiria uhusika
$\emptyset$ .....	Mofimu kapa, ikiashiria udondoshaji
{ a,b,c ..... }	fungu lenye elementi a,b,c .....
n (A) .....	idadi ya elementi katika fungu A
*	si sawa kisarufi.



# DIBAJI

Matlaba ya tasnifu hii ni kufanya uchanganuzi wa kiufafanuzi wa kikundi nomino cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar' Katika kiolezofaridi cha nadharia ya sarufi geuzamaumbo sanifu panuzi.

Tumeibawibu kazi hii katika sura tano. Katika sura ya kwanza, tunatoa maelezo ya kimsingi yanayohusu kikundi nomino cha Kiswahili. Aidha, sura hii inaeleza somo la utafiti, madhumuni ya utafiti na upeo wa tasnifu. Mambo mengine ambayo yanaangaliwa ni pamoja na sababu za kulichagua somo, kikundi nomino kikiwa ni maarubu yetu, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

Sura ya pili inachunguza mofolojia ya nomino ya Kiswahili. Unyambuaji na uambishaji ni dhana zinazopewa nafasi kubwa katika sehemu hii. Ngeli za nomino zinachanganuliwa na upatanisho uliopo.

Sura ya tatu inahusu uvumishaji wa nomino na kategoria tofauti za kisintaksia zinazohusiana na kikundi nomino. Kiini cha sura hii kiliangaza, hususan, maneno mbalimbali yanayovumisha nomino katika lugha ya Kiswahili.

Sura ya nne inachunguza kwa tafsili kikundi nomino cha Kiswahili. Mifumo miwili ya kuwakilisha miundo ya kategoria inatumika. Mifumo hiyo ni kiunzi

cha sarufi muundo virai na kiunzi cha 'X-bar'.

Hata hivyo mfumo wa sarufi muundo virai ulitumika tu kama msingi na kitangulizi cha sintaksia ya X-bar ambayo tumeitumia kukichanganua kikundi nomino cha Kiswahili.

Sura ya tano ni hitimisho jumuishi ambapo matokeo ya utafiti wetu yanaelezwa. Nadharia tete zetu zinaangaliwa na mapendekezo yanatolewa kuhusiana na kipengele cha sintaksia, hususan kikundi nomino cha Kiswahili.

Katika sura hii, mwanzo kabisa tunatoa maelezo ya kimsingi yanayohusu dhana ya kikundi Nomino. Baadaye tunaeleza kwa tafsili somo la utafiti, madhumuni ya utafiti na upeo wa tasnifu.

Mambo mengine ambayo yamejadiliwa katika sura hii ni sababu za kulichagua somo, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

Maelezo mbalimbali yametolewa kuhusu kikundi nomino, dhana tunayoshughulikia, nasi tulitathmini maelezo hayo kabla ya kujitokeza na ufafanuzi ulio mahususi.

Hartmann na Stork ( 1955) wanaeleza kikundi nomino kama:

Neno au kundi la maneno  
ambalo lina nomino au kiwakilishi  
kama neno kuu linalofanya kazi  
ya nomino kama kiima, yambwa  
au shamirisho katika sentensi.<sup>1</sup>

( Tafsiri ni yetu)

Kwa mujibu wa Kamusi sanifu ya isimu na lugha ( 1990), kikundi nomino ni:

kikundi ambacho hufanya kazi ya nomino. <sup>2</sup>

Jacobs na Rosenbaum (1968) wanaongeza kusema kwamba aghalabu huwa kuna kanuni mbili za kimsingi zinazoeleza kikundi nomino.<sup>3</sup> Moja ya kanuni hizo zinasema kwamba kikundi nomino kinaweza kikawa na nomino pekee;  $KN \rightarrow N$ . Kanuni nyingine ni kuwa kikundi nomino kinaweza kikawa ni kibainishio pamoja na nomino,  $KN \rightarrow Kbn, N$ . Kanuni zote mbili zinaweza zikawekwa kama moja zikaonyesha uwezekano wa kila mojawapo;

$$KN \rightarrow \left\{ \begin{array}{l} Kbn, N \\ N \end{array} \right\}$$

Maelezo hayo ya Jacobs na Rosenbaum (Ibid) hayajitoshelezi kwa namna ambavyo wamejifinya, na kama ambavyo tulivyoona, kikundi nomino kinapanuka zaidi kinyume na kama wanavyotueleza.

Culicover (1976) anatoa ufafanuzi kuhusu kategoria sintaksia. Kwamba, ikiwa kategoria sintaksia imebeba neno moja pekee, hiyo inakuwa kategoria leksika.<sup>4</sup> Pale ambapo imebeba kundi la maneno, inakuwa kategoria kirai. Kategoria inayobeba kikundi nomino, kibainisho cha nomino, kibainisho pamoja na kivumishi cha nomino ni kikundi nomino.

Pei (1966) anasema hivi kuhusu kikundi nomino:

Ni neno au kundi la  
maneno linalofanya kazi  
kama nomino.<sup>5</sup>

Katika kutathmini kauli zilizotolewa, tunaona kuwa maelezo yote yanatupa mwelekeo fulani kuhusu kikundi nomino.

Maelezo ya Hartmann na Stork(Ibid) yanajikita katika dhana ya kikundi nomino na vipengele vya nomino au kiwakilishi kama jambo la kimsingi. Haya ni maelezo muhimu kwa sababu nomino katika sentensi hutekeleza wajibu wa kusimamia dhana za yambwa, kiima na shamirisho.

Takriban, maelezo ya Kamusi sanifu ya isimu na Lugha (Ibid) hayatofautiani sana na maelezo ya Hartmann na Stork (Ibid) ila tu yalikosa kueleza kazi inayotekelezwa na nomino kama vile yambwa; kiima na shamirisho.

Mawazo ya Rosenbaum na Jacobs (Ibid) yanajitosheleza kwa kiasi. Yote yanajikita katika kipashio muhimu cha vipengele vya kikundi nomino na kanuni zilizopo. Kama ambavyo tulivyosema awali, kanuni hizo wanazozitoa si kamili. Katika lugha ya Kiswahili tuna kategoria mbili; kategoria leksika na kirai. Katika kategoria leksika tunapata:

$$\begin{array}{c} ( T ) \\ \left. \begin{array}{c} N \\ E \end{array} \right\} \\ | KIO | \\ | KIW | \\ ( KIV ) \end{array}$$

Katika kategoria ya virai tunapata;

$$\begin{array}{c} ( KN ) \\ \left. \begin{array}{c} KT \\ KKIV \end{array} \right\} \\ | KE | \\ ( S ) \text{ n.k.} \end{array}$$


Ufafanuzi wa Culicover (Ibid) unatupa mwanagaza zaidi kuhusu kikundi nomino kwa vile anaanza kwa kutupa msingi wa dhana hii. Hata hivyo, hatuelezi baadhi ya vipengele ambavyo vimo katika kikundi nomino, ambavyo ni baadhi ya azimio tulilionalo katika kazi hii.

Maelezo ya Pei (Ibid) yanalingana na mawazo ya Hartmann na Stork (Ibid). Anasisitiza kwamba kikundi nomino kinaweza kikawa ni neno moja tu, kama kategoria leksika, au zaidi ya neno moja, kama kategoria kirai.

Tukipiga hatua kidogo, maelezo ya kategoria ya KN yanaweza yakawa ya kimuundo, kisarufi au kisemantiki.


Kimuundo, katika umbo msingi, KN ndicho kategoria mwenzi ya KT ambapo KN na KT vinapatikana chini ya mawanda ya S, na mwenzi kwa T- ambapo kitenzielekezi - chini ya mawanda ya KT. Mchoro huu (1) hapa chini unafafanua maelezo ambayo tumeyatoa hapo juu.

(1)



Kisarufi, KN kinaweza kuelezwa kama kategoria ambayo uamilifu wake ni kufanya kazi ya kiima au yambwa ya kitenzi. Mchoro huu (2) hapa chini unafafanua maelezo haya:


2)



Kisemantiki, KN ndicho kategoria inayoweza ikafanya kazi kama agiumenti na chini ya KT, tunakuwa na kitenzi na KN kama agiumenti chini ya KT.

Mchoro (3) hapa chini unafafanua maelezo haya:

(3)



Baada ya kuangalia fasili za wataalamu mbalimbali wa isimu na kuona namna ambavyo fasili hizo zinakaribiana, sehemu inayofuata itashughulikia somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, upeo wa tasnifu, sababu za kulichagua somo, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

### 1.1.0

### SOMO LA UTAFITI

Kazi hii ni jaribio la kufanya uchanganuzi wa kiufafanuzi wa KN cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar' katika kiolezofaridi cha nadharia ya sarufi geuzamaumbo panuzi.

Kiini cha utafiti huu kilikuwa ni kutumia sintaksia ya 'X-Bar' katika



kuchanganua KN cha Kiswahili, na katika kufanya hivi, tulikuwa vilevile tunafanya jaribio la kuthibitisha iwapo madai ya nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar' kuhusu miundo ya lugha asilia yana mashiko yoyote au la.

Kwa muhtasari, tulichanganua na kufafanua KN cha Kiswahili kisintaksia kwa usaidizi wa nadharia hii na hivyo kuweza kuthibitisha madai yake, baada ya kuiangalia.

Sintaksia ya 'X-Bar' inadaid kwamba katika kiunzi chake, inawezekana kukatokea hali kuwepo kwa zaidi ya kirai kimoja cha kategoria leksika  $X^0$ .<sup>6</sup> Hivi ni kusema kwamba katika kiunzi hiki, tunaweza tukapata kategoria zifuatazo:

(i)  $X$  (au  $X^0$ ) = Kategoria leksika  $X^0$

(ii)  $\bar{X}$  (au  $X^1$ , 'X-Bar' au 'X-bar moja')


(iii)  $\bar{\bar{X}}$  (au  $X^2$ , 'X-bar mbili')

(iv)  $\bar{\bar{\bar{X}}}$  (au  $X^3$ , 'X-bar tatu')

Kila kategoria ya 'bar' inaoana na kategoria leksika  $X^0$  na inaitwa 'uvurumishaji wa bar'.<sup>7</sup> Hivyo basi, tulidhamiria kuthibitisha iwapo muundo huu (KN cha Kiswahili) una kategoria leksika na kategoria kirai. Kabla ya kutoa mifano yetu, tunatoa maelezo machache kuhusu  $\bar{X}$ , ambayo kwa mara nyingine yameelezwa kwa undani sana katika sura ya nne ya kazi hii.


Jambo muhimu kuhusu KN ni kwamba viambajengo vyake vinategemea nomino kuu. Leksika kuu  $x^0$  na shamirisho yake kwa pamoja zinaunda kiambajengo  $\bar{X}$  na kiambajengo  $\bar{X}$  pamoja na kibainishi<sup>8</sup> chake kinaunda  $\bar{\bar{X}}$ . Ishara ya  $X^0$  kwa hivyo inawakilisha makundi ya kategoria leksika ambayo yanaweza yakawa kiini cha virai- kitenzi (T), nomino (N) , Kivumishi (KIV), Kiwakilishi (KIW) na kielezi (E). Nadharia ya  $\bar{X}$  kwa hivyo inatupa ujumla wa muundo kirai utakaotumika katika kazi hii:

(4)




Nao muundo wa kishazi wa nadharia ya  $\bar{X}$  ni:

(5)




Ambapo  $X^0$  inasimamia shamirisho. Mchoro tutakaotumia kuthibitisha iwapo muundo huu (KN) una kategoria ya kati, baina ya kategoria leksika na kategoria kirai ni huu hapa chini:

(6)




Na iwapo kibainishi kitatangulia tunakuwa na mchoro kama huu:

(7)



Isitoshe, kama tunavyofahamu ni kuwa, katika mfumo uliotangulia wa SMV, Mvulana Mzuri sana sio, wala haijengi kiambajengo kama tunavyoona katika kielelezo tungo kifuatacho:

8)



Tunashughulikia kujua iwapo ni kweli kuwa kirai mvulana mzuri sana ni kiambajengo, hivi kwamba ni kidogo kuzidi KN na ni kubwa zaidi ya KL na hivyo ni kiambajengo ambacho kinapaswa kuelezwa kama kiambajengo huru, ambacho kinajisimamia, mbali na viambajengo hivi viwili.

Kielelezo tungo (8) kinaonyesha viambajengo viwili, kategoria leksika kama vile 'mvulana' na kikundi nomino 'mvulana mzuri sana'. Katika SMV, kategoria mbili ndizo zinazotambuliwa:

- (i) Kategoria leksika kama
- $$\left( \begin{array}{c} N \\ T \\ KIV \\ E \\ KIO \\ KIW \end{array} \right)$$
- (ii) Kategoria virai kama
- $$\left( \begin{array}{c} KN \\ KT \\ KKIV \\ KE \\ S \end{array} \right)$$

Hakuna kategoria za kati kubwa kuzidi neno au ndogo kuzidi kirai. Hakuna kategoria ya kati iliyo kubwa kuzidi nomino au labda ndogo kuzidi KN. Kulingana na SMV, kiambajengo cha nomino sharti kiwe N au KN. Lakini kuna ithibati ya ujarabati kwamba viambajengo hivyo vya kati vipo.

Chomsky (1968)<sup>9</sup> alipendekeza mfumo wa sintaksia ya 'X-Bar' kutoa uhusiano kati ya KN na KT. Hata hivyo, mfumo huu unafanyiwa mabadiliko ili kuwepo na uhusiano kati ya KN na S katika kiolezofaridi cha sarufi

uhusika. Uhusiano huo unaelezwa hivi: <sup>10</sup>

a.  $\bar{X} = [Kbn \bar{X}] \bar{X}$


b.  $\bar{X} = X \bar{N} \bar{N} \dots\dots\dots$

a.  $\bar{N} = [Kbn \bar{N}] \bar{N}$

b.  $\bar{N} = N \bar{N} \bar{N} \dots\dots\dots$

a.  $\bar{V} = [Kbn \bar{V}] \bar{V}$

b.  $\bar{V} = V \bar{N} \bar{N} \dots\dots\dots$



KN = KIO N

NOM = N KN KN

S = KIV KIH

KIH = T KN KN

Maelezo hayo yanaweza kufanywa kimuhtasari hivi:

- a)  $\bar{X} = S, KN$
- b)  $\bar{X} = KIH, \text{ Nomino}$
- c)  $X^0 = K, N$
- d)  $[Kbn \bar{X}] = KIV, KIO$

Radford (1981: 93) anasema hivi, kwa kifupi, ni kasoro ya namna hii ndivyo sintaksia ya 'X-Bar' inajizatiti kurekebisha.

(Tafsiri ni yetu)

Je, kuna lolote la kurekebisha? na je, sintaksia ya 'X-Bar' inairekebisha?

Haya ndiyo baadhi ya maswali tuliyonayo akilini.

Allerton Cook (1969:84) anasema hivi kuhusu kirai:

.....wakati wanaisimu  
wanazungumzia 'Kirai',  
wanamaanisha shada ya maneno  
ambayo yameumbika katika  
makundi yaliyolizunguka umbo  
la neno kuu.

(Tafsiri ni yetu)

Kwetu sisi, 'umaumbo wa neno kuu' utakuwa ni nomino na hivyo basi, kupanuka kwa neno kuu hadi KN. Hii ilihusisha kujaribu kutafuta na kueleza njia mbalimbali ambazo maneno yanaweza yakawekwa pamoja kujenga VN hivyo. Kwa mintarafu hii, tulidhamiria mambo yafuatayo kuhusu KN cha Kiswahili:

- i) Kuthibitisha madai ya sintaksia ya 'X-Bar' kuhusu uwezekano wa kuwepo na kiambajengo kingine mbali na kategoria leksika na kirai nomino.
- ii) Kueleza kwa fasili muundo wa KN cha Kiswahili. Tulidhamiria kuonyesha viambajengo vya KN na kujadili mpangilio wao kulingana na nomino au neno kuu, tukizingatia vionyeshi, vivumishi, idadi n.k.
- iii) Kuchunguza ili kugundua na kueleza sheria ambazo kwazo VN vinajengeka. Hizi ndizo sheria ambazo mzungumzaji asili wa lugha fulani anaelewa na zinampa uwezo wa kujua iwapo KN kimeundwa vizuri au la.

- iv) Kujadili uambishaji na unyambuaji wa nomino ya Kiswahili.

### 1.3.0

### UPEO WA TASNIFU

Kiswahili kina lahaja zaidi ya kumi na nane.<sup>11</sup> Lahaja hizi ni nyingi kiasi kwamba ni vigumu kwetu sisi kushughulikia kila moja yazo katika kazi hii. Utafiti wetu ulijikita katika lahaja ya Kiswahili sanifu. Tulichagua lahaja ya Kiswahili sanifu kwa sababu lahaja sanifu ndiyo inayotumiwa na watu wengi zaidi katika maongezi yao na vile vile katika maandishi ikilinganishwa na lahaja nyingine za Kiswahili ambazo watu wachache wanazitumia.

Ile tofauti iliyoko kati ya Kiswahili sanifu na lahaja nyingine ni ndogo, hivyo basi, kazi hii ni wakilishi na matokeo yake yanatarajiwa kusaidia kuelewa lahaja yoyote ile ya Kiswahili.

Kazi hii ilishughulikia KN cha Kiswahili. Tulitazama muundo wa KN, na nafasi ambayo KN kinaweza kikashikilia katika sentensi. Tulijadili KN na kategoria ambazo zinaivumisha.

Tulitumia sintaksia ya 'X-Bar' kwa mujibu wa Radford (1981). Tatizo letu lilifafanuliwa kwa kutumia nadharia hii katika kiolezofaridi cha nadharia ya standard panuzi kama ilivyopendekezwa na Chomsky (1980).

Ingawa upatanifu ni muhimu katika utafiti huu, tuliurejelea ilipotulazimu



lakini hatukuzama kilindini kueleza kwa undani kuhusu kwayo. Hi ni kwa sababu maelezo ya aina hiyo hasa yanajikita katika mofosintaksia na hivyo basi, itazidi upeo wetu huu wa sasa.

Pia hatukujishughulisha na maswala ya sifa kiarudhi zinazohusu tempo, mkazo, kidato, toni na kadhalika. Hivyo, hatukuzitaja, hadi pale tuliposhindwa kuziepuka.

Kwa kiasi kikubwa katika vielelezo vyetu, tulitumia sentensi sahili,<sup>12</sup> na hatushughulikia sentensi ambatano na changamano.

Kwa kuwa bado hakuna ukubaliano kamili juu ya nyingi za istilahi za isimu katika lugha ya Kiswahili, kwa upande wetu tulizitumia kama zilivyo katika Kamusi sanifu ya isimu na lugha (Ibid). Pale ambapo istilahi tofauti ilitumiwa, tulitoa maelezo.

#### **1.4.0 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO**

KN ni kipengele muhimu cha kisintaksia katika lugha yoyote ile kwa sababu ni kategoria kuu ambayo uamilifu wake unajitokeza kama kiima na yambwa. Kwa hivyo, sisi tuliona manufaa makubwa utafiti ufanywe kuhusu KN.

Kadri tujuavyo, kazi yetu ndiyo ya kwanza yenye lengo la kukichambua KN

cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar'. Tulitumai kwamba kazi yetu itaweza kuziba pengo ambalo liliachwa na watafiti waliotutangulia. Kazi hii pia itatoa mchango katika hazina ya tafiti zilizofanywa juu ya lugha ya Kiswahili.

Kazi hii ilisaidia kuthibitisha umuhimu au uwezekano wa nadharia ya 'X-Bar' kufanya kazi katika kutafiti KN cha Kiswahili, na hatimaye kukubalika kwa nadharia hiyo.

Vilevile kwa sababu tulikuwa tunatumia nadharia ambayo imejengeka katika msingi wa lugha nyingine (Kiingereza) ambayo haina uhusiano wa kinasaba na Kiswahili, hii ilikuwa nafasi bora kupiga msasa na kuthibitisha madai yake na hivyo basi kwa kufanya hivi, kuchangia katika kuitathmini.

Tunapendekeza kazi hii iwe kama changa moto na hatua moja zaidi na mchango wa utafiti kuhusu KN cha Kiswahili. Tumaini letu kubwa ni kwamba kazi hii imemulika na kuangaza ufahamu wetu wa KN cha Kiswahili.

### **1.5.0 NADHARIA TETE**

Utafiti wetu ulitathmini nadharia tete zifuatazo; kwamba,

- i) KN cha Kiswahili kinaweza kuchambuliwa kikamilifu kwa kutumia sintaksia ya 'X-Bar'
- ii) KN cha Kiswahili kina viambajengo vya kati, kati ya kategoria

## 1.6.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi mbalimbali zimeandikwa juu ya sarufi ya lugha ya Kiswahili. Kuna kundi la waandishi ambao walishughulikia na kuandikia sarufi ya Kiswahili wakiwa na matlaba ya kuwasaidia wageni kufahamu Kiswahili, wageni waliokuja Afrika mashariki na hata wale waliodhamiria kuzuru eneo hili. Baadhi ya waandishi hawa ni Ashton (1944), Loogman (1965), Polome (1967) na kadhalika.

Kundi jingine ni la wasomi ambao waliandika sarufi ya Kiswahili kwa malengo ya kitaalamu. Katika kundi hili wako Kondo (1967), Maw (1969), Myachina (1973), Othman (1976), Vitale (1981), Kapinga (1983), Mdee(1986) na kadhalika.

Pia kuna wasomi ambao tasnifu zao zinarejelea dhana ya KN katika lugha zingine mbali na vipengele vingine vya sarufi. Wao ni kama vile Kamango(1980), Mwove(1987), Mebo (1989), Ogutu (1989), Owili (1989), Thande(1988), Mgullu (1990), Mweri(1991), Baya (1993) na kadhalika.

Tasnifu ambazo vilevile zinagusia KN ni kama vile Kurgatt(1989), Perez(1985) na Mazrui (1983).

Tulifaidika mno na baadhi ya kazi hizi na tathmini yetu kuzihusu bila shaka itathibitisha dai hili.

Kamango (1980) katika tasnifu ya M.A. ameshughulisha KN katika Ki-Giriama. Anafanya uchanganuzi wa KN cha Ki-Giriama na kategoria zake, muundo virai na ugeunzajimaumbo. Kazi yake ilitufaa sana kwa namna ambavyo anashughlikia lugha ambayo vilevile ni ya kibantu kama Kiswahili. Kipengele cha KN katika sintaksia kinakaribiana katika lugha za kibantu. Ingawa anumia nadharia tofauti na yetu, tuliona jinsi muundo wa virai ulivyojitokeza na hii ilitufaa sana katika kazi yetu.

Mebo (1989) katika tasnifu yake ya M.A alijishughulisha na KN katika lahaja ya Lwisukha, moja ya lahaja za lugha ya kiluhya inayozungumzwa mkabala wa tarafa za Kabras (Kaskazini), Tiriki (Mashariki), Tsotso (Magharibi) na Idakho (Kusini). Anatumia nadharia ya 'X-Bar' katika utafiti wake. Kazi ya Mebo (ibid) ilitusaidia sana kuelewa nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar'.

Lwisukha kama vile lahaja za Bukusu, Kabras, Tiriki, Idakho, Kisa, Tsotso, Wanga, Logooli, Khayo, Nyala K, Nyole, Samia, Marachi, Tachoni, Marama na Nyala B ziko chini ya kiluhya ambayo ni lugha ya kibantu. Hivi basi, lugha ya kiluhya ina sifa za kiisimu zinazoafikiana na Kiswahili ambacho nacho ni kibantu.

Utafiti wake ulitufaidi sana katika kuangalia mofolojia ya nomino ya

Kiswahili, KN cha Kiswahili na sintaksia ya 'X-Bar'

Mwove (1987) katika tasnifu yake ya M.A anaangalia KN cha Kikamba. Sura ya 2,3,na 4 ya tasnifu hii ambayo haijchapishwa ilitufaa sana katika kazi yetu. Katika sura ya 2, anaangalia KN katika lugha nne za kibantu; Kikuyu, Kimbere, Kikuria na Kiswahili. Katika sura ya 3 anashughulikia KN cha kikamba na katika sura ya 4, anatazama mahali pa KN. Ingawa anaangalia KN cha Kiswahili, anatofautiana nasi kwa sababu za kinadharia. Sisi tunajikita katika nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar' naye alitumia SZGM. Hata hivyo kazi hii ilitufaa sana katika kuelewa KN cha Kiswahili.

Mweri (1991) katika tasnifu yake ya M.A anaangalia ubadilishanaji nafasi katika KN cha Ki-Giriama akitumia nadharia ya umilikifu na masharti. Katika kueleza nadharia hii, anataja nadharia nyingine zinazojenga hii nadharia kuu. Moja kati ya nadharia hizo ni 'X-Bar'. Anatoa muhtasari wa nadharia hii. Hivyo basi, tasnifu yake ilitufaa mno katika ile sehemu ya msingi wa nadharia.

Omondi (1982) alishughulikia kundi tofauti la lugha (niloti) na wakati huo huo kutumia nadharia ya 'standard'. Kazi hii pia inachunguza kwa undani vipashio muhimu vya kisintaksia. Omondi (Ibid) anatumia kielelezo cha ugeuzajimaumbo, na ingawa anashughulikia sintaksia, anatoa maelezo ya kimsingi kuhusu fonolojia na mofolojia ya lugha hiyo. Hatimaye anaangalia

sheria za msingi, aina za sentensi, mfanyiko wa viunganishi, urejeshaji, ujalizishaji na kauli ya kutendewa. Kazi yake ilitufana sana.

Kurgatt (1989) katika tasnifu yake ya M.A ameshughulikia kipengele cha ugeuzajimaumbo katika sintaksia ya kinandi. Katika sura ya tatu na nne ya kazi hii, tulifaidika sana kwa vile mbali na kwamba inashughulikia ugeuzajimaumbo, vipashio muhimu vya sintaksia vinajadiliwa na ni moja wapo ya vipengele tunavyoviangalia.


Ogutu (1989) anaangalia na kujadili sentensi za masharti akitumia nadharia ya 'standard panuzi' kama msingi wake wa nadharia na kupiga hatua kidogo na kujiingiza katika nadharia iliyoduruswa ya 'standard panuzi'. katika sura ya 4 ya kazi hii, anashughulikia ugeuzajimaumbo. Anatazama vilevile sifa ya sheria za mugeuzajimaumbo. Kazi yake ilikuwa ya manufaa kwetu sisi, kwa vile ambavyo vile vipengele muhimu katika sentensi vinajadiliwa, sehemu mojawapo tunayoishughulikia.

Perez (1985) katika tasnifu yake ya Phd anatazama kipengele cha ujalizo katika lugha tatu za Kibantu; Kikuyu, Kirundi na Kishona akitumia mkabala wa nadharia ya umilikifu na masharti ambayo ni nadharia ya kisasa katika kazi hii. Anashughulikia ubadilishanaji nafasi wa KN, hivyo kazi yake ilikuwa ya manufaa kwetu. Hata hivyo, Perez (Ibid) hashughulikii muundo wa KN ambao ni sehemu muhimu sana katika kazi yetu.


Mazrui (1993) pia alikuwa wa manufaa katika kazi yetu kwa sababu anajadili vipashio muhimu vya kisintaksia katika lugha ya Kiswahili. Ingawa kazi hii inatumia nadharia tofauti ya 'standard' ilitupa mwangaza na mwelekeo kuhusu kauli ya kutendewa. Mazrui (Ibid) anatoa maelezo kuhusu KN na pia KT katika sentensi naye tulimtegemea katika kuchambua vipashio muhimu katika sentensi.

Baya (1993) katika tasnifu yake ya M.A amechunguza kitenzi kisaidizi cha Kiswahili kwa mtazamo wa SZGM. Katika sura ya pili, amechunguza KN cha sentensi ya Kiswahili kama msingi wa kuelewa kisaidizi cha kitenzi cha sentensi ya Kiswahili. Anaeleza kuwa KN cha Kiswahili kinaweza kuwa na N, KIW, KIV, KIO au vipengele hivi zaidi ya moja.

Ingawa anatumia zile kategoria zilizoko katika KN, anatumia nadharia ya SZGM katika kuchanganua KN kinyume na sisi ambao tumetumia sintaksia ya 'X-Bar' ambayo inashikilia kuwepo na kategoria zaidi ya mbili mbali na kategoria ya leksika (nomino) na kategoria ya KN. Ingawa anatumia kuwa nomino ndicho kichwa cha KN kwa kuurejelea ule mfumo wa SMV, anatoa mfano huu:



Hata hivyo, katika sintaksia ya 'X-Bar' maelezo hayo hapo juu yatawakilishwa hivi:





Katika mchoro wa pili unaozingatia sintaksia ya 'X-Bar' tunaona kiambajengo cha tatu ambacho kinawakilishwa na  $\bar{N}$ . Hii  $\bar{N}$  haipo katika mfumo wa sintaksia ya SMV. Hata hivyo, kazi ya Baya (Ibid) ilitufaa sana kwa vile ambavyo muundo wa KN ulivyoshughulikiwa na vile vipengele vyote vinavyokijenga.

Vitale (1981) amefanya uchunguzi juu ya lugha ya Kiswahili kwa kutumia nadharia ya SZGM. Ametumia nadharia ya Chomsky (1965), lakini pia na nyongeza fulani zilizoendelezwa na watu kama vile Bowers (1973), Fillmore (1968), Edmonds (1970) na Chomsky (1970). Kazi ya Vitale (Ibid) ilikuwa ya manufaa kwetu maana tulitegemea sana nadharia yake kama msingi wa nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar' ambayo imejikita humo. Nadharia yetu hata hivyo ilijikita katika Radford (1981) bila nyongeza yoyote kama tulivyokwisha sema. Vitale (Ibid) katika kazi yake anajadili muundo wa sentensi katika Kiswahili. Anataja KN na vipengele vyake, na katika kuvitaja vipengele hivi, aliweza kwa kiwango kikubwa kueleza kwa tafsili muundo wa KN cha Kiswahili.

Mgullu (1990) alichanganua aina tofauti za sentensi za Kiswahili. Ingawa anatumia nadharia tofauti na yetu, kazi yake ilitufaa mno kwa vile alivyochambua KN cha Kiswahili. Sisi tuliegemea sana uchanganuzi wa sentensi sahihi za Kiswahili naye ameshughulikia sentensi hizi sahihi. Hii sehemu ya kazi yake ilikuwa ya manufaa kwetu sisi.

Ashton (Ibid), Polome (Ibid) na Loogman (Ibid) waliandika juu ya karibu sarufi yote ya Kiswahili. Uchambuzi wa Ashton (Ibid) umehitimisha kwamba tungo nomino za Kiswahili zaweza kugawanyika katika sehemu mbili.<sup>13</sup>

- i) Tungo nomino zenye kitenzi-KUWA
- ii) Tungo nomino zisizo na - KUWA, bali zina KOPULA<sup>14</sup> 'ni' na kadhalika.

Wanasema kuwa kimsingi, - KUWA ni kipashio kimojawapo cha Kopula katika tungo nomino. Ili kutofautisha kiumbo, tungo nomino zisizo na-KUWA hujengwa na 'vitenzi -ungio' kama vile 'ni' na kadhalika. Jambo la msingi hapa ni kwamba kitenzi-KUWA na vitenzi-ungio, vyote ni Kopula, zinazofanya kazi ya kutambulisha tungo nomino za Kiswahili.

Maelezo haya yalitufaa sana hasa tulipokuwa tukitoa mifano katika sura ya nne kuhusu sentensi sahili.

Fauka ya kuwa wataalamu hawa hawakuiangalia lugha au KN kwa kutumia nadharia yoyote, wengine tuliowataja mwanzoni, ingawa tumefaidika sana na kazi zao, na pia kutokana na hayo ambayo tumeyasema hapo juu, tunadhani ya kuwa kazi yetu ni ya uasisi.

## **1.7.0 MSINGI WA NADHARIA**

Katika faslu hii, tunaeleza nadharia tunayoitumia katika kazi yetu. Sarufi

Zalishi Geuzamaumbo (SZGM) imekuwa kipaumbele kwa wanaisimu wengi hasa katika miaka ya sitini na sabini. Mwasisi wa nadharia hii ya SZGM alikuwa Noam Chomsky (1957)<sup>15</sup> alipoiwasilisha mara ya kwanza katika Syntactic Structures na baadaye ikaendelezwa katika Aspects of the Theory of Syntax (1965).

Lengo kuu la nadharia ya isimu kama ilivyofafanuliwa na Chomsky katika Syntactic Structures lilikuwa ni kueleza sintaksia; sheria za kisarufi zinazojenga sentensi. Lakini katika Aspects of the Theory of Syntax, dhamira ilipanuka hivi kwamba matlaba ilikuwa ni kueleza mahusiano yaliyopo ya kiisimu kati ya mfumo wa sauti (Kitengo cha Kifonolojia ) na mfumo wa maana (Kitengo cha Kisemantiki). Haya yalielezwa kwa kutumia nadharia ya semantiki ambayo ilikuwa imeasisiwa na Katz na wengine (1964) na ugeuzajimaumbo ulihifadhi maana. Kulikuwepo na uimarishaji kama unavyoonekana kutoka kwa Bornstein (1977:24)

Kipengele cha sintaksia ni changamano kuzidi vipengele vya isimu vya awali, na hata namna ambavyo sintaksia ilivyoangaliwa. Inagawanyika katika msingi, ambayo imebeba kanuni muundo virai na msamiati (orodha ya mofimu na maneno), na kipengele cha ugeuzajimaumbo. Kule kuongezwa kwa msamiati kuliwezesha kurahisishwa kwa kanuni muundo virai, kwa vile havikulazimika kuelezea uteuzi wa maneno.

(Tafsiri ni yetu)

Katika kazi hizi zilizotangulia za (1957) na (1965) hapo juu, muundo wa sentensi uliwakilishwa na mfumo uliojulikana kama 'sintaksia muundo virai'.


Katika Syntactic Structures, kipengele cha muundo virai ni moja kati ya sehemu tatu ambazo zinaunda sarufi. Katika Aspects of the Theory of Syntax, hizi kanuni sasa zinapatikana katika kipengele cha sintaksia changamano, katika sehemu ya msingi.

Allerton (1979:79-80) anasema:  
sarufi muundo virai(SMV)  
zimepewa umuhimu mkubwa  
kwa sababu ya sifa zao za  
kupata utoshelevu wa ufafanuzi  
kupitia upatanisho wa kanuni  
na vielelezo matawi(kupitia  
unyambuaji). Zina umaalumu  
na hivyo basi zinahitajika katika  
kufafanua lugha asili ya binadamu.


(Tafsiri ni yetu)

Katika Chomsky (1965) nadharia ya 'standard' ilianguka sarufi kama ilivyoundwa na vijenzi vitatu.

Vijenzi hivi tayari vimetajwa katika sehemu ya mwanzo wa msingi wa nadharia. Mchoro ufuatao unawakilisha namna vitengo vya kifonolojia, semantiki na kisintaksia vinavyojitokeza na kuhusiana.



Kitengo cha kisintaksia huwa na sehemu msingi na kipashio cha ugeuzajimaumbo. Sehemu msingi ya kitengo cha kisintaksia ni mfumo wa sheria ambao huzalisha seti iliyofinywa ya mikufu msingi kila mmoja ukiwa na ufafanuzi maalum wa kimuundo unaoitwa kielelezo tungo msingi. Vielelezo tungo msingi hivi ndivyo vipashio vya kimsingi ambavyo hujenga umbo wa ndani katika sentensi. Sehemu msingi pia huwa na leksikoni (msamiati). Msamiati ni seti ya maneno yasiyopangwa na yasiyokuwa katika muktadha maalum na sheria za uziada. Sheria hizi za uziada zinahusika katika upangaji wa maneno ili kusiwe na urudijirudijaji pale ambapo si lazima. Vielelezo tungo vinavyozalishwa na sehemu msingi huchukua umbo lifuatalo.



Msamiati huwekwa katika sehemu ya chini ya michoro hii ili kuunda umbo ndani la sentensi. Kitengo cha ugeuzajimaumbo huwa na kanuni ugeuzajimaumbo ambazo zinaweza kuondoa, kuongeza, kubadili nafasi na kadhalika.

Kitengo cha kisemantiki hudhihirisha fasiri ya kisemantiki ya sentensi, yaani huhusisha muundo uliozalishwa na kitengo cha kisintaksia na mawasilisho fulani ya kisemantiki. Katika nadharia 'standard', fasiri ya kisemantiki ilifanywa katika kile kiwango cha umbo ndani. Hata hivyo, arki fulani za umbo nje zinaweza kuwa mwafaka katika kufanya fasiri ya kisemantiki. Ni wazi basi kwamba vitengo vya kifonolojia na vya kisemantiki ni vya kiufasiri.

Kwa mintarafu hii, sarufi ina jukumu mahsusi ambalo limeelezwa kwa kifupi na Chomsky(1965) kwamba:

Athari ya mwisho ya sarufi,  
hivyo basi, ni kuhusisha  
ufasiri kisemantiki na ufasiri  
Kifonetiki, yaani, kuelezwa  
namna ambavyo sentensi  
inavyofasiriwa. Uhusiano huu  
unahusishwa na kitengo cha  
sintaksia ya sarufi ambacho kinabeba  
sehemu inayotenda majukumu muhimu'  
(Tafsiri ni yetu)

Crystal (1971) ana maoni kama hayo kwamba:

katika 'Aspects' sarufi ya lugha inachukuliwa  
kama mfumo wa kanuni unaohusisha maana ya  
sentensi inayozalishwa na sauti.

(Tafsiri ni Yetu)

Tunapoziangalia Syntactic Structures (1957) na katika kiunzi cha 'standard'  
(1965) tuliona kuwa kiunzi cha 'standard' ni mfano ulioimarishwa na  
kufanyiwa ukarabati wa Syntactic Structures na katika kiunzi cha 'standard'  
mabadiliko yafuatayo yanaweza kuonekana.

1. Kitengo cha semantiki sasa ni sehemu muhimu ya sarufi.
2. Ufasiri kisemantiki unafanywa katika umbo ndani.
3. Sifa ya uchamko wa sarufi inaweza kuelezwa chini ya kanuni muundo  
virai katika msingi na wala sio kwa kutumia kanuni za kijumla  
ugeuzajimaumbo (kama ilivyo katika Syntactic Structures).
4. Kwa mintarafu ya (3) hapo juu, 'Aspects' haina kanuni za kijumla za  
ugeuzajimaumbo.
5. Sentensi za msingi hazina hadhi ya kujitosheleza au kujitegemea katika

sarufi.

Hii nadharia ya 'standard' ilifanyiwa ukarabati na kukazuka nadharia ya 'standard panuzi'. Dhamira kuu ilikuwa ni kupata utoshelevu kiuteuzi. Nadharia ya 'standard' kwa kutilia maanani kanuni za ugeuzajimaumbo ingeweza kufaulu kupata utoshelevu kiuteuzi. Nadharia mpya ya 'standard panuzi' ilianzisha nadharia ya 'X-Bar.' Nadharia hii ilidurusiwa na nadharia nyingine ikajitokeza ya 'standard panuzi iliyodurusiwa' ambayo hujulikana kama umilikifu na masharti.

Katika kazi zake, kwa mfano (1972), Chomsky anapendekeza nadharia ya 'standard panuzi' ikiwa ni udurusu au marekebisho ya kielelezo cha 'standard'. Nadharia hii inaamini kuwa maana yote haijitokezi katika muundo wa ndani na kwamba sehemu fulani ya maana inaathiriwa na muundo wa nje. Hivyo basi, chini ya nadharia ya 'standard panuzi' maana ya kisemantiki inapatikana kutokana na kanuni za ufasiri ambazo zinafanya kazi katika miundo ya nje. Mfumo ambao Chomsky anautumia katika nadharia ya 'standard panuzi' ndio umekuja kujulikana kama sintaksia ya 'X-Bar'.

Hii vilevile ndiyo nadharia ambayo madai yake utafiti wetu ulijaribu kushughulikia kwa kutumia KN cha Kiswahili. Sintaksia ya 'X-Bar' inashutumu sintaksia muundo virai kwa sababu mbili:



i) Kwamba sintaksia muundo virai inajifinya sana kiasi kwamba ni kikwazo kwa idadi ya namna mbalimbali za kategoria inayoruhusu.


ii) Kwamba sintaksia muundo virai haizui au kusonga idadi ya seti ya kanuni muundo virai zinazoweza kukubalika.

(Radford 1981:91)


Katika sintaksia ya muundo virai aina mbili za kategoria zinaruhusiwa:

- i) Kategoria ya leksika kama vile N, KIV.KIW, T, E, SH, KBN, na kadhalika.
- ii) Kategoria kirai kama vile KN, KT, K.KIV, KIW, KE na kadhalika.

'X-Bar' inadai kwamba kategoria kama hizo na wafuasi wake wanaonyesha hivi kwa kutumia mfano wa Kiingereza.



Kielelezo tungo hicho hapo juu kinawakilisha sentensi hiyo kwa mujibu wa ule mfumo wa SMV. Lakini sintaksia ya 'X-Bar' kwa sababu inawajibika kutambua kategoria za kati zinazopatikana kati ya kategoria za leksika na kategoria ya virai, inadai kuwa mkufu 'very tall girl' unajenga kiambajengo ingawa kielelezo tungo kilichoko hapo juu hakidhihirishi hili. Hivyo basi, sintaksia ya 'X-Bar' inaonyesha muundo wa KN 'this very tall girl' kama ifuatavyo:



Kirai 'very tall girl' kinawakilisha aina moja ya kategoria ya kati kubwa kuzidi N, lakini ni ndogo kuzidi KN na kuthibitisha iwapo hiki hasa ni kiambajengo, ithibati za kijarabati zinatolewa kama tutakavyoona hivi punde.


Sintaksia ya 'X-Bar' inaweka 'msichana mrefu sana' kama kiambajengo na hivyo kategoria ambayo sasa inajulikana kama  $\bar{N}$  au 'N-bar'. Kwa muhtasari, sintaksia ya 'X-Bar' inatambua kwamba upo upanuzi au uvurumishaji wa ziada wa kirai kimoja cha kategoria leksia  $X^0$ . Kwa hivyo, kiunzi hiki kwa mujibu wa Radford(1981:93) kina aina za kategoria zifuatazo:

- (i)  $X$  (au  $X^0$ )=Kategoria leksika  $X^0$
- (ii)  $\bar{X}$  (au  $x^1$ , 'X-Bar' au 'X-bar moja')
- (iii)  $\bar{\bar{N}}$  (au  $X^2$ , 'X-Bar mbili')
- (iv)  $\bar{\bar{\bar{N}}}$  (au  $X^3$ , 'X-Bar tatu')
- (v) n.k

kila mojawapo ya kategoria ya 'bar' inayoafikiana na kategoria leksika  $X^0$  inajulikana kama 'uvurumishaji' wa  $X^0$ . Njia moja ya kuangalia tofauti iliyoko kati ya sintaksia ya muundo virai na sintaksia ya 'X-Bar' ni kwamba SMV ni sura nyingine ya 'X-Bar' ambayo inaweka sharti kuwa uvurumishaji wa 'bar' ya kategoria yoyote ile ni moja (kwa sababu katika SMV, kuna kuvurumishwa kwa kirai kimoja tu katika kategoria yoyote).

Kwa sababu hii, sintaksia ya 'X-Bar' inajizatiti kuondolewa kwa muundo virai na kategoria zake za X na KX na mahali pake kuchukuliwa na zile za sintaksia

ya 'X-Bar' ambapo zaidi ya kirai kimoja kilichovurumishwa cha kategoria leksika inatambulika. Hii inamaanisha kuwa matokeo ya kielelezo tungo hapo juu yatakuwa hivi:



Utagundua kwamba 'msichana mrefu sana na 'msichana' zinaelezwa kama  $\bar{N}$  kwa sababu zote zinaweza kuwakilishwa na yule. (Ni viwakilishi vya kuashiria, na hivyo basi ni viambajengo huru.)

Kiunzi cha SMV hakikujitosheleza kwa sababu ya kuepuka kudadisi muundo wa kategoria virai. Dhana ya 'neni kuu la kirai' haikushughulikiwa ipasavyo na kiunzi cha muundo virai. Hii ni dhana muhimu kwa sababu neno kuu la kirai lina uhusiano na kifundo kikuu. Kwa mfano, watoto hawa wazuri. Kwa vile watoto ni wingi, kirai chote kitakuwa kwa wingi. Kwa vile N ni wingi,  $\bar{N}$  pia ni wingi. Mfumo wa SMV hauonyeshi uhusiano huo. Riemsdijk na

Williams ( 1986: 40) wanasema:

Njia inayotumiwa kuelezea  
'kichwa cha kirai' sharti ihakikishe  
mwanzoni kwamba kifundo cha  
wingi na kifundo cha mwisho  
vinashahibiana kisifa.<sup>16</sup>

(Tafsiri ni yetu)

Katika nadharia ya 'X-Bar', neno kuu katika kirai linaashiriwa kama  $X^0$  au  $X$ ,  
kategoria kirai inayobeba  $X^0$  au  $X$  inaashiriwa kuwa  $\bar{X}$  au  $X^1$ , ile kategoria  
kirai inayobeba  $\bar{X}$  au  $X^1$  inaashiriwa na  $\bar{\bar{X}}$  au  $X^2$  nayo kategoria kirai  
inayobeba  $\bar{\bar{X}}$  au  $X^2$  inaashiriwa na  $\bar{\bar{\bar{X}}}$  au  $X^3$  na kadhalika. Hivyo basi  $\bar{X}, \bar{\bar{X}}, \bar{\bar{\bar{X}}}$  na  
kadhalika zinachukuliwa kama zile 'bar zilizovurumishwa' za  $X$ . Hivi ni  
kusema kwamba KN katika sintaksia ya  $\bar{X}$  nayo hubeba kategoria ya kirai kati  
ya  $\bar{X}$  au 'N-Bar" ambayo ni kategoria isiyopatikana katika muundo virai.  
Hivyo  $\bar{X}$  inabeba N. Hii inabadilisha muundo kirai kulingana na Radford  
(1981:103)



Sheria hizi zinafupishwa hivi:

$$x^n \text{ ————— } \dots\dots\dots x^{n-1} \dots\dots\dots$$

Hili lilimaanisha kuwa kirai chochote cha kategoria X kilicho na idadi n ya 'bar' ni sharti kibebe katika neno kuu kiambajengo cha kategoria X kilicho na 'n-1' bars.

Nadharia ya 'standard panuzi iliyodurusuwa' ambayo hujulikana kama nadharia ya umilikifu na masharti, ambamo nadharia ya 'X-Bar' inapatikana vilevile ina nadharia nyingine. Nadharia hizi pamoja na 'X-Bar' ndizo huijenga nadharia ya UM.

### **1.7.1 UTANGULIZI WA NADHARIA YA UMILIKIFU NA MASHARTI**

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni, kazi ya kuelezea na kupambanua kazi yetu ilijikita katika nadharia ya umilikifu na masharti.<sup>17</sup> Nadharia ya UM imekuzwa na Chomsky na wengine kutokana na jaribio la kuunda nadharia ya sarufi bia.

Nadharia ya SB ni nadharia ya kidhahania yenye hali jumulifu katika miundo ya kiisimu ambayo inaweza kuonekana katika hali mbalimbali. Wajibu wa isimu katika kukuza nadharia kama hiyo ni ule wa kufanya uainishaji wa kidhahania wenye hali jumulifu katika miundo ya kiisimu ambayo inaweza

kuonekana katika hali mbalimbali.

Nadharia ya SB ni sharti itimize hali mbili zifuatazo:

- (i) Ni sharti ipatane na aina nyingine ya sarufi zilizopo.
- (ii) Ni sharti ijibane na kuiwekea mipaka upeo.  
unaokubalika ili kueleza sababu kwamba kila aina hizo za sarufi zinakuwa katika akili laza.

Mawazo ya Chomsky katika nadharia yake kuhusu kitengo cha sintaksia ni kwamba yanazalisha miundo ya kidhahania ambayo inawakilishwa kifonetiki na kimantiki.

Katika msingi huu, nadharia ya SB inahitajika kupambanua sifa za uwakilishaji tatu, miundo ya nje (MN), umbo kifonetiki (UF) na umbo kimantiki (UMT). Pia ni lazima ipambanue:

- i) Sifa za kitengo sintaksia zinazobadilisha MN ,
- ii) Sifa za kitengo cha UF zinazobadilisha MN hadi UF na
- iii) Sifa za kitengo cha UMT zinazobadilisha MN hadi UMT au ufasiri kisemantiki.

Katika nadharia ya Chomsky, kanuni za UF hasa ni za kimitindo kuzidi kisarufi. MN wa kidhahania unatokana na umbo ndani (UD) kwa kuzingatia kanuni ugeuzajimaumbo unaojulikana kama 'uhamishaji  $\alpha$ '. UD unazalishwa

na msingi ambao unahusisha kitengo cha kategoria na leksikoni.

Kanuni za UM zinahusiana na UD ili kupata uwakilishaji ambapo maswala kama vile upeo wa uvumishaji na ufasiri wa urejeshi unaweza ukafikiwa.

Hivyo, UMT ni kiwango kimoja cha uwakilishaji kisintaksia.

Wazo la kimsingi katika nadharia ya UM ni kwamba upambanuzi wa sifa na mifumo ya uwakilishaji kisintaksia katika lugha inaweza kufanikishwa kwa kutumia nadharia ya Masharti katika uwakilishaji. Nadharia ya UM ndiyo nadharia inayohusu kundi la nadharia zilizoko chini yake ambayo kila mojawazo inashughulikia sehemu fulani muhimu ya sarufi. Katika nadharia hii, sarufi ya lugha inaelezwa kwa kuhusisha nadharia hizi zote. Kila mojawapo ya nadharia hizi za chini zina sifa zake, ambazo tutazijadili kwa muhtasari:

- i) Nadharia ya 'X-Bar'.
- ii) Nadharia ya  $\theta$  (theta).
- iii) Nadharia ya uhusika.
- iv) Nadharia ya Masharti.
- v) Nadharia ya Umilikifu.
- vi) Nadharia ya Umipaka.
- vii) Nadharia ya Ufafanuzi wa kiima cha kishazi kisoukomo



## 1.7.2 NADHARIA YA $\theta$ (THETA)

Nadharia ya  $\theta$  inahusika na uhusiano kati ya ‘majukumu ya’ au ‘agiumenti ya’ na kiarifu-kitenzi. Kazi muhimu ya  $\theta$  ni kuonyesha hali ambapo KN kinaweza kuwa 'agiumenti' ya kitenzi.

Wazo kuu katika  $\theta$  ni kwamba KN katika sentensi kitakuwa kiima cha kiarifu au shamirisho. Hata ikiwa KN kitachukua nafasi gani katika sentensi, sharti kiwe na ‘jukumu’. Muundo wa ‘agiumenti’ unakaa vipi? dhana ya ‘agiumenti’ ina nguvu nyingi; tukiangalia muundo wake ambapo tunaona yale ambayo ni ‘agiumenti’ na yale yasiyo ‘agiumenti’. Kwa mfano kuna ukubaliano kwamba (1) kitenzi 'penda' kina 'agiumenti' mbili, KN Yohana na Maria.

1. Yohana anampenda Maria. Mwanamantiki anaweza kuashiria sentensi hiyo kama;
- 2 Anampenda (Yohana, Maria) Nadharia ya  $\theta$  inatoa sheria kwamba kila agiumenti inabeba jukumu moja tu la  $\theta$  na kila jukumu la  $\theta$  linahusishwa na 'agiumenti' moja tu.

Sheria hii ya  $\theta$  linaeleza kutowezekana:

- (i) Kuwekwa jukumu zaidi ya moja ya  $\theta$  kwa ‘agiumenti’ na
- (ii) Kuwekwa jukumu la  $\theta$  moja kwa zaidi ya 'agiumenti' moja.

### 1.7.3 NADHARIA YA UHUSIKA

Katika nadharia hii, inachukuliwa kuwa kidhahania, 'uhusika' ni sifa ya lazima katika KN cha sentensi. Sharti hili linaelezwa na kauli ya nadharia ya uhusika inayojulikana kama kauli ya kichujo.

Hivi ni kusema kwamba, sentensi yoyote ambayo inabeba KN ikiwa na kipengele cha leksia lakini hakina 'uhusika' sio sawa kisarufi.

### 1.7.4 NADHARIA YA MASHARTI

Kwa mujibu wa nadharia hii, KN cha 'agiumenti' kilicho na wajibu wa  $\theta$  kinaonekana katika kategoria tatu :

- i) Mirejeosabiki
- ii) Uwakilishi
- iii) Urejelezi

Mirejeosabiki inafafanuliwa kama KN ambayo urejeaji wao ni katika sentensi yenye kibainishi katika umbo wa ndani na ambayo haiwezi ikawa na urejeaji huru.

Katika nadharia ya Masharti, mirejeosabiki ni za aina mbili;

Mirejeosabiki wakilishi- hii ikiwa ni mirejeosabiki ambayo visabiki vyake

vina jukumu huru la  $\theta$ .

Mirejeosabiki isowakilishi-ni mirejeosabiki ambayo visabiki vyake havina jukumu huru la  $\theta$ . Viwakilishi ni KN ambacho hakina kipengele maalum cha leksika na vina sifa, idadi, uana na 'uhusika'.

Kanuni za masharti katika nadharia hii zinatoa masharti ambapo KN kinafasiriwa kama kirejeoenza na KN kingine katika sentensi hiyo kama ifuatavyo:

- i) Mirejeosabiki sharti iambatanishwe na kategoria inayoimiliki .
- ii) Kiwakilishi sharti kiwe huru katika kategoria yake ya umilikifu .
- iii) Urejelezi sharti uwe huru kila mahali .

### **1.7.5 NADHARIA YA UMILIKIFU**

Dhana ya 'umilikifu' ni kiini katika nadharia ya SB. Inaeleza uhusiano ulioko kati ya neno kuu na shamirisho yake. Muundo wa uhusiano wa 'umilikifu' unafafanuliwa kama ifuatavyo.

X inamiliki Y pale ambayo Y inapatikana kufasiri ukamilifu wa  $X(X^{\max})$ , na  $X^{\max}$  ndiyo ufasiri uliokamilika inayobeba Y na X.

Hivyo X inayomiliki inazuiliwa kumiliki chochote kisicho nje ya ufasiri

kamilifu. Vizuizi vyote vinakuwa ufasiri kamilifu ambavyo ni S,KN,KIV, K,KIH na T.

Bynon (1977: 149) anatoa maelezo kuhusu ishara ambazo zinatumiwa katika nadharia hii. [ $\alpha$  idadi ], [ $\beta$  jinsiya], na [ $\gamma$  uhusika] ambapo  $\alpha$  inasimamia kima cha umoja au wingi,  $\beta$  ikisimamia jinsi ya kiume, kike na jinsi kati. Nayo  $\gamma$  inaashiria uhusika kiima ambao ni umbo la uhusika ambalo huwekwa kwenye nomino au kiwakilishi kuonyesha kuwa nomino au kiwakilishi hicho ni kiima cha sentensi. Vilevile,  $\gamma$  ikiashiria uhusika yambwa ambao ni uhusika unaonyesha kuwa nomino katika tungo inayohusika ndiyo inayotendwa au inayotendewa.

Kutokana na maelezo ya Bynon (Ibid) tuliweza kuelewa maelezo anayotoa Cowper (1992) kuhusu nadharia ya umilikifu, kwamba:

$\alpha$  inamiliki  $\beta$  ikiwa

a  $\alpha$  ni  $X^0$ , ya baadhi ya X .

b.  $\alpha$  na  $\beta$  zimo katika kishazi kimoja.

c. Ufasiri wote uliokamilika  $\gamma$ , ikiwa  $\gamma$  inamiliki  $\beta$  basi  $\gamma$  inamiliki  $\alpha$ .

Hiyo sehemu ya (c) inamaanisha kwamba leksika KN( $\beta$ ) haiwezi kamwe kutenganishwa na kimiliki ( $\alpha$ ) kwa namna yoyote ya ufasiri kamilifu.

## 1.7.6 NADHARIA YA UMIPAKA

Nadharia hii inahusu dhana ya ‘uelekezaji’ wa kiambajengo. Dhana ya ‘uelekezaji wa kiambajengo’ inafafanuliwa kama:

Kiambajengo X kinaelekeza  
Kiambajengo Y, iwapo hakuna  
Kinachomiliki kingine na kifundo  
cha kwanza juu ya X katika  
kielelezo tungo kinachovibeba  
nacho kinamiliki (sio lazima imiliki punde) Y.

Haya yote yanawezekana kwa sharti kuwa hakuna chochote kinachoweza kuelekeza viambajengo nje ya uvurumishaji ulio kamilifu unaokibeba.

Reimsdijk (Ibid:275)

## 1.7.7 NADHARIA YA UFAFANUZI WA KIIMA CHA KISHAZI KISOUKOMO

Katika nadharia ya ‘standard’ ya sarufi geuzamaumbo, ilichukuliwa kwamba mambo yanayohusu sintaksia yanayoingiliana na ufasiri wa kisemantiki yalielezwa katika kiwango cha muundo wa ndani. Hili lilimaanisha kwamba ugeuzajimaumbo haukuweza kubadilisha maana; iwapo muundo wa nje ulikuwa na maana tofauti na ile ya muundo wa ndani, na iwapo sheria za ufasiri zinapatikana na kufanya kazi tu katika muundo wa ndani, kutatokea upungufu mkubwa wa baadhi za maana katika sentensi.

Nadharia ya ufafanuzi wa kiima cha kishazi kisoukomo inaelezwa kwa mujibu wa Horrocks (1987:131) kwa kutoa mifano miwili.<sup>18</sup>

i) Ted alimwahidi mkewe kutupilia mbali talaka .

ii) Ted alimsihi mkewe kutupilia mbali talaka.

(Tafsiri ni yetu).

Katika mifano hiyo hapo juu, ni dhahiri kwamba katika mfano (i) Kiima kapa 'Kinatawaliwa' kwa maana ya 'controlled' na kiima cha kishazi kikuu na katika mfano (ii) na yambwa ya kishazi kuu. Sheria zinahitajika kueleza mambo haya.

Ni dhahiri kwamba shamirisho ya 'kuahidi' na 'kusihi' ipo katika nafsi sawa katika viwango vya UMT; kwamba kiima kapa ni sharti kitolewe kama sehemu ya ufasiri, kwa sababu kiima kapa katika kila mfano hapo juu ni agiumentu inayopewa wajibu wa  $\theta$ . Uvurumishaji katika nadharia hii unahitaji kwamba muundo wa shamirisho katika kiwango kimoja cha uwakilishaji sharti utokeze katika viwango vingine. Hivyo basi 'Kuahidi' na 'kusihi' vitakuwa na vishazi vyenye shamirisho katika MN na UD na pia katika UMT.

## **1.8 NJIA ZA UTAFITI**

Sehemu kubwa ya kazi hii ilikuwa kubukua yaliyoandikwa kuhusu kazi yetu, katika maktaba. Tulisoma kazi mbalimbali ambazo zimeandikwa juu ya

nadharia tuliyoitumia ili kutuwezesha kuifahamu nadharia yetu kikamilifu.

Tulisoma pia kazi zilizoandikwa juu ya nomino kwa ujumla ili tuweze kujua waziwazi nomino ni nini na jukumu lake katika sentensi.

Aidha tulisoma kazi mbalimbali ambazo zimeandikwa juu ya kikundi nomino cha Kiswahili kwa ujumla, na zile zilizoandikwa juu ya nomino ya Kiswahili na muundo wake. Kazi hizi zilitupa ujuzi wa kijumla juu ya uwanja tuliotaka kuushughulikia. Fauka ya hayo, yalituwezesha kuchuja mawazo yote ambayo yalikuwa na uwezo wa kutusaidia katika utafiti wetu. Isitoshe, yalituwezesha kuona yale ambayo yamekwisha kufanywa, na pia lile pengo lililoachwa ambalo tulijaribu kuliziba.

Pia, tulipata fursa ya kuwahoji wataalamu au magunge wa isimu ya Kiswahili na Kiingereza. Tulizungumza, tukajadiliana na kuomba ushauri kutoka kwao , ili tuweze kupata mwongozo bora kutuwezesha kuyafikia malengo yetu.

Tulitumia vilevile tajriba yetu ya lugha ya Kiswahili kutoa mifano na kufasiri data zetu.

# TANBIHI

1. Hartmann, R na F. Stork (1973) Dictionary of language and Linguistics. Applied Science Publishers Ltd, London. uk 155.
2. Kamusi sanifu ya Isimu na Lugha (1990) Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam uk 42.
3. Rosenbaum, P na J Roderick (1968). English Transformational Grammar. Ginn and Company Ltd. London uk 45.
4. Culicover, P (1976) Syntax Academic Press, New York uk 13.
5. Pei, M (1966) Glossary of Linguistic Terminology. Columbia University Press, New York. uk 182
6. Radford, A (1981) Transformational Syntax. Cambridge University Press, Cambridge.UK.93
7. Tumetafsiri 'bar-projection' kama 'uvurumishaji wa bar'. Baadhi ya istilahi hizi hazikupatikana katika kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990) inayochapishwa na TUKI, Dar-es-salaam.
8. Kibainishi kimetumika hapa kuashiria dhana ya 'specifier'.
9. Noam Chomsky siye mwasisi wa nadharia ya sintaksia ya 'X-Bar'. Mfumo wa 'X-Bar' ilijaribiwa miaka ya nyuma na mwanaisimu Zellig Harris katika miaka ya hamsini.
10. Stockwell, R (1973) The Major Syntactic Structures of English. Holt, Rinehart and Winston, Inc. New York uk 21.
11. Idadi kamili ya lahaja za Kiswahili haijafikiwa. Sisi tuna maoni kama yale ya Baya (1993) kwamba Kiswahili kina lahaja zaidi ya kumi na nane.
12. Kwa mujibu wa Koutsoudas(1966), sentensi sahili ni sentensi kinachobeba kiarifu kimoja. Naye Bach (1964) anadai kwamba, sentensi sahili ni sentensi ambayo ina kishazi kimoja. Hatukujiingiza kujadili sentensi sahili. Hata hivyo maoni yao yalitiliwa maanani katika kuiangalia sentensi sahili ya Kiswahili.
13. Msanjila, Y (1985) "Tofauti za msingi kati ya Tungo nomino na Tungo vitenzi katika Kiswahili" katika Mdee, J na E.Mbogo (Whr) Mulika na 17.



14. Kopula ni kijineno cha kitenzi KUWA kinachotumiwa kuunganisha kiarifu na kiima katika tungo nomino.
15. Mgullu,R (1990)The Structure of Kiswahili Sentences: A Transformational Generative Approach. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi uk.21
16. Riemsdijk,H na E. Williams (1986) Introduction to the Theory of Grammar. The Massachusetts Institute of Technology (MIT) Press, Massachusetts. uk 40.
17. Tuliweza kutafsiri nadharia ambazo zipo katika 'Government and Binding'. Nadharia ya 'Government' imetafsiriwa kama 'umilikifu'; 'Binding' imetafsiriwa kama 'masharti'; 'theta' au  $\theta$  imetafsiriwa na kuendelezwa vivyo hivyo 'Theta' au  $\theta$ . Nadharia nyingine kama vile 'case' imetafsiriwa kama 'uhusika' nayo tulifasiri nadharia ya 'bounding' kama 'umipaka' na 'control' tulitoa maelezo tu. Tumeasisi nadharia hii kwa lugha ya Kiswahili na hivyo, tuliweza kukumbana na matatizo katika kutafsiri na kufasiri baadhi ya istilahi hizi.
18. Horrocks,G (1987) Generative Grammar. Longman,London uk 131.

## 2.0

## SURA YA PILI

### 2.0.0

### MOFOLOJIA YA NOMINO

Sura hii inachunguza mofolojia ya nomino ya Kiswahili. Katika kufanya hivi, mosi kabisa, ngeli za majina au nomino zilihakikiwa. Katika kuangalia ngeli hizi, misingi mbali ya kuainisha ngeli ilitumika kama vile uainishaji kisemantiki, kisintaksia na kimofolojia. Tulifanya hivi kwa sababu ya kufafanua na kuangaza zaidi maelezo yetu na takriban kueleza kwa tafsili baadhi ya mifano tuliyotoa. Mpangilio tuliotumia katika sura hii ni pamoja na ule wa hisabati na wa viambishiawali. Ni vigumu wakati mwingine kuepuka kutumia mitindo yote miwili hasa pale panapohitajika maelezo zaidi.

Mofolojia ya nomino ni sehemu muhimu sana katika kazi yetu. Katika kuangalia KN cha Kiswahili, dhana ya uambishaji na pia unyambuaji ziliangaliwa kwa sababu maneno katika Kiswahili yanawekwa chini ya misingi ya dhana hizi mbili katika kipengele cha mofolojia. Tulitoa mifano na kuchambua ngeli zote za Kiswahili, huku tukizingatia kiambishiawali ambacho husababisha ule upatanifu wa maneno mengine katika sentensi au kishazi. Hivyo basi kabla ya kuangalia KN, tuliona ni jambo muhimu kuweka msingi imara unaohusu upatanifu. Katika sintaksia ya 'X-Bar' jambo lililo muhimu sana ni neno kuu. Kwamba iwapo neno kuu, kwa mfano, lipo katika wingi, basi upatanisho unaojitokeza katika maneno mengine kwenye sentensi hiyo au kishazi hicho, ni viambishiawali vya kurejelea

wingi wala si umoja. Vilevile, tuliangalia unyambuaji na viishio vinavyohusika. Tuliona namna ambavyo maneno yanavyoundwa kutoka neno la awali au kutoka kwa mzizi kwa matlaba ya kuongeza kiambishiawali au kiambishi tamati.

## 2.1 NGELI ZA NOMINO

Nomino katika lugha ya Kiswahili zinaainishwa katika makundi mbalimbali kwa kuzingatia viambishi<sup>1</sup>. Hata hivyo, maelezo haya hayajitoshelezi kwa sababu haipo lazima kwamba viambishi vizingatiwe. Hatukujiingiza kufafanua haya kwa sababu maelezo ya jinsi hiyo yangekiuka upeo wetu wa sasa. Mfumo huu wa upangaji nomino haupatikani tu katika lugha ya Kiswahili bali hata katika lugha nyingine za kibantu.

Mpangilio wa nomino katika ngeli ni muhimu kwa kuwa viambishi vyote hutegemea nomino. Viambishi vya nomino katika umoja ni tofauti na vya wingi wa nomino zizo hizo.

Baadhi ya nomino hazina viambishi katika umoja lakini wingi wa nomino hizi zaonyesha viambishi kama katika mfano (1)

(1)	Ngeli 5/6	<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>
		Tunda	Matunda
		Embe	Maembe

Hakuna kiambishi katika maneno ya (1) Lakini kiambishi /ma/ ni kiambishi cha ngeli ya 6. Pia kuna nomino nyingine ambazo hazionyeshi viambishi katika hali ya umoja na wingi. Kwa mfano katika mfano(2)

(2)	Ngeli 9/10	<b>Umoja</b>	<b>Wingi</b>
		Chai	Chai
		Filimbi	Filimbi
		Kalamu	Kalamu
		Meza	Meza

Kwa mujibu wa Meinhof (1910), makundi ya nomino kimofolojia katika Kiswahili ni kama ifuatavyo kwenye jedwali (i)

### Jedwali (i)

Nambari	Kiambishiawali	Mifano
1.	Mu	Mtu
2.	Wa	Watu
3.	Mu	Mti
4.	Mi	Miti
5.	Ji-Ø	Jicho
6.	Ma	Macho
7.	Ki	Kitanda
8.	Vi	Vitanda
9.	N	Nyumba
10.	N	Nyumba
11.	U	Ufa
10a.	N	Nyufa
11a	U	Ugonjwa
6a	Ma	Magonjwa
15	Ku	Kuimba
16.	Pa	Pahali
18.	Ku	Kwetu

Meinhof (Ibid) hata hivyo anaonekana hakumakinika ipasavyo na

mpangilio wa ngeli katika Kiswahili. Sisi tulijiuliza alikotupilia ngeli 14 na kiambishiawali MU, kwa sababu ngeli hizi zipo.

Kama tulivyosema awali, tunatumia pia mpangilio wa nomino za Kiswahili unaotumia hisabati 1,2,3,4 hadi 18, ambapo nomino ya hali ya umoja na ya hali ya wingi huwa katika ngeli mbili tofauti. Ngeli zile zinazotumia viambishi ni M-WA, M-MI, JI-MA, KI-VI, N,U na MAHALI. Nazo ngeli zinazotumia

hisabati ni 1-18.<sup>2</sup>

Mbali na ule mpangilio wa Meinhof (Ibid), hapa chini kuna ile orodha ya jinsi hisabati na viambishi zinavyopatanishwa katika jedwali (ii).

*Jedwali (ii)*

NAMBARI	VIAMBISHI	MIFANO
1.	M-	Mtoto
2.	Wa-	Watoto
3.	M-	Mto
4.	Mi-	Mito
5.	Ji-	Jina
6.	Ma-	Majina
7.	Ki-	Kiti
8.	Vi-	Viti
9.	N-	Nyumba
10.	N-	Nyumba
11.	U-	Ufa
14.	U-	Ugonjwa
15/17	Ku-	Kucheza
16.	Pa-	Pahali
18.	M(u)	Mahali

Tunapotumia alama ya mkato katika ngeli ya 15/17, ni kuonyesha kuwa ngeli hizo hutumia kiambishi awali hicho cha nomino. Kwa mintarafu hiyo, tunaweza tukawa na 11/14. Hivyo basi ngeli ya 11 na 14 hutumia kiambishi /u/ na ngeli za

15 na 17 zote hutumia kiambishi /KU-/.

Katika kujadili ngeli za Kiswahili, kwanza tulitumia njia zote mbili yaani herufi na hisabati. Baadaye tulitumia hisabati pekee yake. Kabla ya kujadili ngeli hizi, tulitanguliza faslu hii kwa kupiga msasa dhana ya uambishaji. Hatuwezi kuanza kujadili ngeli za Kiswahili kabla ya kuweka msingi kamili kwa kuzingatia dhana ya uambishaji.

## **2.2 UAMBISHAJI**

Uambishaji ni utaratibu wa kuweka viambishi kwenye mzizi wa neno ili kulipa maana mahususi.<sup>3</sup> Ni vigumu kujadili uambishaji katika lugha bila kuangalia kategoria za sintaksia ambazo zinawakilisha.<sup>4</sup> Katika faslu hii, tuliangalia ngeli za majina na namna ambavyo uambishaji unavyotukia.

### **2.2.1 KUNDI LA 1/2**

Ngeli ya 1/2 inarejelea nomino nafsi na pia nomino za wanyama lakini nadra kwa vitu visivyoo na uhai. Nomino nyingi za binadamu ziko katika ngeli hizi kwa mujibu wa viambishi vya nomino, kama tuonavyo katika mfano (3).

**(3) UMOJA**

Mnyama

Mdudu

**WINGI**

Wanyama

Wadudu

Nomino hizo katika mfano (3) ziko katika ngeli ya 1/2 kwa kuwa zina viambishi /M/ na /wa/. Jambo hili linamaanisha kuwa nomino za binadamu, wanyama na Wadud ambazo hazina viambishi /M/ na /wa/ haziko katika ngeli hizi licha ya kuwa viambishi vya maneno mengine kwenye sentensi ni sawa na vya nomino zenye viambishi M-WA. Tazama mifano 4 (a-f) na ulinganishe na mifano 5 (a-f)

- Mifano            4 a.    Mtu huyu mfupi anakimbia.  
                              b.    Watu hawa wafupi wanakimbia.  
                              c.    Mnyama huyu mfupi anakimbia.  
                              d.    Wanyama hawa wafupi wanakimbia.  
                              e.    Mdudu huyu mfupi anakimbia.  
                              f.    Wadudu hawa wafupi wanakimbia.

- Mifano            5 a.    Kilema huyu mfupi anakimbia.  
                              b.    Vilema hawa wafupi wanakimbia.  
                              c.    Mende hawa wafupi wanakimbia.  
                              d.    Twiga huyu mfupi anakimbia.  
                              e.    Twiga hawa wafupi wanakimbia.

Nomino za sentensi 4(a-f) zinapatikana katika kundi la 1/2 kwa kuwa zina viambishi /M-/ katika umoja na /Wa-/ katika wingi. Nomino za sentensi 5(a-e) ziko katika kundi tofauti hata ingawa viambishi vingine vyote katika sentensi ni sawa na vile vya sentensi 4(a-f).



Baadhi ya nomino za ngeli hizi ni zile zilizoundwa kutokana na vitenzi. Nomino nyingi huundwa kutokana na vitenzi kwa kuongeza viambishi /m na /wa/ kabla ya kitenzi kama katika mfano (6)

<b>(6)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO</b>
	Ganga	Mganga/Waganga
	Lima	Mkulima/Wakulima

Katika mfano (7) kiambishi cha nomino za hali ya umoja katika ngeli hizi huwa /m/ au mw/ na la wingi ni /wa/

<b>(7)</b>	<b>NGELI 1</b>	<b>NGELI 2</b>
	Mkiritimba	Wakiritimba
	Mkoo	Wakoo
	Mkimwa	Wakimwa
	Mwalishi	Walishi
	Mwandazi	Wandazi
	Mwanga	Wanga

### **2.2.2 KUNDI LA 3/4**

Kiambishi /m/ cha ngeli ya 3 ni cha umoja na /mi/ cha ngeli ya 4 ni cha wingi wa nomino za ngeli hizi. Aghalabu, makundi ya 3/4 ni ya mimea ingawa baadhi ya

vitu visivyo na uhai hupatikana humu kama vile mfano (8)

- (8) (i) Mlima  
(ii) Moshi

Takriban, sehemu za mwili na wingi wake kama katika mfano (9) hupatikana katika ngeli hii.

- (9) (i) Mkono  
(ii) Mdomo  
(iii) Mguu

Baadhi ya nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi ili kuonyesha matokeo ya vitenzi huwa katika ngeli hizi, katika mfano (10)

(10)	<b>KITENZI</b>	<b>NGELI 3</b>	<b>NGELI 4</b>
	Shona	Mshono	Mishono
	Unda	Muundo	Miundo
	Dunda	Mdundo	Midundo
	Enda	Mwendo	Miendo
	Cheza	Mchezo	Michezo

Ule muundo wa kiambishi cha hali ya umoja hutegemea sauti ya kwanza katika mzizi wa nomino kama tulivyosema kuhusu ngeli za 1/2. Katika Kiswahili, ikiwa

mzizi wa nomino utanza kwa konsonanti, kiambishi cha hali ya umoja kitakuwa /m/. Muundo wa kiambishi cha wingi haubadiliki kama inavyoonyeshwa katika mfano (11)

(11)	NGELI 3	NGELI 4
	M-figili	Mi-figili
	M-goza	Mi-goza
	M-gunda	Mi-gunda
	M-lima	Mi-lima

Mzizi ukianza kwa vokali, kiambishi cha hali ya umoja hubadili muundo na kuwa /mw/. Sio nia yetu kujadili mabadiliko ya kifonolojia katika kazi hii. Tuone mfano (12).

(12)	NGELI 3	NGELI 4
	mw-aridi	mi-aridi
	mw-imo	mi-imo
	mw-ezi	mi-ezi
	mw-iba	mi-iba
	mw-avi	mi-avi

Baadhi ya nomino za ngeli ya 3/4 huanzia kwa /mu/katika hali ya umoja kama inavyoonekana katika mfano (13)

<b>(13)</b>	<b>NGELI 3</b>	<b>NGELI 4</b>
	Mu-unda	Mi-unda
	Mu-wele	Mi-wele
	Mu-wa	Mi-wa
	Mu-hogo	Mi-hogo.

Hata hivyo, majina yote yenye mianzo /m/ katika umoja na /mi/ katika wingi lakini upatanisho wake wa kisarufi ni wa ngeli ya 1/2, hayawekwi katika ngeli hii<sup>5</sup>. Kama tunavyoona katika mfano (14)

<b>(14)</b>	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
	Mtume	Mitume
	Mungu	Miungu

### **2.2.3 KUNDI LA 5/6**

Ngeli ya 5/6 ni mseto wa vitu ainati. Nyingi kati ya nomino ambazo hupatikana katika ngeli hizi ni za sehemu za mwili kama vile katika mfano (15)

	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
<b>(15)</b>	Jino	Meno
	Sikio	Masikio
	Jicho	Macho

Sehemu za miti kama vile katika mfano (16) pia zinapatikana katika ngeli hii

	<b>UMOJA</b>	<b>WINGI</b>
(16)	Tunda	Matunda
	Tawi	Matawi
	Jani	Majani

Ngeli hii ina majina yenye viambishi /ji/ katika umoja na /ma/ katika wingi. Kiambishi /ji/ cha umoja hupatikana kwenye nomino chache tu. Hivyo, nomino nyingi za ngeli hizi hutambulika kwa kiambishi cha wingi /ma/. Ifuatayo ni mifano ya nomino za ngeli hizi ambazo zina kiambishi /ji/ cha umoja. Katika kazi hii, sio nia yetu kuingia kilindini kuangalia miundo ya ndani ya majina katika ngeli hizi kwa vile hatukudhamiria kujadili mabadiliko ya kifonolojia. Mifano (17) hapa chini ni nomino za ngeli zilizo na kiambishi /ji/.

(17)	<b>NGELI 5</b>	<b>NGELI 6</b>
	Ji-we	Ma-we
	Ji-cho	Ma-cho
	Ji-ko	Me-ko
	Ji-no	Me-no

Kuna nomino katika lugha ya Kiswahili ambazo zina mizani mbili nazo huanza kwa kiambishi /ji/ katika hali ya umoja na huhifadhi hicho kiambishi katika hali ya wingi pia kama tunavyoona katika mfano (18)

(18)	NGELI 5	NGELI 6
	Ji-rafu	Ma-jirafu
	Ji-simu	Ma-jisimu
	Ji-pu	Ma-jipu
	Ji-mbo	Ma-jimbo

Vilevile, baadhi ya nomino katika ngeli ya 5/6 huwa hazina viambishi vya umoja.

Mifano (19) inathibitisha dai hili

(19)	KIAMBISHI	NGELI 5	NGELI 6
	∅	duka	ma-duka
	∅	soko	Masoko
	∅	gari	ma-gari
	∅	bonde	ma-bonde

Majina mengine yasiyo na viambishi katika umoja, na /ma/ katika wingi, lakini yenye upatanisho wa kisarufi kama katika 1/2 hayawekwi katika ngeli hii, kama tunavyoona katika mfano (20)

**(20) KIAMBISHI****UMOJA****WINGI**

Ø

bwana

ma-bwana

Ø

hakimu

ma-hakimu

Ø

jambazi

ma-jambazi

Ø

bingwa

ma-bingwa

Ø

bubu

ma-bubu

Katika ngeli ya 6 kuna nomino ambazo hupatikana katika hali ya wingi kama tuonavyo katika mfano (21) hapa chini.

**(21) NGELI 6**

Maziwa

Maana

Maisha

Mauti

Maudhiko

Mafuta

Mate

Manukato

Maji

Nomino hizo hapo juu hazina umoja wake.

Kapinga (1983:46) anasema kuwa majina ya ngeli hii kwa kawaida ni majina ya vitu visivyokuwa na uhai, vyombo vya matumizi ya kila siku, majina ya mambo au hali zinazotokana na matukio ya maisha, mazoea, desturi na namna au jinsi<sup>6</sup> Maelezo ya Kapinga (Ibid) ni ya kisemantiki, ambayo awali tulisema kila mara tulirejelea pale ambapo tulitaka maelezo yetu yaweze kueleweka vyema. Mbaabu (1990:89)<sup>7</sup> vilevile ana maoni kama haya.

Baadhi ya vitu visivyo na uhai katika ngeli hii ni kama hivi vifuatavyo katika mfano (22)

(22)	NGELI 7	NGELI 8
	Ki-sugu	Vi-sugu
	Ki-nga	Vi-nga
	Ki-ng'ora	Vi-ng'ora
	Ki-peto	Vi-peto
	Ki-pini	Vi-pini

Baadhi ya nomino za ngeli hizi huanzia kwa [tʃ] katika umoja na /vy/ katika wingi kutegemea sauti ya kwanza ya mzizi wa nomino kama inavyoonekana katika mfano (23) hapa chini. Muundo wa ndani ni /ki/ ambapo [tʃ] imetokea kwa sababu za ukaakaishwaji.



(23)	NGELI 7	NGELI 8
	tʃ-andalua	vy-andalua
	tʃ-ano	vy-ano
	tʃ-emni	vy-emni
	tʃ-enezo	vy-enezo
	tʃ-ondo	vy-ondo

Kunayo mifano mingi ya nomino za vitu visivyo na uhai ambavyo hata ingawa huanza kwa [tʃ] katika umoja haziko katika ngeli hizi. Hii ni kwa sababu hakuna /ki/ katika muundo wa ndani kama, katika mfano (24)

(24)	Chembe
	Chimba
	Changarawe
	Chokaa
	Chimbo

Viwakilishi vya nomino hizi pamoja na viambishi vingine katika sentensi ni sawa na vya ngeli ya 1/2 kama katika mfano (25) hapa chini.

(25)	Kisu kile ki-kali ki-memkata
	Visu vile vi-kali vi-memkata
	Kiwete yule mrefu amenunua nyumba
	Wiwete wale warefu wamenunua nyumba

Nomino nyingi za ngeli hii hazina tofauti ya umbo kati ya umoja na wingi. Ingawa majina katika kundi la 9/10 hujulikana kama ngeli N, nyingi kati ya nomino hizi hazina kiambishi /n/. Nyingi kati ya nomino za ngeli hizi ni za vitu vya kawaida kama vile katika mfano (26) hapa chini.

(26) Nyumba

Nazi

Njia

Kuna nomino za wanyama kama vile katika mfano (27) hapa chini.

(27) Ngamia

Ng'ombe

Mbuzi

Mifano (27) inawekwa katika ngeli hizi kwa sababu umoja na wingi wake huwa sawa. Pia nomino nyingi zilizokopwa huwa katika ngeli hii. 'Ngeli hii ndiyo ichukuayo majina mengi yatokanayo na lugha za kigeni .....'.<sup>8</sup> Baadhi ya majina haya ya kigeni yanapatikana katika mfano (28)

(28)	UMOJA	WINGI
	Meza	Meza
	Bima	Bima

Baiskeli	Baiskeli
Ada	Ada
Chapa	Chapa
Fedha	Fedha

Nomino za ngeli hizi ambazo huwa na kiambishi /n/ ni kama hizi katika mfano(29)

<b>(29)</b>	<b>NGELI 9</b>	<b>NGELI 10</b>
	Nari	Nari
	Nandu	Nandu
	Nyumba	Nyumba
	Nzumari	Nzumari
	Nyika	Nyika
	Nusukaputi	Nusukaputi

Mifano ya nomino katika ngeli ya 9/10 huwa haina kiambishi /n/ kama mifano ifuatayo katika mfano (30)

<b>(30)</b>	<b>NGELI 9</b>	<b>NGELI 10</b>
	Dago	Dago
	Faharasa	Faharasa
	Meza	Meza
	Krini	Krini
	Mofa	Mofa

Kundi la 11 huwa hasa ni la vitu vilivyo na umbo refu na jembamba. Nomino ambazo zina kiambishi /u/ hugawanywa katika ngeli mbili-ngeli ya 11 na 10. Nomino za ngeli ya 11 ni zile ambazo huchukua viambishi vya ngeli 10 (wingi wa ngeli N) kama wingi wake. Nomino zote za ngeli hii ya 11 ni za vitu vinavyoweza kuguswa kama tuonavyo katika mfano (31) hapa chini.

(31)	NGELI 11	NGELI 10
	Ubati	Mbati
	Ubeleko	Mbeleko
	Ubavu	Mbavu
	Uzi	Nyuzi
	Upo	Nyupo
	Ubugu	Mbugu
	uta	Nyuta

Baadhi ya nomino za ngeli hii 11 huanzia kwa /w/ na hazina tofauti kati ya umoja na wingi kama tunavyoona katika mfano (32) hapa chini.

(32)	NGELI 11	(UMOJA)	WINGI(12)
		Wino huu	Wino huu
		Wali huu	Wali huu

Sehemu ya pili ya nomino hizi zinazoanzia kwa kiambishi /u/ni nomino za ngeli

ya 11a (angalia mpangilio wa Meinhof) na ni za vitu tunavyohisi au vitu visivyoweza kuguswa kama tunavyoona katika mfano (33a na b)

<b>(33)</b>	<b>(a)</b>	<b>NGELI 11a</b>	<b>(b)</b>	<b>NGELI 11a</b>
		Urembo		Ukulima
		Ukarimu		Uvuvi
		Ukiritimba		Utafiti
		Ubora		Uhunzi
		Uzee		Uhariri

Zile nomino katika mfano 33(a) hutokana na vivumishi na ya orodha b hutokana na vitenzi. Mengi kuhusu vivumishi angalia sehemu 3.2

Nomino katika kundi 11a kimuundo hazionyeshi hali ya umoja au wingi. Ikiwa zitatumiwa kama nomino za hali ya wingi, nomino za ngeli 11a huchukua viambishi vya ngeli 6a kama wingi wake kama inavyoonekana katika mfano (34)

<b>(34)</b>	<b>NGELI 11a (UMOJA)</b>	<b>NGELI 6a (WINGI)</b>
	Ugonjwa huu	Magonjwa haya
	Upana huu	Mapana haya
	Ugomvi huu	Magomvi haya
	Ulezi huu	Malezi haya
	Ulalo huu	Malalo haya

## 2.2.7 KUNDI LA 15

Nomino zote za ngeli hii huundwa kutokana na vitenzi vya Kiswahili. Kiambishi /ku/ huongezwa katika mwanzo wa vitenzi vya Kiswahili ili kuunda nomino za ngeli hii, kama tuonavyo katika mfano (35) hapa chini.

(35)	KITENDO	NGELI 15
	Cheza	Kucheza
	Imba	Kuimba
	Cheka	Kucheka
	Shona	Kushona
	Andika	Kuandika
	Tawanya	Kutawanya
	Soma	Kusoma

Upatanisho wa kisarufi kati ya vitenzi-jina na vivumishi pamoja na vitenzi halisi unaonekana kwa kiambishi /ku/. Nomino za ngeli ya KU-kitenzi hazina kiambishi cha pekee katika wingi. Alama ya maumbo ya vitenzi-jina ni hii moja tu, yaani /ku/. Kapinga (Ibid) anasema kuwa katika ngeli zote, ni ngeli hiyo tu ambayo majina yake huchukua mtindo wa kauli ya kutenda, kutendwa na kutendeka kama katika mfano (36) hapa chini.

(36)

<b>KAULI YA</b>	<b>KUTENDA</b>	<b>KUTENDWA</b>	<b>KUTENDEKA</b>
	Kupika	Kupikwa	Kupikika
	Kucheza	Kuchezwa	Kuchezeka
	Kuona	Kuonwa	Kuonekana
	Kuimba	Kuimbwa	Kuimbika

Majina ya vitenzi yanasimama daima katika hali ya kutodhihirika. Majina haya hayadokezi nafsi wala wakati, yaani hayajulishi nani wala nini linahusika

#### **2.2.8 KUNDI LA 16,17, na 18**

Ngeli za 16, 17, na 18 hurejelea mahali kwa kuwa hiyo ndiyo nomino ya pekee inayopatikana katika ngeli hizi. Nomino hizi zinaweza kugawanywa mara tatu kutegemea viambishi vitatu tofauti vya nomino hii kama katika mfano (37) hapa chini.

- (37) (i) Mahali ha-pa au pa-le (16)  
(ii) Mahali hu-ku au ku-le (17)  
(iii) Mahali hu-mu au m-le(18)

Kiambishi /pa/ katika mfano 37(i) huonyesha mahali kamili panapotajwa. Kiambishi /ku/ katika mfano 37 (ii) huonyesha upande au mahali kwa jumla, bila

ya kupataja pahali penyewe, na kiambishi /mu/, katika 37(iii) huonyesha undani wa mahali. Ifuatayo ni mifano ya viambishi katika sentensi, huu ukiwa mfano (38)

(38) Pale pembeni pana mti.

Kule nje kuna nyasi.

Mle chumbani mna nyoka.

Ngeli ya 16,17, na 18 hukopa majina toka ngeli zingine kwa kuongeza kiambishi kiangama /ni/ mwishoni mwa jina. Hata hivyo majina haya kwa kweli huwa ni virai vihusishi, kama katika mfano (39)

(39)	NGELI	UMOJA	WINGI
	3/4	Mtini	Mtini
	5/6	Jichoni	Machoni
	7/8	Kichwani	Vichwani
	9/10	Nguoni	Nguoni
	11/10a	Ufani	Nyufani

Ingawaje kwa kuongeza kiangama /ni/ mwishoni mwa jina, maana asilia ya jina haibadiliki, lakini mtazamo wa upatanisho wa kisarufi huweka wazi zaidi maana ya neno lenyewe katika uhusiono wake na mahali.



Kihistoria unyambuaji ni uundaji wa neno kutoka neno la awali au kutoka kwa mzizi kwa kuongeza kiambishiawali au kiambishi tamati.<sup>9</sup>

( Tafsiri ni yetu)

Nyingi ya nomino katika lugha ya Kiswahili zinanyambuliwa kutoka vitenzi na chache zinanyambuliwa kutoka vivumishi. Nomino zinazotokana na unyambuaji zinaundwa na kule kuongezwa kwa kiambishi tamati cha nomino kwa mzizi wa kitenzi.<sup>10</sup> Nomino ambazo hutokana na vitenzi huchukua kiambishi awali na kiambishi tamati. Viambishi tamati ni /-ni/, /-a/, /-u/ na /-o/ ambavyo, kila kimoja kina umuhimu wake isipokuwa /-a/ ambayo haina maana bainifu.

Viambishi tamati vinapaswa kuangaliwa pamoja na viambishi awali ili kuelewa ile nomino mpya inayotokana na kitenzi.

Ifuatayo ni mifano ya nomino zilizotokana na unyambuaji kama ilivyo katika mfano (40)

(40)	KITENZI	NOMINO (NGELI 1/2)
	Lima	Mkulima/Wakulima
	Pika	Mpishi/ Wapishi
	Fuata	Mfuasi/Wafuasi

Iba	Mwizi/wezi
Jenga	Mjenzi/ Wajenzi
Lea	Mlezi/ Walezi

Nomino hizo ni tendi na hubeba kiambishi tamati/-i/. Idadi kubwa ya nomino huundwa kwa kutumia kiishio /-i/ . Nomino nyingi zinazoundwa kutokana na vitenzi zikitumia kiishio /-i/ humaanisha mtu au kitu kinachotenda tendo<sup>11</sup>. Tunaangalia kila kiishio katika unyambuaji.

### 2.3.1 KIISHIO -i

Nomino zilizoundwa kwa kutumia kiishio /-i/ zaweza kuwa na kiambishi kitangulizi /-u/, na kuwa katika ngeli ya 11a, kama katika mfano (41)

(41)	KITENZI	NOMINO (NGELI 11a)
	Ongoza	Uongozi
	Angalia	Uangalizi
	Tumika	Utumishi
	Zuka	Uzushi

Mdee (1986:80) anasema kwamba kiishio -i kiambatishwapo katika mzizi wa kitenzi kikiwa ni kiambishi tamati, huweza kuunda majina kwa kushirikiana na viambishi vingine.<sup>12</sup> Vitenzi vyenye kuchukua kiambishi tamati -i pamoja na

viambishi awali /ma-/ au/u-/ hujenga majina kama katika mfano (41).

### 2.3.2 KIISHIO -JI

Kiambishi -ji katika Kiswahili hudokeza dhana ya mazoea ya kutenda au kutendeka kwa jambo.<sup>13</sup> Kikitumika pamoja na kiambishi cha ngeli za 1 na 2 humaanisha mtu anayefanya kitendo hicho kama kazi yake ya mara kwa mara. Mara nyingine, tofauti kati ya nomino zilizo na kiishio -ji kama vile msomaji na muombaji na nomino zenye kiishio -i kama vile msomi na muombi hutegemea matumizi. Katika Kiswahili, kitenzi kinapoanza kwa konsonanti isiyokuwa na mghuno kama vile katika mfano (42)

#### (42) KITENZI

Tazama

Sikia

Chunga

nomino zinazoundwa huishia kwa -ji kama vile katika mfano (43) hapa chini

#### (43) NOMINO

Mtazamaji

Msikilizaji

Mchungaji

Ashton (1947: 285) anasema kiambishi hiki -ji hudokeza ile dhana ya mazoea au kurundia kutenda jambo. Kwamba, kiishio -ji ni kama kile kiambishi tamati cha kitenzi -GA<sup>14</sup> kinachopatikana katika lugha nyingi za kibantu.

Kwa kawaida, kiambishi hiki huambishwa katika majina yaliyonyambuliwa kutokana na vitenzi ambavyo vina viambishi awali m-/ki- vya kutenda ambavyo hukamilisha kuundwa kwa jina ambalo linadokeza mazoea ya mtenda au kitendo.

Hasa hujitokeza katika ngeli ya 1/2 kama tunavyoona katika mfano (44)

- (44)
- M-tazama-ji
  - M-soma-ji
  - M-cheza-ji
  - Mw-imba-ji
  - Mw-omba-ji
  - M-shika-ji
  - M-rusha-ji
  - M-tega-ji

### 2.3.3. KIISHIO -E

Katika Kiswahili, kiishio -e kinapotumika kuunda nomino kutokana na vitenzi, humaanisha mtu au kitu kinachotendewa tendo (Ashton 1947: 289). Nomino ambazo zinaumbwa kwa kutumia kiishio -e ni chache zikilinganishwa na zile

zinazoundwa kwa kutumia kiishio -i . Nomino ambazo zinaundwa hivyo huwa na viambishi tofauti. Mifano ya nomino za mtu aliyetendewa tendo ni kama ifuatavyo katika mfano (45)

<b>(45)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO(NGELI 1/2)</b>
	shinda	Mshinde/Washinde
	Teua	Mteule/Wateule
	Tuma	Mtume/Watume <sup>15</sup>
	Pamba	Mpambe/Wapambe

Vilevile, mifano katika (46) inaonyesha nomino za vitu vilivyotendewa tendo.

<b>(46)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO (7/8)</b>
	Umba	Kiumbe/Viumbe
	Pete	Kipete/ Vipete
	Toboa	Kitobwe/Vitobwe
	Tona	Kitone/Vitone

pia, tuna mifano katika ngeli ya 5/6 kama katika mfano (47)

<b>(47)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO</b>
	Hama	Mahame
	Vunda	Mavunde
	Tanda	Matande

### 2.3.4 KIISHIO -O

Polome (1967) anaeleza kuwa kiishio -o huleta maana mbili.<sup>16</sup> Mosi, kiishio hiki kinaashiria kitu au chombo kinachotumiwa kwa kutenda tendo . Kwa hivyo, nomino nyingi zenye maana hii ya kwanza huchukua viambishi vya ngeli za 7/8 kama katika mfano (48)

(48)	KITENZI	NOMINO (NGELI 7/8)
	Tua	Kituo/Vituo
	Pima	Kipimo/Vipimo
	Funika	Kifuniko/Vifuniko
	Vuka	Kivuko/Vivuko
	Ziba	Kizibo/Vizobo
	Funga	Kifungo/Vifungo

Baadhi ya nomino huwa na kiishio -O katika ngeli nyingine pia, kama tuonavyo katika mfano (49)

(49)	KITENZI	NOMINO	NGELI
	Sikia	Sikio/Masikio	5/6
	Lisha	/Malisho	6
	Tega	Mtego/Mitego	3/4
	Unda	Nyundo/Nyundo	9/10
	Fungua	Ufunguo/Funguo	11/10a
	Fagio	Ufagio/Fagio	11/10a
	Pepea	Upepeo/Pepeo	11/10a

Jambo jingine linalotekelezwa na kiishio -o ni matokeo ya tendo. Nomino nyingi zenye kiisho -O na maana hii huwa katika ngeli za 3/4 kama tunavyoona katika mfano (50) hapa chini

(50)	KITENZI	NOMINO(NGELI 3/4)
	Unda	Muundo/Miundo
	Lia	Mlio/Milio
	Cheza	Mchezo/Michezo
	Inuka	Mwinuko/Miinuko
	Tega	Mtego/Mitego
	Shona	Mshono/Mishono

Hata hivyo, sheria hii wakati mwingine inakiukwa kwa sababu ya kuwepo kwa nomino za matokeo katika ngeli tofauti kama vile 5,6,9,10 na 11 kama tunavyoona katika mfano (51)

(51)	KITENZI	NOMINO	NGELI
	Funza	Funzo/mafunzo	5/6
	Waza	Wazo /Mawazo	5/6
	Imba	Wimbo/Nyimbo	11/10
	Ponya	Ponyo/Maponyo	5/6
	Unda	Nyundo/Nyundo	9/10

wakati mwingine viambishi huweza kuambishwa mwanzoni mwa vitenzi pamoja na kiambishi tamati -o na kuunda neno linaloashiria tokeo la kitendo. Viambishi hivi ni kama katika mfano (52) hapa chini.

(52)	KITENZI	NOMINO
	Fika	M-fik-o
	Ja	M-j-o
	Lima	M-lim-o
	Kimbia	M-kimbi-o

Mtindo wa (52) umetumiwa kuunda maneno mapya ya elimu mbalimbali kama vile fizikia, kemia na baiolojia. Katika mfano (53) hapa chini ni majina ya fizikia.

(53)	M-chapuk-o	= Acceleration
	M-shikaman-o	= Adhesion
	Mu-ambatan-o	= Cohesion



Toke-o	= Resultant
Egeme-o	= Pivot
Badilish-o	= Replacement

### 2.3.5 KIAMBISHIAWALI U-

Kiambishiawali U- pia hujulikana kama U- ya udhahania. Udhahania ni fikra au hali inayowazika au kufikiriwa tu. Fikra hii ni juu ya jambo lisiloonekana wala kushikika. Udhahania katika maneno hudokezwa na kiambishi U- katika mnyambuliko ulioambishwa kiambishi awali U-.

Udhahania hujitokeza tu katika maneno yaliyonyambulishwa na kuambishwa u-. Maneno yawezayo kuambishwa u- ya udhahania ni vitenzi, vivumishi na majina ambayo huwa majina yaambishwapo kiambishi U- ni kama katika mfano (54)

- (54)
- U-zuri
  - U-kubwa
  - U-salama
  - U-chokozi
  - U-tetezi
  - U-hasama
  - U-zito

### 2.3.6. KIISHIO -U

-U inaweza vilevile kuwa kama kiishio. Idadi ya nomino zinazoundwa kwa kutumia kiishio -u ni ndogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya nomino zinazoundwa kwa kutumia viishio -i na -o. Nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi kwa kutumia kiishio -u humaanisha ama hali au mtu ambaye yuko katika hali fulani.

Nomino zinazomaanisha hali fulani huwa na kiambishi -U cha ngeli ya 11a. Zile zinazomaanisha mtu au watu walio katika hali fulani huchukua viambishi vya ngeli za 1 na 2. Mfano (55) hapa chini inadhihirisha hali hii.

(55)	KITENZI	NOMINO (NGELI1/2)	HALI(NGELI 11A)
	Tulia	Mtulivu/Watulivu	Utulivu
	Tukuka	Mtukufu/ Watukufu	Utukufu
	Legea	Mlegevu/Walegevu	Ulegevu
	Choka	Mchofu /wachofu	Uchofu
	Pungua	Mpungufu/Wapungufu	Upungufu

Vilevile kiishio -U kinaweza kutumiwa pamoja na kiambishi /ma/ cha ngeli ya 6 kama ilivyo katika mfano (56)

**(56) KITENZI NOMINO**

Onea Maonevu

Umia Maumivu

Sifu Majisifu

**2.3.7 KIISHIO -A**

Vokali -a haitumiwi kama kiishio cha kuunda nomino kutokana na vitenzi vyenye asili ya kibantu. Nomino nyingi ambazo huundwa kwa kutumia kiishio -a hazina viambishi vyovyote vya ngeli za nomino. Hii ndiyo sababu karibu nomino hizo zote huingizwa katika ngeli za 9 na 10 ambazo hazihitaji nomino kuwa na viambishi tofauti katika hali ya umoja na wingi.

Ikiwa kitenzi huishia kwa vokali -i hiyo -i ndiyo hutoweka na mahali pake huchukuliwa na kiishio -a kama katika mfano (57)

**(57) KITENZI NOMINO (NGELI 9/10)**

Fitini Fitina

Hoji Hoja

Faidi Faida

Fedhehi Fedheha

Hakiki Hakika

Vokali zingine katika nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi vya kukopwa zaweza kubadilika pia na kuwa -a kama ilivyo katika mfano (58).

(58)	KITENZI	NOMINO(NGELI 9/10)
	Jeruhi	Jeraha
	Fariji	Faraja
	Safiri	Msafara (ngeli 5)
	Bariki	Baraka

Mabadiliko haya hupatikana katika vitenzi vinavyoishia kwa vokali -u au -e hata ingawa vitenzi vinavyoishia kwa vokali -i ni haba sana, kama ilivyo katika mfano

(59)

(59)	KITENZI	NOMINO (NGELI 9/10)
	Heshimu	Heshima
	Hudumu	Huduma
	Husudu	Husuda
	Gharimu	Gharama
	Ruhusu	Ruhusa

Nomino zilizoundwa kwa kutumia kiishio -a huwa na maana mbalimbali. Nyingi humaanisha aina kadha za matokeo ya vitenzi kama tuonavyo katika mfano(60)

<b>(60)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO (MATOKEO)</b>
	Faidi	Faida
	Baridi	Baraka
	Lazimu	Lazima
	Dhuru	Dhara
	Sifu	Sifa

Kuna nomino zingine ziishiazo kwa vokali -a nazo huleta maana inayokaribia maana ya ngeli ya 1 la, yaani uhisi au udhahania wa maana, hata ingawa nomino zenyewe ni matokeo. Hata hivyo, baadhi ya maneno haya yamo katika ujenzi ghairi, ule uundaji wa neno ambao huenda kinyume na utaratibu wa kawaida. Mfano (61) hapa chini unadhihirisha.

<b>(61)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO</b>
	Ishi	Maisha
	Baini	Bayana
	Faniki	Fanaka
	Anisi	Anasa
	Ghofiri	Ghofira

Baadhi ya nomino hizi humaanisha vitu vinavyoweza kuguswa kama katika mfano (62).

<b>(62)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO</b>
	Nakili	Nakala
	Dhamini	Dhamana
	Katibu	Mkataba
	Ajiri	Ujira
	Ashiri	Ishara

Kuna pia nomino zingine zenye kiishio -a ambazo humaanisha mahali kwa mfano

(63)

<b>(63)</b>	<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO ( MAHALI)</b>
	Barizi	Baraza
	Durusi	Darasa

Pia ngeli nyingine zina majina ambayo yanaishia kwa kiishio -a kama tunavyoona katika mfano 64(a-f)

(64) a. KUNDI LA 1/2

<b>KITENZI</b>	<b>NOMINO</b>
Ogopa	Mwoga
Wia	Mwia
Wiwa	Mwiwa
Lima	Mkulima

b. KUNDI LA 5/6

**KITENZI**

**NOMINO**

Tata

Matata

Zoea

Mazoea

Nyonyota

Manyonyota

Kosa

Makosa

Teka

Mateka

c. KUNDI LA 7/8

**KITENZI**

**NOMINO**

Chana

Kitana

Pewa

Kipawa

d. KUNDI LA 11a

**KITENZI**

**NOMINO**

Shinda

Ushinda

Ogopa

Woga

Ganga

Uganga

e. KUNDI LA 3/4

**KITENZI**

**NOMINO**

Zinga

Mzinga

f. KUNDI LA 9/10

**KITENZI**

**NOMINO**

Oa

Ndoa

### 2.3.8 NOMINO KUTOKANA NA VIVUMISHI

Nomino zinazotokana na vivumishi kwa jumla ni chache ikilinganishwa na zile zinazotokana na vitenzi. Nomino zilizonyambuliwa katika kategoria hii huchukua viambishi awali kutoka ‘ngeli’ ya 11a na zina kiishio -a kama tuonavyo katika mfano (65)

(65)	VIVUMISHI	NOMINO
	-baya	Ubaya
	-jinga	Ujinga
	-gonjwa	Ugonjwa

Kama tulivyosema hapo awali, kiambishi tamati -a hasa hueleza hali ya mambo fulani. Katika kueleza unyambujaji wa nomino katika Kiswahili, tuliona kuwa unyambujaji huu ulihusu kuweka kiambishi awali kabla ya mzizi. Kawaida, vivumishi huwa havina viambishi awali vyao. Hii haimanishi kuwa vivumishi vinaweza vikajisimamia vyenyewe katika kufanya kazi. Kivumishi hupata hadhi yake kama neno katika sentensi kwa kuchukua kiambishi awali cha nomino kinachovumisha.



Ni dhahiri kutokana na maoni yetu hapo juu, kwamba nomino zinazotokana na unyambujaji zina mifanyiko kama ilivyo katika nomino nyingine. Namna moja ya kuonyesha jambo hili ni namna ambavyo nomino hizo zilizonyambuliwa zinachukua viambishi vitangulizi vya upatanifu kama ambavyo nomino nyingine zinavyofanya. Hii inaweza ikaelezwa kama ilivyo katika mfano (66) na (67).

(66)            Kisu    Kile    Kikali    Kimemkata .  
                  Visu    Vile    Vikali    Vimemkata .

(67)            U-funguo      U-mepotea .  
                  M-pishi        M-zuri .  
                  M-kulima      M-zuri .  
                  Ku-cheza      Hu-ko          Ku-lipendeza .  
                  mi-ti          Mi-wili        Mi-kubwa.

## 2.4      MUUNDO WA KIMSINGI WA NOMINO

Nomino ya Kiswahili, kama ilivyo katika lugha nyingi au labda zote, ni neno ambalo linataja mtu, mahala, wazo au jambo. Nomino huweza kuwa ni mofimu moja au zaidi zilizoambatishwa kwa mzizi wa neno. Mfano (68) ni nomino yenye mofimu moja iliyoambatishwa mzizi.

(68) M+zee = Mzee

Vilevile, kuna nomino zilizo na zaidi ya mofimu moja zinazoambatishwa kwenye mzizi wa neno. Mfano (69) unadhihirisha hili

(69) M+chek+esha+ji =Mchekeshaji.

Nomino ya Kiswahili hivyo inaweza ikaashiriwa kama ni (KMK+MZ). Lugha ya Kiswahili ina ugeuzajimaumbo ambao unatangamanisha kiambishi kitangulizi cha ngeli na nomino hivi kwamba mizizi ya nomino inakosa nguvu (Tazama 2.1). Nomino ni muhimu sana kwa kuwa kila sentensi ni lazima iwe na nomino au kiambishi kinachochukua nafasi ya hiyo nomino. Nomino kuu ndiyo neno-tangulizi katika KN chochote. Kikundi chote ni upanuzi wa kategoria hii na ikijulikana kama kitangulizi cha kikundi.

Inawezekana, kubadilisha neno-tangulizi na kundi katika kiunzi hicho cha sarufi wastani bila kusababisha mabadiliko ya muundo wote wa kisarufi. Sentensi katika mfano (70) hapa chini zina nomino kuu pamoja na viambishi vitangulizi vya umoja katika ngeli ya 7/8

(70) Ki-kombe      hi-ki              ki-kubwa      ki-tapotea.

Ki-jiko            hi-ki              ki-refu        ki-tatupwa.

(71) Ku-cheza      hu-ku              ku-baya        ku-nahofisha .

Hili linaonekana kote katika sentensi sawa na sentensi (71) ambapo viambishi vitangulizi ni vya kundi la 15, na kuathiri sentensi yote. Hivyo, ni kupitia kwa mfumo wa upatanifu ndipo uhusiano wa kisarufi wa nomino kwa sentensi yote unadumishwa. Kila nomino ina sifa mbili za upatanifu.

(i) Upatanifu wa viwakilishi vya upatanifu ambavyo vinatumika pamoja na mizizi ya viwakilishi, vimilikishi, vionyeshi na kadhalika.

(ii) Vivumishi vya upatanifu au nomino za upatanifu. Hivi ni vya maumbo sawa kama viambishi - vitangulizi vya ngeli na zinachukua mizizi ambayo inatumika kama vivumishi. Mfano (72) unaonyesha haya.

(72)	a)	M-ti	M-zuri	(3/4)
	b)	Ki-ti	Ki-zuri	(7/8)

Katika mfano (72) (a) M- inaleta mzizi -zuri kuwa na uhusiano wa upatanifu na m-ti.

#### 2.4.1 UDOGO WA NOMINO

Nomino za Kiswahili zinaweza kugawanywa katika sehemu tatu kutegemea ukubwa. Sehemu ya kwanza ni nomino za kawaida kama ilivyo katika mfano (73) hapa chini.

(73) Nyumba

Mji

Mtoto

Mbwa

Mtu

Mfano (74) hapa chini ni nomino ambazo zinaonyesha udogo wa nomino za mfano (73) hapo juu.

(74) Kijumba

Kijiji

Kitoto

Kijibwa

Kijitu.

Mfano (75) hapa chini ni nomino ambazo zinaonyesha ukubwa wa nomino za mfano (73) hapo juu.

(75) Jumba

Jiji

Jitoto

Jibwa

Jitu

Udogo wa nomino huundwa kutokana na baadhi ya ngeli za nomino wala sio kila ngeli. Ngeli hizo ni kutoka ya 1 hadi 10.

Ili kuunda nomino inayoonyesha udogo tulitumia kiambishi /ki/ katika hali ya umoja na /vi/ katika hali ya wingi. Mtindo wa kuongeza viambishi /ki/ na /vi/ hutumika kwa wingi hata ingawa baadhi ya nomino huwa na tofauti ndogo ndogo kama tunavyoona hapa chini.

#### 2.4.1.1 KUNDI LA 1/2

Katika kundi la 1/2 nomino zifuatazo zinaonyesha namna viambishi /ki/ na /vi/ vinavyoashiria dhana ya udogo. Mfano (76)

(76)	NOMINO (KUNDI 1/2)	UDOGO
	Mtu/watu	Kijitu/vijitu
	Mjakazi/Wajakazi	Kijakazi/Vijakazi
	Mjukuu/Wajukuu	Kijukuu/Vijukuu
	Mzee/Wazee	Kijizee/ Vijizee

Inaonekana kuwa mbali na kutumia viambishi /ki/ na /vi/ vya udogo, baadhi ya nomino hutumia viambishi /ji/ ambavyo ni viambishi vya nomino za ukubwa (ngeli 5). Viambishi kiji-au viji-huja mara tu kabla ya mzizi wa nomino. Nomino nyingi zinazotumia kiji-au viji-ni zile ambazo zina mizani zisizozidi mbili katika mzizi kama ilivyo katika mfano(77).

(77)	<u>Mtu</u>
	<u>Mwana</u>

Mwizi

Mke

Sehemu zilizopigwa mstari hazizidi mizani mbili. Kiambishi /ki/ au /vi/ huongezwa kwenye mzizi wenye mizani mbili au zaidi. Pale ambapo mzizi una mizani moja tunatumia viambishi vyote viwili/kiji/au /viji/. Iwapo mzizi una mizani mbili, na mizani ya kwanza iwe ni vokali, yaani ikiwa mzizi wa neno lenye mizani mbili huanzia kwa vokali, inatubidi kutumia viambishi vyote viwili /kiji/ au /viji/. Kupatikana kwa viambishi /kiji/ kutangulia mizizi ya nomino hupatikana pia katika nomino za ngeli zingine kama tunavyoona katika mfano (78)

(78)	NOMINO	KUNDI	UDOGO
	Mto/Mito	3/4	Kijito/Vijito
	Jicho/Macho	5/6	Kijicho/Vijicho
	Mbwa/Mbwa	9/10	Kijibwa/Vijibwa
	Njia/Njia	9/10	Kijia/ vijia

Viambishi /Ki/ na /Vi/ ni vya ngeli za 7/8. Nomino za kawaida zilizoko katika ngeli hizo huwa na viambishi hivyo. Ili kuthibitisha kwamba nomino ya ngeli ya 7/8 ipo katika hali ya udogo, kiambishi /ji/ huongezwa baada ya kiambishi cha udogo. Hivyo, viambishi kiji-vyaweza kutumiwa ikiwa mzizi una mizani zaidi ya mbili kama katika mfano (79) hapa chini.

<b>(79)</b>	<b>NOMINO (7/8)</b>	<b>UDOGO</b>
	Kibanda/vibanda	Kijibanda/Vijibanda
	Kitanda/Vitanda	Kijitanda/Vijitanda
	Kipande/Vipande	Kijipande/Vijipande
	Kibarua/Vibarua	Kijibarua/Vijibarua
	Kimada/Vimada	Kijimada/Vijimada

Nomino za ngeli zingine pia hujaribu kuiga mtindo huu licha ya kuwa na zaidi ya mizani mbili kwa hivyo nomino za hali ya udogo kama zifuatazo katika mfano (80) hutumika ingawa sheria tuliyoizungumza awali haifanyi kazi hapa.

<b>(80)</b>	<b>NOMINO</b>	<b>KUNDI</b>	<b>UDOGO</b>
	Kondoo/Kondoo	9/10	Kijikondoo/ Vijikondoo
	Kikapu/Vikapu	7/8	Kijikapu/Vijikapu
	Mshale/Mishale	3/4	Kijishale/Vijishale
	Karatasi/Makaratasi	5/6	Kijikaratasi/ Vijikaratasi

#### **2.4.1.2. KUNDI LA 3/4**

Katika kundi la 3/4 mifano ya nomino za hali ya udogo zinazotokana na nomino za ngeli ya 3/4 ni kama ilivyo katika mfano (81)

<b>(81)</b>	<b>NOMINO</b>	<b>UDOGO</b>
	Mlima/Milima	Kilima/Vilima
	Mkonge/Mikonge	Kikombe/vikonge
	Mkia/Mikia	Kijikia/Vijikia

### **2.4.1.3 KUNDI LA 5/6**

Nyingi ya nomino ya hali ya udogo katika kundi hili ama huanza bila ya kiambishi chochote au huanza kwa kiambishi/ma/. Kuonyeshwa kwa hali ya udogo hufuata mitindo kadha kutegemea kiambishi cha umoja. Nomino nyingi hasa zile nomino zenye asili ya kigeni hutumia viambishi /ki/ na /vi/ kama katika mfano (82).

<b>(82)</b>	<b>NOMINO (KUNDI) 5/6</b>	<b>UDOGO</b>
	Bibi/Mabibi	Kibibi/kibibi
	Kadhi/Makadhi	Kikadhi/Vikadhi
	Shamba/Mashamba	Kishamba/Vishamba

Baadhi ya nomino zenye kiambishi /ji/ cha umoja huwa na nomino za hali ya udogo kama ilivyo katika mfano (83)



<b>(83)</b>	<b>NOMINO</b>	<b>UDOGO</b>
	Jimbo/majimbo	Kijimbo/Vijimbo
	Jitu/Majitu	Kijitu/Vijitu
	Jini/Majini	Kijini/Vijini
	Jino/meno	Kijino/Vijino

viambishi /ki/ na /ji/ vimetumika pamoja ili kuunda nomino za udogo. Nomino za udogo zilizoko hapo juu hazionyeshi dalili za kuongezwa kwa kiambishi /ji/.

#### **2.4.1.4 KUNDI LA 7/8**

Awali tulisema kuwa baadhi ya nomino za ngeli hizi tayari ni udogo wa nomino za ngeli zingine, kama tuonavyo katika mfano (84).

<b>(84)</b>	<b>NOMINO(KUNDI) 1/2)</b>	<b>UDOGO</b>
	Mtoto/Watoto	Kijitoto/Vijitoto

Wakati mwingine unaweza ukatumia kitoto (Umoja) na vitoto (wingi). Nomino hizi huwekwa katika hali ya udogo kwa kutumia viambishi /ki/na /vi/ ambavyo ni viambishi vya nomino za ngeli za 7/8. Kwa sababu viambishi vya kuonyesha udogo wa nomino hutumika katika ngeli ya 7/8, nomino nyingi za ngeli hizi hazihitaji viambishi zaidi kama katika mfano (85).

- (85) Chakula-Vyakula  
Chama-Vyama  
Kiazi-Viazi  
Kichwa-Vichwa

#### 2.4.1.5 KUNDI LA 9/10

Umoja na wingi wa nomino za ngeli hizi huwa na umbo linalofanana. Nomino za ngeli hizi, hufuata taratibu sawa na zile tulizoeleza katika ngeli zingine zilizopita. Ikiwa mzizi wa nomino unayo mizani moja basi kiambishi /ji/ huongezwa katikati ya kiambishi cha nomino za udogo /ki/ na / bwa/ kama katika mbwa ili kuunda nomino ya kijibwa, kutokana na nomino ya kawaida hiyo. Mfano (86) ni mifano ya nomino zinazotumia kiambishi /ki/ na /vi/.

(86)	NOMINO	UDOGO
	Simba/simba	Kisimba/Visimba
	Kobe/Kobe	Kikibe/Vikombe
	Nazi/Nazi	Kinazi/Vinazi

Sio lazima nomino za ngeli hizi ziwe na kiambishi /n/ au /m/. Nomino za ngeli hizi ambazo huwa na kiambishi /n/ au /m/ hupoteza kiambishi hicho wakati nomino inapobadilishwa na kuwa katika hali ya udogo. Nafasi ya kiambishi hicho huchukuliwa na kiambishi cha udogo wa nomino ama /ki/au /vi/ kama

ilivyo katika mfano (87).

(87)	NOMINO	UDOGO
	Mboga/Mboga	Kiboga/Viboga
	Ndizi/Ndizi	Kidizi/Vidizi
	Njugu/Njugu	Kijugu/Vijugu

Hizo ndizo taratibu za uundaji nomino za hali ya udogo katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya mambo muhimu tuliyotaja ni kwamba viambishi vya udogo ni /ki/ na /vi/. Nomino ambazo zina mizizi yenye mizani moja au mbili na ya kwanza iwe vokali, huongezwa kiambishi /ji/ baada ya /ki/.

#### 2.4.2 UKUBWA WA NOMINO

Ukubwa wa nomino kwa kawaida husababisha maana ya ongezeko la umbo lililozidi la kawaida. Wakati mwingine, nomino za ukubwa zaweza kugusia wingi wa idadi na hata kuleta maana ya dharura au pengine mshangao.

Nomino za ukubwa kila mara huwa katika kundi la 5/6. Zinaweza kuwa na kiambishi ji-katika hali ya umoja au zisiwe na kiambishi ji- katika hali ya umoja lakini ni lazima kiambishi cha wingi kuwepo. Ingawa kiambishi /ma/ cha wingi hutumika sana, baadhi ya lahaja hutumia mi- badala yake. Mfano (88) unaonyesha ukubwa wa nomino.

(88)	NOMINO	UKUBWA
	Ny-umba	Jumba/Majumba
	Ny-ungu	Jungu/Majungu
	Ny-oka	Joka/Majoka
	Mw-izi	Jizi/Majizi

Kiambishi hiki /ji/ hubaki wakati nomino inapokuwa katika hali ya wingi. Hivyo basi kiambishi /ma/ cha wingi hakichukui nafasi ya /ji/ bali vyote hutumiwa pamoja. wakati mwingine, viambishi vingine vya nomino katika sentensi huwa sawa na viambishi vya ngeli za 5/6 na tunaweza tukaunda sentensi kama katika mfano (89)

(89) Jungu hili jipya la mama limevunjika  
Majungu haya mapya ya mama yamevunjika

Tumetaja kwamba kiambishi /ji/ hupatikana iwapo mzizi huanzia kwa vokali au ikiwa mzizi unao mizani moja ambayo pia huwa na kiambishi hiki /ji/ kama katika mfano (90)

(90)	NOMINO	UKUBWA
	Nguzo	Jiguzo/Majiguzo
	Kivuli	Jivuli/Majivuli

Nomino hizo zisizofuata taratibu tulizozieleza hapo juu ni chache sana. Mbali na

nomino zinazochukua kiambishi /ji/ katika hali ya umoja, kunazo nomino zingine ambazo hazina kiambishi hicho. Nyingi kati ya nomino hizo huwa na mizani mbili au zaidi kwenye viini kama katika mfano (91).

(91)	NOMINO	UKUBWA
	Paka	Paka/Mapaka
	Kikombe	Kombe/Makombe
	Kibanda	Banda/Mabanda

Ili kuunda nomino za ukubwa kutokana na nomino za kawaida kama hizo za hapo juu, kiambishi cha nomino hupotea. Nomino banda na kombe zimeundwa kwa kuchopoa kiambishi /ki/ cha ngeli ya 7.

Si rahisi kuonyesha ukubwa wa kila nomino ya Kiswahili. Tuangalie mfano(92)

**(92)** Farasi

Ili kueleza juu ya farasi mkubwa zaidi, matamshi 'jifarasi' husikika yakitumiwa na wengi ingawa huonekana kama hayafai matamshi haya. Nomino nyingi ambazo ziko katika hali hiyo huonyesha ukubwa kwa kutumia vivumishi kadha katika sentensi. Pia matumizi ya viambishi vya ngeli za 5/6 katika sentensi husaidia kuleta maana ya ukubwa kama ilivyo katika mfano (93)

**(93)** Farasi langu limenona sana halwezi kuruka ua.

Maelezo haya yatuonyesha kwamba ukubwa wa nomino unaweza kushirikisha

muundo wa sentensi mbali na umbo la nomino. Pia viambishi vyote vya nomino za ukubwa ni sawa na viambishi vya ngeli ya 5 katika umoja na kundi la 6 katika hali ya wingi.

Tuliona namna ambavyo ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili zinavyopatanishwa, ule uambishaji wa makundi yote ya nomino, unyambuaji ambapo tulichunguza viishio mbalimbali, muundo wa kimsingi wa nomino, udogo na ukubwa katika nomino. Haya yote kwenye faslu hii yalidhamiriwa katika kuelewa dhana ya kikundi nomino cha Kiswahili. Ujenzi au muundo wa nomino hushirikisha dhana zote hizo ili kueleweka ipasavyo. Katika sura tatu, hatukuwa na budi kwanza kujadili mofolojia ya nomino na kutoa mwangaza dhana ya uvumishaji wa nomino.

# TANBIHI

1. Ashton, E ( 1947) Swahili Grammar Including Intonation, London uk 10
2. Hata hivyo, kundi la 12/13 haliko katika Kiswahili, ingawa linapatikana katika baadhi ya lugha za kibantu.
3. Kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990) Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) chuo kikuu cha Dar-es-Salaam uk 32
4. Matthews, P. (1972) Inflectional Morphology Cambridge University Press Cambridge uk 3
5. Kapinga,M(1983) Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. TUKI, Dar-es-Salaam uk 44
6. Kama 5 hapo juu uk 46
7. Mbaabu , I (1992) Sarufi ya Kiswahili Longman,Nairobi uk 89
8. Kama 5 hapo juu uk 50
9. Pei, M (1966) Glossary of Linguistic Terminology. Columbia University Press, New York uk 63
10. Polome, E (1967) Swahili Language Handbook. Centre for Applied Linguistics. Washington. uk 77
11. Kama 10 hapo juu
12. Mdee, J (1986) Kiswahili: Muundo na matumizi yake. International publishers ltd. Nairobi uk 80
13. Kama 12 hapo juu uk 78.
14. -GA inapatikana katika Kiswahili kwenya vitenzi kama vile koroga, taga na kanyaga
15. Mitume yenye upatanisho 'wa'
16. Kama 13 hapo juu

## 3.0

## SURA YA TATU

### 3.0.0

### UVUMISHAJI WA NOMINO

Katika sura ya kwanza, tulitanguliza KN kama, ‘neni au kundi la maneno ambalo lina nomino au kiwakilishi kama neno kuu linalofanya kazi kama kiima, yambwa au kijalizo katika sentensi’<sup>1</sup>.

( Tafsiri ni yetu)

Matlaba yetu kwenye faslu hii ni kuangalia jinsi ambavyo nomino ya Kiswahili inavyovumishwa. Tuliangalia maneno amilifu kama vile vivumishi, vimilikishi, vionyeshi, idadi , sifa na kadhalika. Katika kupanua nomino hadi kuwa KN, Kiswahili hutumia kategoria tulizozitaja za maneno.<sup>2</sup> Tuliweza kutoa mifano mbalimbali kuthibitisha kwamba, nafasi ile ya nomino inaweza ikakaliwa na kiwakilishi<sup>3</sup>.

Vivumishi vya nomino ni yale maneno au kundi la maneno ambayo yanatoa maelezo kuhusu nomino kuu. Kwa mintarafu hii, inamaanisha kuwa KN sharti kibebe nomino itakayovumishwa kwa lengo la kuangaza upanukaji wake kupitia mfanyiko wa uvumishaji. Bila neno kama hilo (nomino huu), vivumishi hivyo havitakuwa na kazi ya kutekeleza katika kueleza nomino. Sentensi inayofuata katika mfano (1) ina maana tatu kuhusu neno kuu Mvulana.

1) Mvulana mrefu, aliyevaa fulana ya samawati, ndiye ninayemjua



Sentensi (1) hapo juu imebeba maana tatu inavyoelezwa na sehemu zilizopigwa mstari katika mfano (2)

- 2) i) Mvulana ni mrefu .
- ii) Mvulana amevaa fulana ya samawati .
- iii) Namjua mvulana .

Hivyo basi, vivumishi vyote vinatoa maana kuhusu nomino ambazo zinavumishwa. Maana kama hizo zinaweza zikaelezwa katika KN kama ilivyo katika mfano (3)

- (3) i) Mvulana mrefu .
- ii) Mvulana aliyevaa fulana ya samawati .
- iii) Mvulana ninayemjua .

Maelezo kama hayo yanatueleza mengi kuhusu nomino kuu. Katika lugha ya Kiswahili, kuna wakati ambapo kivumishi hakiingizwi. Kwa mintarafu hii, KN kitakuwa hakina kosa la kisarufi kutokana na kutokuwepo au kuwepo kwa kivumishi. Katika mfano (4) hapa chini, tunaweza kuchopoa vivumishi vyote na kubaki na neno kuu Mvulana likifanya kazi kama KN.

- 4) i) Mvulana yule mzuri .
- ii) Mvulana .

Katika mfano (4) hapo juu, tumechopoa maneno amilifu Mzuri na Yule.

### 3.1

### VIVUMISHI

Katika sarufi, hivi ni vipashio ambavyo hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino.<sup>4</sup>

Mebo (1989:53) anavieleza vivumishi kama maneno au kikundi cha maneno ambacho kinaelezea hali au sifa ya nomino. Kitendo hiki ambapo kivumishi kinatekeleza wajibu wa kutoa maelezo fulani kuhusu nomino, huelezwa kama uvumishaji wa nomino ambapo hivi sasa nomino husika inakuwa na sifa mpya.

Vivumishi katika lugha ya Kiswahili huwa na upatanisho na zile nomino zinazovumisha. 'upatanifu unaonyeshwa na' mfumo wa viambishiawali vinavyoorodheshwa katika mofolojia ya Kiswahili, zamani zikielezwa na nambari 1-15.<sup>5</sup>

( Tafsiri ni yetu)

Vivumishi vinafanywa kupatana na nomino kwa kuviambisha na viambishi vitangulizi vya kundi la majina ya nomino zinazohusika ama katika umoja au wingi kulingana na jinsi ambavyo hali ilivyo. Maw ( 1969: 75) pia ana maoni kama haya. Baadhi ya hivi vivumishi vinaonyeshwa katika mfano (5) hapa chini.

- 5)            -baya  
               -tamu  
               -zuri  
               -dogo  
               -kubwa  
               -refu  
               -fupi  
               -nene  
               -eusi  
               -eupe  
               -ekundu  
               -embamba  
               -chungu

Mifano hiyo hapo juu ni mizizi ya vivumishi.

### **3.1.1            VIVUMISHI VYA SIFA**

Vivumishi vya sifa ni maneno yanayotaja tabia, yaani namna watu walivyo au jinsi vitu vilivyo.<sup>6</sup> Baadhi ya vivumishi hivi vinachukua upatanisho wa kisarufi kwa kuambatisha viambishi ngeli na vile visivyochukua viambishi ngeli katika upatanisho wa kisarufi.

Vivumishi vya sifa vya upatanisho wa kisarufi ni vile vyenye kuchukua viambishi awali vya jina linalovumishwa kama ilivyo katika mfano ( 6) hapa chini.

(6)

<b>VIVUMISHI VYA SIFA VINAVYOCHUKUA VIAMBISHI NGELI KATIKA UPATANISHO WA KISARUFI</b>	<b>UPATANISHO WA KISARUFI BAINA YA MAJINA NA VIVUMISHI</b>
-baya	Mtu mbaya, watu wabaya
-kubwa	Kikombe kikubwa, vikombe vikubwa
-refu	Mlima mrefu, milima mirefu
-uchafu	Kiti kichafu, viti vichafu
-bovu	Sanduku bovu, masanduku mabovu

Ngeli ambazo mifano (6) inapatikana inaelezwa katika mfano (7) hapa chini.

- 7)
- i)  $1/2$  : Mtu mbaya
  - wg : Watu wabaya
  
  - ii)  $7/8$  : Kikombe kikubwa
  - wg : Vikombe vikubwa
  
  - iii)  $3/4$  : Mlima mrefu
  - wg : Milima mrefu
  
  - iv)  $5/6$  : Sanduku baya
  - wg : Masanduku mabaya

Uwezekano wa kuambatisha viambishi vya majina kwenye mashina ya vivumishi unasababisha uwezekano wa vivumishi kutumika kama majina. Kwa njia hiyo, tunaweza kupata mifano kama katika mfano (8) i-ii hapa chini :

- 8) i) Chema chajiuza, kibaya chajitembeza .  
ii) Kipya kinyemi, ingawa kidonda .

Chema katika (8) i, na Kibaya katika (8)ii ni vivumishi vya sifa vilivyotumika kama majina.

Kuna vivumishi vya sifa visivyochukua viambishi ngeli vya upatanisho wa kisarufi. Viambishi hivi ni maneno ya mkopo yatokayo katika lugha za kigeni kama kiarabu au lugha nyinginezo kama tuonavyo katika mfano (9) hapa chini.

- 9) -Stadi  
-Safi  
-Bora  
-Nadhifu

Ingawa havichukui viambishi ngeli, tunaweza tukatunga sentensi ambazo zinawekwa katika kundi maalum kama katika mfano (10) hapa chini.

- (10) i) 1/2 : Mwindaji Stadi  
wg : Wawindaji Stadi
- ii) 3/4 : Mlango safi  
wg : Milango safi
- iii) 7/8 : Kitu bora  
wg : Vitu bora
- iv) 5/6 : Vazi nadhifu  
wg : Mavazi nadhifu

Kisintaksia, vivumishi ni tofauti na nomino vivumishi hufuata, na wala haviji mbele ya nomino, kama inavyodhihirika katika mfano (11) hapa chini.

- (11) i) Mvulana mzuri  
ii) \*Mzuri mvulana

Pia inawezekana kuongeza neno la kipeo<sup>7</sup> kando ya kivumishi wala hili halifanyiki kwa nomino kama inavyoonekana katika mfano (12) hapa chini.

- 12) i) Mvulana mzuri sana .  
ii) \*Mvulana sana mzuri .

Kutokana na sababu kwamba neno la kipeo linafuata kivumishi kama katika (12)i, linamaanisha kwamba limeongezewa kivumishi na wala sio nomino. Lakini katika (12) ii, neno la kipeo sasa linafuata nomino punde, na hivyo kukifanya kirai katika sentensi hiyo isiwe sawa kisarufi na hivyo basi KN chote si sawa kisarufi.

Pale ambapo kivumishi kinatumiwa kueleza 'mtu' au 'watu' neno halisi mtu hucholewa kwa vile linachukuliwa kueleweka. Kuchopolewa kwa neno halisi hutokana na kanuni ya kijumla ambayo imo kwenye akili laza ya mzungumzaji kama inavyoonekana katika mfano (13) .

13)	i)	Mvulana	mrefu
		∅	mrefu
			(Mvulana/ msichana)

	ii)	Watu	Wengi
		∅	Wengi
			(Wao)

	iii)	Watu	Wangapi ?
		∅	Wangapi ?
			(wao)

Katika Kiswahili, hatuna kiwango linganishi kinachohusu vivumishi. Hata

hivyo, kiwango linganishi kama tunavyokijua katika Kiingereza kinawakilishwa kwa namna nyingine katika Kiswahili kama inavyoonekana katika mfano (14)

14) i) Kwa matumizi ya hata .

Nitafanya akili gani hata asinichape.

ii) Kwa matumizi ya hadi .

Walingoja tangu asubuhi hadi jioni.

iii) Kwa matumizi ya mpaka .

Toka sayari ya zuhura mpaka dunia ni umbali gani?.

iv) Kwa matumizi ya Au, Ama .

Vyombo utaleta wewe ama tutaleta sisi?

Utakuja au vipi ?

v) Kwa matumizi ya bila .

Siwezi kukaa bila mke .

vi) Kwa matumizi ya Kuliko .

Yeye ni mkubwa kuliko nduguye .

vii) Kwa matumizi ya kushinda .

Nairobi ni mji mkubwa kushinda Mombasa .



Kiwango upeo<sup>9</sup> kinatolewa kutumia kivumishi katika umbo lake sahili, kwa umbo halisi, umbo la msingi ambalo halijafanyiwa uambishaji wa aina yoyote.

### 3.1.2 VIVUMISHI VYA IDADI

Vivumishi vya idadi ni maneno ambayo yana uamilifu wa kuonyesha idadi ya watu, vitu au ya mambo na huonyeshwa katika umoja na wingi.<sup>10</sup> Maneno hayo yanaongeza maana na yanaweka wazi wingi au uchache wa mambo yanayovumishwa, sababu yanajulisha idadi inayohusika.

Jespersen (1924:202) anasema kuwa katika lugha zote za ulimwengu, vivumishi vya idadi huwa na kazi ya kuonyesha idadi ya vitu mbalimbali. Katika Kiswahili, vivumishi vya idadi vinaweza kutoa maana ya jumla kama tunavyoona katika mfano (15)

- 15)            i)     -chache  
                 ii)    -ingi  
                 iii)   -kubwa

Katika sentensi, tunakuwa na sentensi zifuatazo katika mfano (16)

- 16) i) Wafanyikazi wachache  
ii) Wawindaji wengi  
iii) Kundi kubwa

Hata hivyo, katika Kiswahili, idadi ya vitu huonekana wazi zaidi kwa vivumishi vya hesabu kama katika mfano (17)

- 17) -Moja  
-wili  
-tatu  
-nne  
-tano  
\*sita  
\*saba  
-nane  
\*tisa  
kumi

\* Hizi zimeazimwa kutoka kiarabu. Nyingine zina asili ya kibantu. Vivumishi vya hesabu huweza kugawanyika katika mafungu mawili.

- i). Vivumishi vya hesabu vinavyochukua viambishi vya majina yanayovumishwa .

ii). Vivumishi vya hesabu visivyochukua viambishi.

Vivumishi vinavyochukua viambishi ni vichache kama tunavyoona katika mfano

(18)

18)

i) -moja

Mkulima mmoja

ii) -wili

Mikebe miwili

iii) -tatu

Vitu vitatu

iv) -nne

Matunda manne

v) -tano

Nyumba tano

vi) -Mahali

Mahali patano

vii) -nane

Watu wanane

Katika Kiswahili, neno 'kumi' likitumika katika wingi huwa 'makumi'. Unaweza ukasikia watu wakitunga au kusema sentensi zifuatazo katika mfano (19)

- 19) i) Watu kumi na tatu .  
ii) Watu kumi na watatu .

Hata hivyo kuhusu 'makumi' mengine, watu husema ifuatavyo kama ilivyo katika mfano (20)

20)	Ishirini	(20)
	Thelathini	(30)
	Arobaini	(40)
	Hamsini	(50)
	Sitini	(60)
	Sabini	(70)
	Themanini	(80)
	Tisini	(90)
	Mia	(100)

Miongoni mwa watu, orodha hiyo katika mfano (20) itapewa majina kama katika mfano (21)

21)	Makumi	mawili	(20)
	Makumi	matatu	(30)
	Makumi	manne	(40)
	Makumi	matano	(50)
	Makumi	sita	(60)
	Makumi	saba	(70)
	Makumi	Manane	(80)
	Makumi	tisa	(90)
	Mia		(100)

Katika Kiswahili, hesabu inayofuata 'makumi' zinaongezwa kwa kuingiza neno 'na' ikifuatwa na hesabu inayohitajika. Hizi hesabu zinazochukua upatanisho wa sarufi zinaambatishwa na upatanishi unaofaa kama ilivyo katika mfano (22) hapa chini :

- (22) i) Watoto ishirini na wawili .
- ii) Viti kumi na vinne .
- iii) Machungwa hamsini na matano .

Kuhusu mia, mpangilio wake katika sentensi huwa tofauti. Neno mia hutangulia. Tunapotaka kusema mia kadhaa, idadi hufuata neno hili, kama katika mfano (23).

23)	Mia moja	(100)
	Mia mbili	(200)
	Mia tatu	(300)
	Mia nne	(400)
	Mia tano	(500) n.k

Kuhusu elfu na milioni, mpangilio ni kama ilivyo katika mfano (22) ambapo idadi hufuata maneno haya.

Nomino kila mara hutangulia idadi. Ikiwa kuna kivumishi cha sifa na idadi katika KN, kivumishi cha sifa kila mara hufuata idadi na vyote vinatanguliwa na nomino vinavyovumisha kama ilivyo katika mfano (24).

- 24) i) Mtu mmoja mzuri .  
 ii) Watu wawili wazuri .

Ikiwa mpangilio kati ya kivumishi cha sifa na kivumishi cha idadi utabadilishwa, jambo jingine litaashiriwa ambalo hatukulishughulikia kwa vile lipo nje ya upeo wetu wa sasa. Hata hivyo, ni vizuri kuzingatia kwamba mpangilio wa kivumishi cha sifa na idadi unaweza ukabadilika. Vinaweza vikabadilishana nafasi kwa sababu moja au nyingine, lakini mpangilio wa nomino na kivumishi cha idadi kamwe hautangulii nomino. '-ngapi' hutumika katika idadi na hufanya kazi vilevile kama kivumishi. Mfano (25) unafafanua.

- 25)            i)     Watu wa-ngapi?  
                 ii)     Vitu vi-ngapi ?  
                 iii)    Miti mi-ngapi?  
                 iv)    Machungwa ma-ngapi?  
                 v)     Pahali pa-ngapi?

Kawaida, 'ngapi' huchukua kiambishi kitangulizi cha nomino kinachoelezea idadi.

Hesabu tulizozitoa katika mfano(20 ) ni za maneno ya kiarabu. Mahali pengine kama Unguja au Mombasa, watu wanatumia maneno ya kiarabu hata kwa hesabu za idadi moja moja. Orodha nzima ya hesabu hizo ni kama ifuatavyo kwa mujibu wa Kapinga(1983: 74) kwenye jedwali (i) hapa chini :

*Jedwali (i)*

<b>ORODHA</b>	<b>MAENDELEZO KWA Kiswahili</b>	<b>MAENDELEZO YA KIARABU KWA VITAMKWA VYA Kiswahili</b>
1.	Wahed	Wahed
2.	Theneni	Ithneni
3.	Thelatha	Thalatha
4.	Arbaa	Arbaa
5.	Hamsa	Khamsa
6.	Sita	Sita
7.	Saba	Saba
8.	Themania	Thamania
9.	Tisa	Tisa
10.	Ashara	Ashara
11.	Hidashara	I-da-ashara
12.	Thinashara	Ith-na-ashara
13.	Thelatha-ashara	Thelatha-tashara
14.	Aruba-tashara	Arubaa-ta-ashara
15.	Hamsta-ashara	Khamsta-ashara
16.	Sitaashara	Sita-ashara
17.	Sabataashara	Sabaata-ashara
18.	Theminita-ashara	Thamanita-ashara
19.	Tisataashara	Tisia-ata-ashara
20.	Ishirini	Ishirini
30.	Thelathini	Thelathini
40.	Arubaini	Arbaini
50.	Hamsini	Khamisini
60.	Sitini	Sitiini
70.	Sabini	Sabiini
80.	Thamanini	Thamanini
90.	Tisini	Tisiini



Pia, hesabu za mafungu hutumika kama vivumishi vya idadi kama tuonavyo katika mfano (26).

26.           Nusu (1/2)  
              Theluthi (1/3)  
              Robo (1/4)  
              Kasorobo (3/4)  
              Khumsi (1/5)  
              Sudusi (1/6)  
              Subui (1/7)  
              Thumuni (1/8)  
              Ushiri (1/10)

### 3.2 VIELEZI KIASI

Mbali na idadi , lugha ya Kiswahili ina vielezi kiasi. Baadhi ya vielezi hivi ni kama vile -ote, o-ote, -ingine, -ingi, kila na kadhalika. Kama vile vivumishi vya idadi, vielezi vya kiasi huchukua viambishi vitangulizi vya majina ya nomino vinavyoeleza. Hata hivyo, kila huwa tofauti kidogo kwa maana haichukui kiambishi kitangulizi chochote kama ilivyo katika mfano (27).

27.    i)     Kila mtu .  
       ii)    Kila ng'ombe .

- iii) Kila mti .
- iv) Kila sufuria .

Tofauti na ilivyo katika vielezi vingine vya kiasi, kila kila mara hutangulia nomino inayoeleza wala haifuati nomino hiyo, kama tuonavyo katika mfano (28)

- (28) i) \* mtu kila .
- ii) \*ng'ombe kila .

Pili, kila huchukua tu nomino katika umoja tofauti na vielezi vingine vya kiasi ambavyo vinavumisha umoja na wingi wa nomino. Kwa mintarafu hii, hauwezi ukasema mifano (29)

- (29) i) \* Kila watu .
- ii) \*Kila Maduka .

Hata hivyo, mfano (29) hapo juu yanaweza kukubalika au kusemwa ikiwa nomino inayohusika inaelezwa kwa muktadha wa jamii moja wala sio kiubinafsi kama inavyoonekana katika mfano (30)

- (30) i) Kila watu na utamaduni wao .

Katika (30) hatuungalii watu kama mtu mmoja mmoja bali kama kundi

linalojenga jamii moja kuhusu kielezi kiasi -ote.

### 3.2.1 MATUMIZI YA -ENYE

Kivumishi " -enye" huonyesha umilikisho wa mali, tabia, hali au cheo. Ashton(1944:63) anaeleza kuwa "-enye" hutumika kueleza "kumiliki" au " kuwa na kitu". Tuangalie mfano (31)

31) i) Mzee mw-enye busara.

Katika mfano (31) hapo juu, maana yake ni mzee anayemiliki busara. Neno "mwenye" katika sentensi hiyo inatufahamisha kwamba 'busara' imekuwa mali ya mtu. Basi -enye kwa jumla huonyesha jambo fulani lipo chini ya mamlaka ya nani. "-enye" huchukua viambishi-ngeli vya majina katika upatanisho wa kisarufi. Kwa mintarafu hii, huweza kusimama peke yake kama kiima cha kitenzi. Na huwa na maana ya mtu anayekuwa na kitu au hali fulani. Kwa maana hiyo '-enye' hutumika katika methali kadha wa kadha kama tunavyoona katika mfano (32) hapa chini.

- (32)
- i) Mwenye kelele hana neno.
  - ii) Mwenye kovu usidhani kapoa.
  - iii) Mwenye kubebwa hujikaza.
  - iv) Mwenye kuumwa na nyoka akiona ungom'o hushtuka.
  - v) Mwenye macho haambiwi tazama.

Kama tuonavyo katika mifano ya hapo juu, -enye huhitaji daima jina au kitenzi cha kukitawala ambacho ni jibu la "-enye" na nini? Upatanisho wa "-enye" ni kama ufuatavyo katika mfano (33)

33)	KUNDI	
	1/2	Mw-enye W-enye
	3/4	W-enye Y-enye
	5/6	L-enye Y-enye
	7/8	Ch-enye VY-enye
	9/10	Y-enye Z-enye

11/10a W-enye

Z-enye

15/17 Kw-enye

16 P-enye

17 Mw-enye

'-enye' kwa ujumla inatumika katika vikundi nomino kukiwa na nomino au kibadala chake kuelezea hali ya kitu fulani. Kwa maneno mengine, '-enye' ni aina ya kivumishi kinachoweza kutumiwa au kuvumisha nomino kwa kutumia kile nomino inamiliki kama ilivyo katika mfano (34)

- (34) i) Msichana mwenye rinda  
ii) Msichana mwenye rinda jekundu

KN katika (34) (ii) hapo juu utawekwa dhahiri kama ilivyo katika mfano (35)

(35) Msichana aliye na rinda jekundu.

Katika hali kama hiyo '-enye' haitumiki.

### 3.2.2

### MATUMIZI YA -INGINE

'- Ingene' vilevile ni kivumishi chenye maana ya, 'sehemu ya', 'baadhi ya' au 'zaidi ya'. '-ingine' huonyesha vitu tofauti na vingine vya aina ile ile kama inavyoonyeshwa katika mfano (36)

- (36)
- i) Wasichana wengine waliimba
  - ii) Watoto wengine walicheza
  - iii) Visu vingine vilinolewa
  - iv) Mti mwingine ulikatwa

Katika mfano (36) (i) tunamaanisha makundi mawili au zaidi ya wasichana ambao walitofautiana katika kuimba na kutoimba. Yaani kundi moja liliimba na kundi jingine halikuimba. Kivumishi '-ingine' hutumika pia kama kiima-kiwakilishi kama ilivyo katika mfano (37) hapa chini

37) Wengine waliimba .

Tunamaanisha 'baadhi ya' tuseme wasichana, kivumishi hicho kinaposimama na jina fulani, huchukua viambishi-ngeli vya lile jina kama ilivyo katika mfano (38) hapa chini.

- (38) 1/2 Mw-ngine  
wengine
- 3/4 Mw-ngine  
mingine
- 5/6 Lingine/jingine  
mengine
- 7/8 Kingine  
vingine
- 9/10 Nyingine  
zingine
- 11/10a mwingine  
zingine
- 15/17 kwingine
16. pengine
17. mwingine

### 3.2.3

## MATUMIZI YA -ENYEWE

'-enyewe' ni kivumishi kinachoeleza msisitizo. Maana nyingine hutumika kuvumisha vitu visivyokuwa nafsi kwa ajili ya kutia mkazo juu ya jambo linalojulikana kwa wanaoshiriki. Mfano (39) unathibitisha.

39) i) Leta barua zenyewe.

Katika (39) hapo juu tunamaanisha tunataka mtu alete barua zile tulizozitaja. Lakini mtu akitoa kauli zifuatazo katika mfano (40)

40) i) Mwenyewe hayupo .  
ii) Mwenye mali hii hayupo .

Maana yake mtu anayemiliki mahali fulani, au mali fulani, au cheo ametoweka. Ndio kusema neno '-enyewe' linaonyesha umilikisho, mamlaka na madaraka. 'enyewe' vilevile huchukua viambishi-ngeli vya majina kwa ajili ya upatanisho wa kisarufi kama tuonavyo katika Jedwali (iia) hapa chini.



*Jedwali (ii)a*

1/2	Mwenyewe Wenyewe
3/4	Wenyewe Yenyewe
5/6	Lenyewe Yenyewe
7/8	Chenyewe Vyenyewe
9/10	Yenyewe Zenyewe
11a/10a	Wenyewe Zenyewe
15/17	Kwenyewe
16	Penyewe
17	mwenyewe

### 3.2.4 MATUMIZI YA -OTE

‘-ote’ ni kivumishi kinachoonyesha kuhusika kwa jambo kwa wingi wake bila kupungua. Tuone mfano (41)

(41) i) Ameiba chakula chote.

Tunataka kusema kuwa mwizi amechukua chakula chake kwa wingi wake, bila kuacha sehemu fulani. Neno hilo hutumika mara nyingi pamoja na viwakilishi vya nafsi kama katika mfano (42) hapa chini.

42) i) Sisi sote .

ii) Ninyi nyote .

‘-ote’ huchukua viambishi-ngeli vya jina linalovumishwa, isipokuwa majina ya ngeli ya 1 kama tuonavyo katika mfano hapa chini.

43) i) mtu .

ii) \*mtu wote .

Jina hili halivumishwi na "-ote". Kirai katika (43) (ii) si sawa kisarufi. Bali tutasema ‘mtu mzima’. Kivumishi ‘-ote’ huweza kutumika kama kiima kiwakilishi-jina ambalo habari zake zajulikana kwa wanaohusika. Tuone mfano

(44) hapa chini.

(44) i) Lote limeliwa na mbwa .

" Lote" litawakilisha kwa mfano samaki, kuku kutegemea jambo la mazungumzo ya wahusika. Vivumishi hivi huonyesha vizuri usawazisho wa matamshi vinapotumika, katika upatanisho wa kisarufi pamoja na majina. Upatanisho wa kisarufi baina ya majina na vivumishi hivyo huleta ujirani wa vokali zinazoelekea kutamkwa kwa urahisi kwa kuzifupisha kama katika jedwali (ii)b

*Jedwali (ii)b*

<b>UJIRANI WA VOKALI</b>	<b>USAWAZISHO WA MATAMSHI</b>	<b>MIFANO</b>	<b>MATOKEO</b>
A + E	E	Wa + enye	W-enye
A + I	E	Wa + ingine	W-ngine
A + O	O	Wa + ote	W-ote
I + E	Y + E	Vi + enyewe	Vy-enyewe
I + I	I	Vi + ingine	V-ngine
I + O	Y + O	I + ote	Y-ote
U + E	W + E	Ku + enye	Kw-enye
U + I	W + I	Ku + ingine	Kw-ngine
U + O	W + O	Ku + ote	Kw-ote
Ki + O	Ch + O	Ki + o + ki + ote	Cho-chote

### 3.2.5

## MATUMIZI YA O-OTE

'O-ote' ni kivumishi kitokanacho na mwunganiko wa maneno mawili, yaani -o rejeshi na-ote. Upatanisho wa kisarufi wa-ote umeelezwa katika jedwali(iii)

*Jedwali (iii)*

MAJINA YA NGELI MBALIMBALI, UPATANISHO WA KISARUFI BAINA YA JINA NA -O -OTE

MAJINA	UPATANISHO WA KISARUFI	
	UMOJA	WINGI
Mkulima - wakulima	Mkulima yeyote	Wakulima wowote
Mti - miti	Mti wowote	Miti yoyote
Kiti - viti	Kiti chochote	Viti vyovyote
Jina - majina	Jina lolote	Majina yoyote
Njia - njia	Njia yoyote	Njia zozote
Ugonjwa - magonjwa	Ugonjwa wowote	Magonjwa yoyote
Ufa - nyufa	Ufa wowote	Nyufa zozote
Mahali - mahali	Mahali popote Mahali mwomwote	Mahali kokote
Kucheza - kucheza	Kucheza kwokwote	Kucheza kwokwote

### 3.3.

## VIMILIKISHI

Kamusi sanifu ya isimu na lugha inaeleza vimilikishi kama aina ya maneno ambayo huonyesha uhusiano wa kitu kuwa mali ya mtu.<sup>11</sup> Kapinga (1983:75) pia anakubaliana na maoni haya. Vimilikishi tulivyovijadili hapa ni sita navyo ni -angu, -etu,-ako, -enu, -ake, na -ao. Maneno haya yameundwa kwa mizizi ya -a-

unganifu, ikiwa ni mzizi wa kwanza wa vimilikishi pamoja na mizizi ya -angu, -ako, -ake na kadhalika.

Vimilikishi -angu, -ako, -ako, -etu, -enu huchukua viambishi vya ngeli ili kuleta upatanisho wa kisarufi baina ya majina na vimilikishi. Kawaida, vimilikishi hufuata nomino na kuchukua viambishiawali vya nomino hivyo kama katika mfano (45)

- (45)
- |      |        |   |                |
|------|--------|---|----------------|
| i)   | $1/2$  | : | Mtoto w-angu   |
|      | wg     | : | Watoto wa-angu |
| ii)  | $3/4$  | : | Mti w-angu     |
|      | wg     | : | Miti y-angu    |
| iii) | $5/6$  | : | Jino l-angu    |
|      | wg     | : | Meno y-angu    |
| iv)  | $7/8$  | : | Kiti ch-angu   |
|      | wg     | : | Viti vy-angu   |
| v)   | $9/10$ | : | Nguo y-angu    |
|      | wg     | : | Nguo z-angu    |

Katika mfano 30 (i) na (ii) kuna mabadiliko ya kifonolojia yaliyofanyika yaliyoathiri viambishiawali vya nomino kwa vile viliambishwa katika mizizi ya vimilikishi. Vimilikishi hivi mbali na kuonyesha ule umilikaji, pia vinasaidia kuvumisha nomino kama tuonavyo katika mfano (46)

- (46) i) Mtoto wangu yule.
- ii) Kitanda chako hicho.
- iii) Jicho langu hili.

Wakati vimilikishi vina uamilifu wa kibainishi kwa nomino, huwa karibu kila mara vina vivumishi vya ziada, ambavyo vinafafanua kwa nini vimilikishi hivyo vitatu katika virai hapo juu vina vionyeshi vinavyovifuata. Wakati vionyeshi hivyo vinapoondolewa, vimilikishi hasa hufanya kazi kuonyesha umilikishi.

Nafsi ya pili na tatu zinaweza zikaendelezwa kwa kutumia aina mbili ya vimilikishi. Umbo moja unatokana na kule kudondoshwa kwa kiambishiawali kinachotangulia mzizi wa neno la kumiliki. Hivyo, unaweza ukatumia mfano (47) a na b kama ilivyo hapa chini.

- (47) a) i) Mama yako .
- ii) Mwana wako .
- iii) Shamba lako .
- iv) Tunda lako .

- b. i) Mamako
- ii) Mwanako
- iii) Shambalo
- iv) Tundalo

Hata hivyo, kimilikishi kinaweza kikatangulia nomino na kinapofanya hivyo, sababu huwa ni msisitizo kama inavyoonekana katika mfano (48)

48) Wangu mpenzi amenitaliki.

Mfano (48) hapo juu unasisitiza jambo kuwa'wangu'mpenzi ameniacha. Kuna kimilikishi chenye kutumia mofimu -a. Huwa inakubaliana na kinachomilikiwa kuzidi kinachomiliki. Hili linaelezwa katika sentensi zifuatazo katika mfano (49)

- 49) i) Shamba l-a baba .
- ii) Mtoto w-a mjomba .
- iii) Kitabu ch-a mwalimu .
- iv) Nyumba y-a mkulima .

Hiki ndicho kivumishi cha -a- unganifu .

### 3.4 -A UNGANIFU

-A unganifu ni kiangama cha aina ya kiambishi tamati, kinachoambatishwa kwenye viambishi-ngeli kwa ajili ya kuleta maana inayotakiwa katika upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno. -A unganifu hutumika katika kuunda vivumishi na vihusishi<sup>12</sup> Hivyo, tunaona kuwa katika (49) i) kimilikishi kinapatana na shamba wala sio baba. Katika Kiswahili, vivumishi vya -A unganifu vinahusika kueleza uhusiano wa kimilikishi kati ya kisabiki cha nomino na nomino nyingine kama katika mfano (50)

- (50)
- i) Kisu ch-a mkulima .
  - ii) Mbuji w-a baba .
  - iii) Vijiko vy-a wapishi .

Pia vimilikishi vya -A unganifu vinahusika kueleza uhusiano wa kimilikishi kati ya kisabiki cha nomino na kiulizi kama inavyoonekana katika mfano (51)

- 51)
- i) Nguo z-a nani?
  - ii) Kitanda ch-a nani ?
  - iii) Mipira y-a nani ?

Katika mazungumzo ya kawaida, vimilikishi ndivyo vina uhusiano wa karibu sana na nomino kama katika mfano (52)



- 52)            i)      Vijiko vyangu hivi -  
                 ii)     Watoto wangu wafupi .  
                 iii)    Ng'ombe wako wanne .

Hivyo, maneno yoyote yanayovumisha nomino katika KN yanakuja baada ya kimilikishi ambacho kinafuata baadaye nomino kinachovumisha.

### **3.5    VIONYESHI**

Vionyeshi ni vipashio vinavyorejea kwenye muktadha wa mahali alipo msemaji. Kwa upande mwingine, kivumishi onyeshi ni kivumishi ambacho uamilifu wake ni uonyeshi. Fauka ya hayo, kiwakilishi onyeshi ni kiwakilishi ambacho uamilifu wake ni uonyeshi.

Hartmann na Stork ( 1972: 61) wanasema;

Vionyeshi ni maneno kama vile hili, lile, hivi, hivyo na kadhalika, kuonyesha watu au vitu mahususi.<sup>13</sup>

(Tafsiri ni yetu)

Katika Kiswahili, vivumishi vionyeshi ni vitatu tu kwa ajili ya kuonyesha kitu cha karibu navyo huundwa kutokana na mashina-ha-, hi- hu-. Kwa minajili ya kuonyesha kitu cha mbali, kuna kionyeshi kimoja ambacho shina lake ni -ile. Maneno yanayoonyesha jambo lililokwishatajwa huundwa kwa kuambatisha kiangama -o rejeshi kwenye vionyeshi hivyo vya ujirani.

### 3.5.1

### VIONYESHI VYA UJIRANI

Vivumishi vya kuonyesha karibu huundwa kwa kuongezwa viambishi-ngeli kwenye mashina ya maneno, ha-, hi-, na hu, kama ilivyo katika jedwali (iv)

*Jedwali (iv)*

NGELI	MASHINA YA VIONYESHI VYA KARIBU: UMOJA NA WINGI	VIAMBISHI NGELI: UMOJA NA WINGI	MANENO MAZIMA
1	1 hu- 2 ha-	1 -yu 2 -wa	huyu hawa
2	3 hu- 4 hi-	3 -u 4 -i	huu hii
3	5 hi- 6 ha-	5 -li 6 -ya	hili haya
4	7 hi- 8 hi-	7 -ki 8 -vi	hiki hivi
5	9 hi- 10 hi-	9 -i 10 -zi	hii hizi
6	11 hi- 12 hi-	11 -u 12 -zi	huu hizi
7	13 hu- 14 ha-	13 -u 14 -ya	huu haya
8	15 hu- 16 ha-	15 -ku 16 -pa	huku hapa
9	17 hu- 18 hu	17 -mu 18 -ku	humu huku

Kutokana na jedwali (iv) itaonekana kuwa vokali ya shina la kionyeshi cha ujirani h+ vokali hulingana kabisa na vokali ya kiambishi tamati chake kwa ajili ya usawazisho wa matamshi kama katika mfano (53)

- 53)            i)      hu-u  
                 ii)     ha-wa  
                 iii)    hi-ki

Moravcsik (1978:331) anasema kuwa, kuna uwezekano kuwa katika baadhi ya lugha za ulimwengu, upatanisho au usawazisho wa matamshi unaangaliwa kwa misingi ya sifa kiarudhi ilhali katika lugha nyingine misingi ya ugawanyaji kivipande hutumiwa kama katika ruwaza ya mkazo katika upatanisho.<sup>14</sup>

### **3.5.2 VIONYESHI VYA UJIRANI WA MBALI**

Vivumishi vya kuonyesha mbali huundwa kwa kuongeza viambishi ngeli kwenye shina la mofimu 'le-' kama tuonavyo katika jedwali (v)

*Jedwali (v)*

NGELI	SHINA LA VIONYESHI VYA MBALI: UMOJA NA WINGI	VIAMBISHI - NGELI: UMOJA NA WINGI	MANENO MAZIMA
1	1 -le 2 -le	1 yu- 2 wa-	yule wale
2	3 -le 4 -le	3 u- 4 i-	ule ile
3	5 -le 6 -le	5 li- 6 ya-	lile yale
4	7 -le 8 -le	7 ki- 8 vi-	kile vile
5	9 -le 10 -le	9 i- 10 zi-	ile zile
6	3a -le 10a -le	3a u - 10a zi-	ule zile
7	3b -le 6a -le	3b u- 6a ya-	ule yale
8	11 -le 12 -le	11 ku- 12 pa-	kule pale
9	13 -le 14 -le	13 m- 14 ku-	mle kule

Kwa kawaida, vivumishi vionyeshi huwekwa baada ya jina mwa tuonavyo katika mfano (54)

- 54)            i)     Mti u-le  
                 ii)    Kitabu ki-le  
                 iii)   Mtoto yu-le

- iv) Nyumba i-le .
- v) Jiwe li-le .
- vi) Mahali m-le .

Hata hivyo, utawasikia watu wakisema sentensi (54) hapo juu kama ifuatavyo katika sentensi (55)

- 55) i) U-le mti .
- ii) Ki-le kitabu .
- iii) Yu-le mtoto .
- iv) I-le nyumba .
- v) Li-le jiwe .
- vi) M-le mahali .

### 3.6 KISHAZI REJESHI

Wanaisimu wanatumia istilahi ‘kishazi rejeshi’ kama kwamba inaelezea au kuwakilisha dhana ya sarufi bia.<sup>15</sup> Katika uundaji wa kishazi rejeshi, kiambishiawali rejeshi, ambacho pia kinabeba urejeshaji wa faridipeke, kinaunganishwa kwa kitenzi. Umbo la kiambishiawali rejeshi, unatawaliwa na ngeli ya nomino ambayo inahusika nayo. Kwa maneno mengine, kiambishiawali cha urejeshaji wa upatanisho sharti ulingane na kiambishiawali cha kiwakilishi. Crystal (1987:95) anaorodhesha vipengele mbalimbali vinavyounda kishazi kama kiima, shamirisho, yambwa na kielezi.<sup>16</sup>

### 3.7 AMBA-

Katika usemi, kirejeshi 'amba' hutumika kama kiwakilishi kirejeshi. Matumizi ya amba-ni ya namna nyingi katika lugha ya Kiswahili. Tuone tofauti kati ya sentensi hizi mbili katika mfano (56) hapa chini

- (56)           i)       Viti ambavyo vimevunjika .  
                  ii)       Viti vilivyovunjika .

Katika (56) (i) tunataka kuvibainisha viti vilivyovunjika. Katika (56) (ii) kirejeshi amba-hakijatumika na maana iliyo katika (56) (i) ya kuvibainisha viti vilivyovunjika ingalipo katika (56) (ii). Tofauti hiyo kati ya (56) (i) na (ii) ni ya kisarufi. Neno 'vimevunjika' ni kitenzi halisi na 'vilivyovunjika' sicho kitenzi halisi. Tukisema kama ilivyo (56) (i) neno 'ambavyo' limetumika pamoja na kitenzi 'vimevunjika' kusudi kukirejesha kitenzi halisi hicho kwenye kiima'viti'. Hata hivyo, tukisema 'viti vilivyovunjika' hiyo '-vyo' iliyoungwa kwenye 'vunjika' inafanya kitenzi hicho kisione kama kitenzi halisi.

Matumizi ya 'amba-' pamoja na majina ya ngeli mbalimali huonekana kama ilivyo kwenye jedwali (iv) hapa chini

#### ***Jedwali (iv)***

<b>MZIZI WA KIWAKILISHI KIREJESHI “amba”</b>	<b>-O REJESHI ILIYOAMBATISHWA KADIRI YA NGELI</b>	<b>AMBA ILIYOUNGANISHWA A KWENYE VIAMBISHI</b>
amba-	-ye	amba-ye
amba-	-o	amba-o
amba-	-o	amba-o
amba-	-cho	amba-cho
amba-	-vyo	amba-vyo
amba-	-lo	amba-lo
amba-	-yo	amba-yo
amba-	-o	amba-o
amba-	-yo	amba-yo
amba-	-ko	amba-ko
amba-	-po	amba-po
amba-	-mo	amba-mo

Tuangalia mifano ya upatanisho wa kisarufi baina ya viwakilishi virejeshi na nomino katika mfano (57)

- 57)
- i) Mkulima ambaye amelima ni mzuri
  - ii) Kitu ambacho ni chema kitajiiza
  - iii) Sanduku ambalo limenunuliwa ni zuri
  - iv) Maoni ambayo yametapakaa ni mabaya
  - n) Mji ambamo naishi mna watu wengi

### 3.8 -O REJESHI

-O rejeshi ni kiangama kinachotumika katika semi ili kurejesha mawazo yanayohusu jambo ambalo tayari limetajwa au jambo ambalo linajulikana. -O rejeshi hupatikana katika sentensi zenye viunganishi ambavyo vinatokana na neno 'kwa' vikiwa vinarejelea kwa jina lililotajwa katika vionyeshi vya ujirani wa karibu au vikiwa na vivumishi au viwakilishi na katika kirejeshi 'amba-' kama tulivyoona katika jedwali (vi) sehemu ya 3.7. -O rejeshi hutumika daima katika muunganisho wa viambishi ngeli. Muundo wake katika safu ya tatu (Jedwali vii) umejadiliwa kwa urefu kuzidi safu ya pili (Jedwali v) Kama tunavyoona.



*Jedwali (vii)*

<b>VIAMBISHI NGELI REJESHI</b>	<b>-O REJESHI</b>	<b>-O REJESHI PAMOJA NA VIAMBISHI NGELI</b>	<b>VIONYESHI VYA UJIRANI WA KARIBU VYENYE -O REJESHI</b>	<b>KIHUSISHI “KWA” CHENYE O-REJESHI</b>
Yu-a	-o	-ye	hu-yo	kwa-yo
W-a	-o	-o	ha-o	kwa-o
u-	-o	-o	hu-o	kwa-o
i-	-o	-yo	hi-yo	kwa-yo
ki-	-o	-cho	hi-cho	kwa-cho
vi-	-o	-vyo	hi-vyo	kwa-vyo
li-	-o	-lo	hi-lo	kwa-lo
ya-	-o	-yo	hi-yo	kwa-yo
u-	-o	-o	hu-o	kwa-o
ya-	-o	-yo	ha-yo	kwa-yo
i-	-o	-yo	ha-yo	kwa-yo
zi-	-o	-zo	hi-zo	kwa-zo
u-	-o	-o	hi-zo	kwa-zo
zi-	-o	-zo	hi-zo	kwa-zo
pa-	-o	-po	ha-po	kwa-zo
mu-	-o	-mo	hu-mo	----
ku-	-o	-ko	hu-ko	----
ku-	-o	-ko	hu-ko	----

Tuangle mifano ya sentensi za kuhusisha -O rejeshi katika mfano (58)

- (58)
- i) Mtoto alia-ye amechapwa .
  - ii) Mmea uchipuka-o umekauka .
  - iii) Kiti kisimama-cho kitauzwa .
  - iv) Nguo ipasuka-yo itashonwa .

Muunganisho wa -O rejeshi kwenye vitenzi ni wa namna mbili. Namna ya kwanza, muunganisho wa -O rejeshi kwenye kitenzi huwa kwa kuambatisha -O rejeshi yenye viambishi-ngeli, mwishoni mwa kitenzi kama katika mfano (59)

- (59)
- i) Ua linukialo limeuzwa .
  - ii) Kitabu kitumikacho shuleni ni kizuri .

Muunganisho wa aina hiyo hutakiwa ikiwa katika kitenzi mofimu za wakati hazikuwakilishwa kama ilivyo katika mfano (60)

- (60)
- i) Mtoto aliaye amechapwa .
  - ii) Mti uangukao umeoza .
  - iii) Tunda linukialo limeoza .
  - iv) Mavazi yappendayo yameuzwa .

Muunganisho wa namna ya pili wa -O rejeshi kwenye kitenzi huwa kwa kuweka viambishi vya -O rejeshi baada ya mofimu za wakati, kama ilivyo katika jedwali(viii)

*Jedwali (viii)*

<b>VIAMBISHI KATI VYA -O REJESHI KADIRI YA NGELI</b>	<b>KITENZI</b>	<b>MUUNGANISHO WA -O REJESHI KWENYE KITENZI</b>
-ye-	anapenda	ana-ye-penda
-o-	wanapenda	wana-o-penda
-o-	utaanguka	utaka-o-anguka
-yo-	itachanua	itaka-yo-chanua
-cho-	kitakata	kitaka-cho-kata
-vyo-	vimenolewa	vili-vyo-nolewa
-yo-	yatawekwa	yataka-yo-wekwa
-lo-	lilianguka	lili-lo-anguka
-yo-	imechakaa	zitaka-zo-chakaa
-zo-	zitaoshwa	zitaka-zo-oshwa
-o-	utachomwa	utaka-o-chomwa
-zo-	zitaanguka	zitaka-zo-anguka
-po-	panabomoka	pana-po-bomoka
-ko-	tunakwenda	tuna-ko-kwenda
-mo-	mnanuka	mna-mo-nuka
-ko-	tunasoma	tuna-ko-soma
-o-	unaenea	una-o-enea
-yo-	yanaenea	yana-yo-enea

Katika vitenzi vya mtindo wa kukana, viambishi vya -O rejeshi huambatishwa

katika vitenzi vya wakati uliopo. Kuhusu vitenzi vya mtindo wa kukana katika wakati ujao na wakati uliopita, -O rejeshi huambatishwa kwenye kiwakilishi kibainishi 'amba-' kama tulivyokwishaeleza, kwenye kurasa zilizotangulia. Brandon (1976) anasema kuwa katika lugha ya Kiswahili, hakuna tofauti ya kimaana itakayoonekana katika kupuuza -O rejeshi kama kiambata cha vitenzi vya wakati uliopo. Brandon (Ibid) anasema kuwa ukanushaji huwa katika kitenzi<sup>17</sup> wala hakuna ukanushaji katika viwakilishi.

### 3.9 VIWAKILISHI

Kamusi sanifu ya isimu na lugha inaeleza viwakilishi kama, ' maneno yatumikayo badala ya nomino."<sup>18</sup> Kapinga(1983: 92) anafafanua viwakilishi kama maneno yoyote yanayosimama badala ya majina ili kujulisha kitu kinachohusika na maonyesho, ulizo au kitenzi kinachoarifu tukio fulani ambapo jina la kitu chenyewe halitajwi.<sup>19</sup>

Maoni kama hayo vilevile yanatolewa na Lehmann (1978) ambaye anasema viwakilishi ni vibadala vya nomino,<sup>20</sup> na Jespersen (1924) anayesema viwakilishi husimama badala ya jina la mtu au kitu .<sup>21</sup>

Hata hivyo, ubadilishanaji wa namna hiyo au uwakilishi kibadala unaweza tu kufanyika pale ambapo nomino inayobadilishana nayo hiyo nafasi inadhihirika wazi. Pia, viwakilishi vya Kiswahili ni maneno ambayo yanaweza yakatumika

badala ya nomino kutaja mtu au kitu ambacho tayari kimetambulika.

### 3.9.1 VIWAKILISHI NAFSI

Katika Kiswahili kuna aina tatu za viwakilishi nafsi.<sup>22</sup> Ashton (1947) anavieleza kama viambishiawali vya kiima, viambishiawali vya yambwa na viwakilishi huru.

Rosenbaum na Jacobs (1968)<sup>23</sup> wanashikilia kuwa viwakilishi nafsi hasa hurejelea sifa ya binadamu. Viwakilishi nafsi kawaida vinatumika katika kundi la 1/2 kama katika mfano (61)

- (61)
- Mimi
  - Wewe
  - Yeye
  - Sisi
  - Ninyi
  - Wao

Tazama kiwakilishi nafsi cha tatu hakionyeshi uana wa wanaorejelewa. Hili linaachwa kueleweka katika muktadha na wale wanaozungumza. Tunaweza kutumia mfano (62)

- (62)
- i) Juma anacheza .
  - ii) Anacheza .

Katika (62)ii kiwakilishi kinafanya kazi katika kishazi kama neno kuu. Kiambishi awali -a- kinarejelea nafsi ya Juma. Tofauti na kategoria nyingine, viwakilishi nafsi huru ama vinaweza au visiweze kuwa na kiambishiawali sawa kama kile cha nomino kinachowakilisha kama tuonavyo katika mfano (63) hapa chini.

- (63)
- i) Yeye ni mzuri .
  - ii) Wao ni wazuri .
  - iii) Mimi ni mzuri .
  - iv) Hicho ni kizuri .
  - v) Hiyo ni mzuri .

Viwakilishi jumla na viwakilishi jirejee<sup>24</sup> huchukua viambishiawali kama vya ngeli ya majina yanayowakilishwa kama ilivyo katika mfano (64) hapa chini.

- (64)
- i) Mtu yeyote .
  - ii) Kiti chochote .
  - iii) Mtu mwenyewe .
  - iv) Kitu chenyewe .
  - v) Nyumba yenyewe .

Inawezekana kuwa na nomino na kiwakilishi jirejee katika kirai kimoja au kishazi hasa kwa minajili ya kusisitiza kama ilivyo katika mfano (65)

(65) Juma mwenyewe alikuja. Viwakilishi nafsi sharti vitumike tu kama kiambishiawali cha kiima au kiambishikati cha yambwa lakini sio kama kidadala cha hivi. Hatukuingilia mjadala wa iwapo viambishikati vipo katika Kiswahili ama la. Lakini katika kusisitiza utumikaji wa kiambishindani, kiambishi kinachochopekwa ndani ya mzizi wa neno, tulimnukuu Whiteley (1968) anayesema:

Katika maumbo yasiyo na urejeshaji, kiambishindani huwekwa tu pale msisitizo unaelekezwa kwenye yambwa.<sup>25</sup>

(Tafsiri ni yetu)

Kuna wakati ambapo kiwakilishi cha nafsi hudondoshwa katika hali iliyopo kama inavyoonekana katika mfano (66).

- (66)
- i) Mimi ninaenda shuleni .
  - ii) Ninaenda shuleni .

### **3.9.2 VIWAKILISHI NAFSI-HURU**

Hivi viwakilishi vinaweza vikasimama vyenyewe katika sentensi au kirai kama ilivyo katika mfano (67)

(67) i) Nani huyo?

Mimi

ii) Nani huyo?

Mimi, Juma

Mfano (67) ii umefafanuliwa ingawa (i) ndio hutumika zaidi. Mara nyingi hufanyika kuwa kiunganishi 'na' hutumika katika lugha ya Kiswahili. Katika hali kama hii, watu husema kama katika mfano (68)

(68) i) na mimi

ii) na wewe

iii) na yeye

iv) na wao

Hata hivyo, misinyao ifuatayo inatumika badala ya maumbo hayo ya (68) kama tuonavyo katika mfano (69) hapa chini

(69) i) nami

ii) nawe

iii) naye

iv) nao

Kwa kweli misinyao ya aina hiyo inatumika kila mara kiasi kwamba anayejifunza lugha hii hatapata kujua umbo la asili ya mifano ya (68).



Katika sura hii, tumeona aina ya maneno (soma vivumishi) yanayotoa habari, kueleza habari ya mtu namna alivyo au kitu jinsi kilivyo, jinsi kinavyoonekana au jinsi kinavyofikiriwa kwamba kina tabia fulani au kipo katika idadi fulani.

Katika KN cha Kiswahili, vivumishi vyote vilivyotajwa katika sehemu hii vilihusika na kila mara vilirejelewa. Msingi huu tuliouweka ni imara na ulihibitajika kabla ya kujadili sura ya nne.

# TANBIHI

1. Hartmann, R na F.Stork (1973) Dictionary of language and linguistics Applied Science Publishers Ltd. London uk.155
2. Mdee, J (1968) Kiswahili: Muundo na Matumizi yake. Intercontinental publishers Ltd. Nairobi uk 5
3. Lehmann, W(1978) Syntactic Typology. The Harvester Press Sussex uk.201
4. Kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990) Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) Dar-es-Salaam uk 2
5. Maw,J (1969) Sentences in Swahili: A study of their internal relations. Luzac and Co. Ltd London uk 75
6. Kapinga, M (1983) Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu. TUKI, Dar-es-Salaam uk 71
7. Kipeo ni kipimo cha ulinganisho wa hali ya kuzidiana.
8. Kiwango linganishi ni hali au umbo la kipashio ambalo hutumika kama kipimo cha kulinganishia.
9. Umbo la neno ambalo huonyesha uzaidi wa juu kabisa wa hali linapolinganishwa katika daraja tatu za upishano.
10. Jespersen,O (1924) The Philosophy of Grammar. George Allen and Unwin Ltd, London uk.202
11. Kama 4 uk.47
12. Kama 6 uk.87
13. Kama 1 uk.61
14. Moravcsik, E (1978) 'Agreement' Katika Greenberg, J (mhr) Universals of Human Language Stanford University press, California uk.333.
15. Downing, B (1978) 'Some Universals of Relative Clause Structure' Katika Greenberg,J (mhr) Universal of Human Language. Stanford University Press, California uk 37.
16. Crystal, D (1987) The Cambridge Encyclopaedia of language. Cambridge University Press. Canbridge uk.95

17. Brandon, F (1976) "Quantification, Negation and the Semantic isolation of sentence' Katika Moravcsik, E (hr) Working papers on language Universals vol.20. Stanford University press, California uk.30
18. Kama 4 uk. 49
19. Kama 6 uk.92
20. Kama 3
21. Kama 10 uk.82
22. Ashton, E (1947) Swahili Grammar, including intonation, London uk.42
23. Rosenbaum, P na R.Jacobs (1968) English Transformational Grammar. Ginn and Co. ltd. London uk. 92
24. Kiwakilishi jirejee ni kiwakilishi ambacho hurejea kwenye kiima, K.m. mimi nilijipiga mwenyewe.
25. Whiteley, W(1968) Some Problems of Transitivity in Swahili. Luzac and Co.ltd London uk.9

## 4.0

## SURA YA NNE

### 4.0.0

### MTAZAMO WA SINTAKSIA YA 'X-BAR'

Tumeangalia vipashio vinavyopatikana katika KN cha Kiswahili katika sura ya tatu. Katika faslu hii, lengo letu kubwa hususan lilikuwa kufanya uchanganuzi wa nadharia ya sintaksia ya X-bar pale inapotumika katika KN cha Kiswahili. Takriban, tulipiga msasa sintaksia ya muundo virai kama msingi wetu wa kueleza kwa tafsili nadharia ya X-bar. Tuliadini kuwa kuingizwa kwa sura hii ya uchanganuzi wa KN kutaleta ufahamu wa ndani wa sifa za kisintaksia ambazo zinaunda KN. Hii hasa ni kutokana na sababu kwamba, kwa kutumia michoro ya miti kukivunja kile KN katika vitengo mbalimbali, kama ilivyofanywa katika kaida zilizopo hapa, kulisaidia kutoa picha kamili ya KN cha Kiswahili. Hili baadaye lilisaidia katika kuwezesha ufahamu wetu kuhusu KN kurahisishwa.


### 4.1 KIUNZI CHA MUUNDO VIRAI

Kiunzi cha muundo virai ni sarufi inayozipa umuhimu wa pekee kanuni zinazozalisha vijenzi mbalimbali pamoja na uchambuzi wa viambajengo vya tungo.<sup>1</sup> Sarufi ambayo imejengeka katika kiunzi cha muundo virai hubeba kanuni, kila kanuni ikiwa na alama moja upande wa kushoto ikiunganishwa na alama moja au zaidi upande wa kulia.

Sintaksia muundo virai inadai kwamba sentensi ina muundo wa viambajengo vya

madaraja ambazo zinaweza kuwakilishwa kwa kielelezo tungo.<sup>2</sup> Kielelezo tungo hiki<sup>3</sup> kinabeba vifundo, ambapo kila kifundo kinabeba alama, alama ambayo ni kiwakilishi cha neno. Kila jozi la vifundo vinahusiana kwa kutumia uhusiano wa umilikaji na utangulizi kama katika mfano (1)

(1)




Kifundo -KN kinajitokeza kushoto mwa kifundo-KT, na hivyo, KN hakimiliki KT bali kinakitangulia. Kifundo-S kinamiliki kifundo -KN na kifundo -KT kwa vile kinajitokeza juu ya kielelezo tungo kuzidi KN na KT. Vile vile, KN kinamiliki N na KIO, nayo KT kinamiliki T na E lakini vifundo KN, KT, N, KIO, E, na T vinamilikiwa na kifundo-S.

Kifundo-S kinaunganishwa na kifundo-KN na kifundo -KT kwa kutumia mistari (matawi) yasiyogawanyika, kila tawi likifikia kila mojawapo ya vifundo viwili. Sisi tulishughulikia kifundo -KN ambapo yale maelezo tuliyotoa hapo juu yalizingatiwa kwani KN wakati mwingine huwa na viambajengo vyake na

vifundo vyake vinavyoonyesha hivi viambajengo na vinaweza vikaonyeshwa kama katika mfano(2)

(2)



Kufuatia kile tulichokisema katika mfano (1) tunaona hapa kuwa kifundo -KN kinamiliki kifundo -N na kifundo-KIV.O na kwamba kifundo-N kinatangulia kifundo -KIV.O. Kwa mintarafu hii, kifundo-N na kifundo -KIV.O pamoja vinaunda kiambajengo kinachojulikana kama 'kikundi Nomino'. KN ni kategoria kirai. Kategoria nyingine katika muundo huu ni ule unaowakilishwa na kifundo-N na kifundo-KIV.O . Kategoria hii inajulikana kama kategoria leksika kwa jinsi ambavyo imebeba neno au leksika pekee.

Kategoria kirai na kategoria leksika ni kategoria mbili tofauti kwa sababu kategoria kirai inaelezwa kuhusiana na jinsi inavyojitokeza kama kiambajengo cha sentensi ilhali kategoria leksika inaelezwa kuhusiana na namna ambavyo inavyojitokeza kama msamiati.

Vielelezo tungo vinazalishwa kwa kutumia kanuni mbalimbali zikiwemo kanuni muundo virai.<sup>4</sup> Pia kuna kanuni za msamiati na kanuni ya kuchopeka msamiati unaohitajika. Katika mkabala wa Chomsky (1957) kule kubadilika kutoka kwa uchanganyuzi mmoja wa sentensi kunafanywa kwa kanuni ambazo 'zitazalisha' vielelezo tungo<sup>5</sup> kama tulivyoona katika mfano (1) na (2)

Vielelezo tungo hivyo vinaelezea namna ambavyo kirai au kishazi kinaundwa kutokana na viambajengo. Kila mojawapo ya hivi viambajengo vinagawanywa katika kategoria inayofaa.

Katika Radford (1981:91) na hata wanaisimu wengine, wa Sarufi Zalishi Geuzamaumbo, sintaksia ya muundo virai, ina kategoria mbili ambazo zinatambuliwa: kategoria leksika na kategoria virai.<sup>6</sup> Kategoria leksika ni kategoria yenye maneno kama vile N,T KIH,E, KIV, KBN na kadhalika. Kategoria leksika ni kama vile KN, KT, KKIV, KE na kadhalika.

Hakuna mipaka kuhusu idadi ya elementi ambayo kila seti huenda ikabeba, inaweza ikawa elementi moja au kundi la elementi kama tuonavyo katika mfano(3) hapa chini

- 3 i) Wavulana ni wazuri .
- ii) Wavulana wanene ni wazuri .
- iii) Wavulana wanene warefu ni wazuri .

Kulingana na SMV, maelezo yaliyopigwa mstari kama (3) hapo juu yanachukuliwa yote kama KN. Hii ni kwa sababu yote yanapatikana katika nafasi sawa katika kiwango cha kirai kama vile wavulana na hivyo basi yana nafasi sawa kisintaksia.

Awali katika sehemu hii, tuligusia kuwa kirai au kishazi huwa kinazalishwa katika kielelezo tungo kwa kutumia kanuni mahususi za kanuni muundo virai(KMV).

Kabla hatujarejelea sintaksia ya X-bar, tulionelea ni bora kwa muhtasari tuangalie muundo wa KN sahili kwa mjuibu wa SMV.

#### **4.1.1. MUUNDO WA KN SAHILI**

Tunachukulia kuwa KMV sahili ya KN cha Kiswahili zinawakilishwa kama ifuatavyo:

a {N}

b {N (KIV)}

c {N (K.Kiv)}

KN ---> d {N (K.Kih)}

e {N (Kbn)}

f {Kiw}


Katika sehemu hii ya sura hii, tumechanganua ruwaza ya muundo wa KN cha



Kiswahili. Kwa mujibu wa KMV ya KN sahili cha Kiswahili, elementi moja pekee ambayo ni ya lazima ni nomino.<sup>7</sup> Wakati mmoja tu ambapo nomino huchopolewa kutoka muundo wa KN ni pale ambapo mahala pake panakaliwa na kiwakilishi.

4.1.2      KN → N

Mojawapo ya KN sahili katika Kiswahili kinabeba nomino moja pekee. Katika hali hii, kifundo cha KN kinatawaliwa na neno moja tu. Nomino hizo huashiria majina ya watu, mahali na majina ya kawaida.<sup>8</sup> Kwa mchoro muundo huu utawakilishwa kama katika mfano(4)



4.1.3      KN → KW

Nyakati nyingine, kifundo cha KN kinawakilishwa na kiwakilishi. Viwakilishi ambavyo aghalabu huonekana katika vifundo vya KN katika Kiswahili ni


viwakilishi-nafsi. Ili kutoa habari za matukio ya matendo, nafsi hutajwa ama kwa jina lake ama kwa kiwakilishi chake. Kuna namna mbili za viwakilishi nafsi.<sup>9</sup> Namna ya kwanza ni ya viwakilishi-Nafsi huru ambavyo ni vya maneno moja moja yanayosimama peke yake. Namna ya pili ni ya viwakilishi nafsi viambata yaani mofimu zinazoambatanishwa kwenye fungutenzi kwa ajili ya kujulisha kiima. Viwakilishi huru katika nafsi ya kwanza, pili na tatu zinaonyeshwa katika jedwali (1) hapa chini:

*Jedwali (1)*

NAFSI	UMOJA	WINGI
1	mimi	sisi
2	wewe	ninyi
3	yeye	wao

Viwakilishi nafsi hivyo hapo juu haviambatishwi kwenye fungutenzi ndipo vikaitwa viwakilishi-nafsi huru. Viwakilishi hivyo ni maneno mazima yenye maana kamili. Viwakilishi hivi sita vinaweza vikaonyeshwa katika mfano (5)


(5)



4.1.4 KN → N (KIV)

Aina nyingine ya KN sahili ni kile KN kinachobeba nomino na kivumishi angama, neno lililomo katika KN na ambalo lina uamilifu wa kuvumisha. Jambo muhimu kuhusu uhusiano kati ya nomino na kivumishi chake ni kwamba kiambishi kitangulizi cha nomino kinalazimishwa kufuatishwa kama kiambishi cha kivumishi. Ruwaza ya muundo wa aina hii ya KN inawakilishwa katika mfano (6)

(6)




Vilevile, nomino hujitokeza na vivumishi vingine vya idadi kama vile wengi.

4.1.5 N → N(KKIV)

Katika Kiswahili, KN kinaweza kikawa na nomino ikifuatwa na K.KIV. K.KIV. ni kiambajengo ambacho neno kuu ni kivumishi kinachomiliki vivumishi vingine

vinavyokifuata<sup>10</sup>. Ruwaza ya muundo wa aina hii ni kama katika mfano (7)

7)



Sio lengo letu kuchanganua muundo wa KN kwa kutumia SMV, ila tilitumia mifano michache ya nadharia hii ili tupate msingi thabiti ya ile faslu inayochanganua KN cha Kiswahili kwa mtazamo wa sintaksia ya X-Bar.

## 4.2 KAIDA YA X-BAR

Katika sura ya kwanza, tulitangulizwa na dai la wanasintaksia ya X-bar kwamba kaida ya SMV 'ilijisonga mno kwa idadi ya aina za kategoria inayoruhusu' (Radford 1981:91) na kwamba kilichohitajika kilikuwa upanuzi wa kiufafanuzi wa nadharia hii. Kwa maneno mengine, kiunzi cha SMV kilionekana kama kisichoweza kujitosheleza kamwe kwa sababu kulikuwa na mambo fulani fulani kuhusu muundo wa kategoria za virai ambayo haikuweza kufafanua.

Jambo hili lilifanya SMV kushindwa kudhihirisha wazi uhusiano unaosababisha dhana ya 'kichwa cha kirai'. Dhana hii ni muhimu kwa sababu inaonyesha kuwa nomino kuu huwa na sifa zinazofanana ya kifundo-kirai kinachobeba kama katika mfano (8)

8) Watoto hawa wafupi

Tunaona kuwa kwa vile neno kuu 'Watoto' liko katika wingi, kirai chote vile vile kiko katika wingi. Kwa maneno mengine, kwa vile  $N^0$  ni wingi,  $\bar{N}$  vilevile ni wingi. Mfumo wa SMV haudhihirishi wazi mishabaha hii. Riemsdijk na Williams (1986) wanasema:

Njia inayotumiwa kuelezea 'kichwa cha kirai' sharti ihakikishe mwanzoni kwamba nomino ya wingi inayotangulia katika sentensi inaathiri nomino au neno la mwisho katika sentensi hiyo ambalo pia litaashiria wingi.<sup>11</sup>  
(Tafsiri ni yetu)

Ilionekana kuwa ni jambo muhimu njia kama hiyo iweke bayana mijumuisho inayohusu kategoria zinazotangulia na kufuata nomino kuu katika kirai.

Waasisi wa nadharia ya X-bar walipata kuwa njia hiyo (SMV) haibebi wala haikubali kategoria zaidi ya mbili. SMV ilibeba kategoria mbili: Kategoria kirai na kategoria leksika. Walishikilia kuwa iliwezekana, kwa kutumia ithibati za kijarabati, kuonyesha kwamba kunapatikana kategoria za katikati, kati ya

kategoria kirai na kategoria leksika, jambo ambalo mfumo wa SMV hauruhusu.

Kwa hivyo, hoja ilikuwa ni kwamba, kwa vile kunapatikana kategoria za katikati, kati ya, tuseme nomino na KN, kamwe hakukuwa na haja kwa nini kiambajengo cha nomino chochote kiwe tu ama nomino (kategoria leksika) au KN (kategoria kirai).

Nadharia ya X-bar ilitangulizwa katika Chomsky (1970) na linashughulikia jaribio la awali kabisa la kupata suluhisho la tatizo la SMV <sup>12</sup>. Ufafanuzi na kazi nyingine katika juhudi za kuimarisha SMV zilikuwa za Emonds (1976), na vilevile Jackendoff (1974, 1976, 1977).

Katika ufafanuzi wetu, tunaegemea maelezo ya Radford (1981). Hata hivyo, tungependa kwa muhtasari tu kutoa maelezo ya Jackendoff(1977) na Hornstein na Lightfoot (1981) ili tunapoeleza X-bar kwa misingi ya Radford (ibid), tunaona kuwa tofauti kubwa haipo.


Kwa mujibu wa Jackendoff (ibid), wazo kuu katika nadharia ya X-bar ni kwamba KMV zinazobainisha muundo wa kirai na nomino kuu, iwe kitenzi, nomino, kivumishi au kihusishi zinaweza zikaelezwa hivi:<sup>13</sup>

$$(i) \quad i \longrightarrow \dots X^{i-1} \dots$$

Hapa X ni neno nyambuliki linaloweza kuwa N, KT, KIV na KIH. Vilevile i na i-1 zinawakilisha idadi ya 'bar'. Jackendoff (Ibid) anatumia mpangilio wa  $X^{111}$  Kumaanisha  $X^3$  au 'X-bar tatu',  $X^{11}$  kumaanisha  $X^2$  au 'X-bar mbili',  $X^1$  au 'X-bar moja' na  $X^0$  (X) kwa maana ya 'X bila bar' ambapo maelezo ya

(i)  $X^1 \longrightarrow \dots X^{i-1} \dots$

yanajitokeza katika mchoro wa mfano (9)



$X^0$  huashiria neno kuu. Chochote ambacho kinamilikiwa na  $X^1$  ila tu  $X^0$  kinaitwa kijalizo cha  $X^0$  na chochote kinachomilikiwa na  $X$  ila tu  $X^0$  ni Kibainishi<sup>14</sup> cha  $X^1$ .

Awali, katika sarufi mapokeo<sup>15</sup>, jambo ambalo liliwahusu mno wanaisimu lilikuwa muundo wa neno. Sarufi mapokeo haikuweza kuonyesha uhusiano unaojengeka kati ya vipengele hivi katika muundo wa kisintaksia wa mfumo huo. Maoni kama haya yanapatikana katika maelezo ya Koziol (1937), Kruisinga (1931), Sweet (1900), Poutsma (1928) na Zandvoort (1948).<sup>16</sup>


Jambo muhimu wanalosisitiza Hornstein na Lightfoot (ibid) katika uchanganuzi wao ni kwamba K.KIV kinaweza kutumika ipasavyo kuvumisha N au 'N-bar' ingawa kunazuka tatizo la kimuundo. Katika hali kama hiyo, kirai kihusishi ambacho kinachanganuliwa kama 'Kih-bar mbili' katika kiunzi chao) kinaweza kuvumisha N au 'N-bar'. Wanadai kuwa virai kama vile katika mfano (10)

- (10) i) Yule mwanafunzi mwenye nywele ndefu .  
ii) Yule mwanafunzi wa isimu .


vina miundo tofauti kama tuonavyo katika mfano (11) na (12)



(11)



(12)



Wanadai kuwa tofauti hizi vilevile zinatoa habari kuhusu semantiki ya sentensi hizi. Wanasema:

Tunachukulia pia kwamba muundo wa kiambajengo kisintaksia

utatekeleza jukumu la kueleza semantiki ya vikundi nomino, hivi kwamba  $\bar{N}$  inabainisha sifa ya kisemantiki. Kwa sababu hii, kuhusisha (12) na Yohana ni kuhusisha sifa moja kwake, kwamba anasoma isimu; kuhusisha (11) na Yohana ni kuashiria sifa mbili, kwamba anasoma na ana nywele ndefu. Kwa mintarafu hii, Yohana ni mwanafunzi wa isimu, kuonyesha kwamba kile anachokifanya hakiwezi kuonyeshwa katika (11); kinyume, Yohana ni mwanafunzi mwenye nywele ndefu, haiwezi kuwa na muundo kama (12)<sup>17</sup>

(Hornstein na Lightfoot, Introduction to Explanation in Linguistics (1981)


(Tafsiri ni yetu)

Tuliweza kuchunguza dai la Hornstein na Lightfoot (Ibid). Ikiwa wa isimu inavumisha N, ambapo mwenye nywele ndefu inavumisha 'N-bar', basi iwapo N imo kwenye 'N-bar', tunatarajia kwamba ikiwa virai viwili vyote vitatumika kuashiria maana ile ile, basi kijalizo -N cha wa isimu kitaingizwa ndani ya shamirisho -N mwenye nywele ndefu: kwa maneno mengine, tunatarajia ruwaza ya 13 hapa chini:


13) i) Yule mwanafunzi wa isimu mwenye nywele ndefu .

ii) \*Yule mwanafunzi mwenye nywele ndefu wa isimu .

Ili kuonyesha kwa nini (13 (b) 'haitawezekana' zingatia miundo miwili ya virai katika (13)



(13) (ii)



Ni dhahiri kwamba (13) (ii) inakiuka sheria ile ya 'matawi kutopaswa kupitishana'. Radford (1981:83) asema:

Ikiwa kifundo x kinamiliki vifundo viwili vya y na z na ikiwa inatangulia z, basi kifundo chochote kinachomilikiwa na y sharti kitangulie z na kifundo kingine kile kinachomilikiwa na z.

(Tafsiri ni yetu)

Kwa mujibu wa Radford (ibid), neno kuu katika kirai chochote kinajulikana kama  $X^0$  na kategoria kirai inayobeba  $X^0$  inajulikana kama  $\bar{X}$  au  $X^1$  au 'X-bar -moja' na kategoria inayobeba  $\bar{X}$  ni  $\bar{\bar{X}}$  au  $X^2$  au 'X - bar- mbili', na kategoria ya kirai inayobeba  $\bar{\bar{X}}$  ni  $\bar{\bar{\bar{X}}}$  au  $X^3$  au 'X-bar-tatu' na kadhalika. Tuliweza kueleza haya katika sura ya kwanza ambako tulijitokeza na KMV iliyo katika mfano (77) wa Radford (1981: 103)

- i)  $\bar{X}$  .....  $\bar{X}$  .....
- ii)  $\bar{X}$  .....  $\bar{X}$  .....
- iii)  $\bar{X}$  .....  $\bar{X}$  .....

Kanuni hiyo baadaye inajumulishwa na kuwa,


$$X^n \longrightarrow \dots X^{n-1} \dots$$

Hata hivyo, kwa sababu ya kuweza kuzuka kwa uchamko<sup>18</sup> na pia hali ya uunganishaji,  $X^n \longrightarrow X^{n-1} \dots$  ulibadilishwa na kuwa  $X^n \longrightarrow X^m \dots$  ambayo inairuhusu 'm' kuwa katika kiwango sawa na 'n' au 'n-i' Mfano (14) ni mfano unaonyesha uchamko.

14) Yule mtoto mrefu mweusi mgeni.


Uchamko wa aina hii inajitokeza katika sintaksia ya X-bar kama katika mfano 15

(15)



Tunaweza tukawa na sentensi ndefu zaidi yenye uchamko, kama katika mfano (16) na ukawa na muundo (17) hapa chini. (16) Yule mtoto mrefu mjinga mweusi mgeni.

(17)




Hata ile kanuni ya  $X^n \dots \rightarrow X^m \dots$  huenda bado haijitoshelezi na kwa kweli ni rahisi sana kupata baadhi ya kanuni ambazo zinakiuka kanuni hiyo hapo juu, mfano ni uchanganuzi alioufanya Chomsky (1977) kuhusu TOP (topic) na COMP (complementiser) kama viambajengo katika 'On wh-movement' (uk.91) ambapo Chomsky alipendekeza sheria ya;

- i)  $\bar{S} \dots \rightarrow \text{TOP} \dots \bar{S}$
- ii)  $\bar{S} \dots \rightarrow \text{COMP} \dots \bar{S}$

Mfano mwingine ambapo kanuni ya  $X^n \rightarrow X^{n-1}$  huenda isijitosheleze ni kuhusu uunganishaji. Kwa ujumla inaonekana kuwa viambajengo vilivyounganishwa vina hadhi sawa kategoria. Mfano, kuunganisha vikundi nomino viwili tunapata KN, kuunganisha virai vihusishi viwili tunapata kirai kihusishi .... na kadhalika. Hivyo, muundo wa KN uliounganishwa kama katika sentensi (18) tutakuwa na mchoro kama katika (19)

(18) Msichana mrefu huyu na mvulana mrefu yule .



Kwa sababu ya 15,17, na 21,  $X^n \rightarrow X^m$  ilipendekezwa kuzidi

$X^n \rightarrow X^{n-1}$  Kategoria ya mstari wa uvurumishaji <sup>19</sup>, yaani kichwa  $X^o$  cha  $\bar{X}$  au  $\bar{X}$  na kadhalika ndiyo kategoria ya lazima katika uvurumishaji, ilhali kategoria zile zingine si za lazima. Baltin (1987) anasema:

Nomino kuu zote katika virai kwa mujibu wa  $\bar{X}$  zinapaswa kuchukua shamirisho na iwapo neno cha kipeo ndilo neno kuu katika kirai cha kivumishi, sharti pia iwe na shamirisho .<sup>20</sup> (Tafsiri ni yetu)

Hapa chini tuliangalia vielelezo tungo vya KN vya aina mbali mbali huku tukizingatia sintaksia ya X-Bar, ambayo kama tulivyoona, inaruhusu kuwepo kwa idadi nyingi ya kategoria.

KN kinapobeba nomino moja pekee katika X-bar, kinachambuliwa ambapo uvurumishaji wa 'bar' ulioko juu kabisa ( $\bar{\bar{N}}$ ) ya N haizidishi mbili. Katika hali hii, kifundo  $\bar{N}$  kinatawaliwa na neno moja tu kama katika mfano (22)

(22)




Wakati mwingine katika Kiswahili, tuna KN ambacho kinakuwa na nomino ikifuatwa na kibainishi. Mfano ambao unadhihirisha ruwaza hii ni katika mfano

(23)




(23)




Katika mfano (23) hapo juu, kibainishi kimetumiwa kufanya kazi kama kionyeshi.

Mfano (24) hapa chini unaonyesha namna ambavyo nomino inajitokeza na kivumishi cha idadi.

(24)




Mbali na pale ambapo nomino inajitokeza na kivumishi cha idadi, nomino wakati mwingine hufuatwa na kimilikishi, nacho kimilikishi kikafuatwa na kivumishi cha idadi kama inavyoonekana katika mfano (25)



Kwa kweli, ili kuwe na hali ya mshabaha katika michoro yetu, tunapaswa kuchanganya kategoria kirai K.KIV (= Kikundi kivumishi) kama ilivyo bar zinazohusika, labda KIV; lakini wanaisimu wanapata kuwa ni muhimu na kupunguza utata 'kuchanganya' mifumo yote miwili, kurahisisha ufahamu wetu, (Radford 1981; 91)


Mbali na kufanya kazi kama kibainishi, kionyeshi wakati mwingine hufanya kazi kama kivumishi cha nomino, kama ilivyo katika mfano (26) hapa chini :

(26)




Pia mfano(27) unaonyesha nomino ikifuatwa na kivumishi cha sifa na kielezi kikifuata baadaye.

(27)



Watetezi wa sintaksia ya X-bar wanatoa sababu kuonyesha kuwa kategoria  $\bar{N}$  kwa kweli ni kiambajengo huru kinachoelezwa kwa namna yake. Hivyo basi, wanatoa ithibati za kijarabati kama inayosisitiza kuwa mkufu unaweza ukaelezwa kuwa kiambajengo, iwapo mwingine unafanana nao.  $\bar{N}$  katika mfano (28) hapa chini

28)



ni ya mfuatano wa N ----K.KIV na inaweza ikaunganishwa na mkufu mwingine kama huo kama inavyoonekana katika mfano (29) hapa chini:

(29) Mvulana mrefu sana na msichana mfupi sana hawapendani

Pili, watetezi wa sintaksia ya X-bar walitumia ithibati za kijarabati zinazosema kuwa mfuatano wa N---- K.KIV ni kiambajengo iwapo kinaweza kutumika kama

kisabiki cha yule kama tuonavyo katika mfano (30)

(30) Nampenda mtoto huyu mrefu sana kuliko yule .

Yule katika (30) ni kionyeshi kinachowachwa nyuma baada ya kudondoshwa kwa 'mtoto mrefu sana' ambayo imedondoshwa kwa sababu ilifahamika katika hali hiyo wala sio kwa sababu ya kuingizwa kwa yule. Hata hivyo, mfuatano wa N----KIV hata kwa kutumia kirai cha namna hii, ingali ni kiambajengo.

Baada ya kuthibitisha kuwa kategoria ya hapo juu  $\bar{N}$  ni kiambajengo, sintaksia ya X-bar kisha inazidi kuonyesha kuwa kategoria hii sio KN wala mshabaha wake kwa sababu haina msambao unaofanana na ule wa KN. Hata hivyo, dai hili kwamba kwa vile  $\bar{N}$  ni ndogo kuliko KN , na kwa sababu hii sio KN , halina mashiko katika lugha ya Kiswahili. Mfano (31) unaonyesha jambo hili, kwamba mfuatano wa N----K.KIV una msambao unaotoshana.

(31) i) a (Msichana mnene sana huyu) ni mzuri .

b (Msichana mnene sana) .

Mfano (31) ii) hapa chini ni sawa na Mfano (31) i) hapo juu

(31)ii) Niliongea na (Msichana mnene sana huyu) .

(Msichana mnene sana) .


Mifano (31) ii) inaonyesha KN viwili vya Kiswahili. Tofauti kubwa kati yazo ni ya kimaana tu. Kwa mfano, sentensi ya kwanza katika (31) ii) inamaanisha kuwa msichana tunayemzungumzia anajulikana; ni jambo dhahiri. Ni msichana maalum mnene hali mfano wa pili unazungumzia msichana mnene kwa jumla. Jambo hili pia linadhihirika katika mfano (31) i). Hili linaonyesha kuwa hali kuwa sentensi katika mifano ya pili zina virai kasoro neno moja (katika mfano huu ni kionyeshi huyu) Hali hii haizifanyi virai hivi kuwa na walakini kisarufi kama KN cha Kiswahili. Mfuatano wa N---K.KIV ambao hapa unaashiriwa kama  $\bar{N}$  kwa kweli ni KN 'Kidogo' katika KN 'kikubwa' cha mfuatano N---K.KIV---KIO. 'Kidogo' kwa sababu ni pungufu kwa neno moja 'huyu'. Ingawa ni kubwa kuliko kategoria leksika N<sup>o</sup> lakini sio kategoria ya katikati kati ya kategoria leksika na kategoria kirai ambazo ni tofauti sana. Badala yake, inafanana na KN. Ni kategoria inayofanana na  $\bar{N}$  ya X-bar ila tu vipengele vyake ni vichache kushinda mfuatano wa N---K.KIV---KIO lakini jambo lililo muhimu ni kwamba ingawa kuna upungufu wa vipengele, jambo hili halilifanyi wala kulipa sura mpya chini ya KN kidogo ikilinganishwa na kile kikubwa.

Ni dhamira yetu kujadili hiki kiambajengo kipya cha  $\bar{N}$  lakini kama tulivyogusia hapo juu, tunaona kuwa kionyeshi kinakuja mara upande wa kulia mara upande wa kushoto.


Tumetumia vielelezo tungo viwili kuonyesha mfuatano wa N --- K.KIV ---KIO na upande mwingine pale ambapo kionyeshi kimetangulia. Vielelezo tungo hivi

ni katika mifano ya (32)(i) na (32)(ii)

(32)(i)




(32)(ii)



Katika hali hii (rejelea 32)(i) neno kuu katika kategoria ya  $\bar{N}$  inabaki kuwa  $N^0$  wala sio  $\bar{N}$  ambayo haipo katika Kiswahili, kama ambavyo inavyoeleweka na waliopendekeza nadharia ya sintaksia ya X-bar. Hata ikiwa kwa kiwango gani kirai katika Kiswahili kimechopolewa, bado kitabakia kuwa kirai cha sarufi (katika hali hii, KN) bora tu kunapatikana neno kuu.


Tuangalie miundo ya mifano (33), (34), na (35)

(33)






(34)



(35)



KN katika (33), (34), na (35) kinakubalika katika Kiswahili. Hata hivyo vitakuwa visivyo kisarufi iwapo neno kuu, wakati wowote ule, litatolewa bila kuwepo kwa kibatala. Ni kweli kutokana na vielelezo tungo katika 4.1 kwamba sintaksia ya muundo virai kamwe haionyeshi, kwa mfano, mfuatano wa N----K.KIV kama kiambajengo kwa sababu mfumo huo unaonyesha viambajengo kama 'vizalia sawa.'

Hata hivyo faslu hii hatukuweza kuikamilisha bila kuchanganua zaidi manufaa zaidi ya nadharia ya X-bar mbali na dai kuwa kuna viambajengo vya kati, kati ya kategoria leksika na kategoria kirai. Manufaa nyingine ya sintaksia ya X-bar ni kwamba, inatutua ule utata ambapo hali ya kipashio fulani kuweza kueleweka kwa maana zaidi ya moja unadhihirika kimuundo. Mfano (36) hapa chini unatudhihirishia dai hili;

(36) Mfalme mwingereza .

na una hali ya kipashio katika (36) kueleweka kwa maana zaidi ya moja kimuundo, na tunaweza kupata fasiri mbili kama katika mifano (37)


(37) a) Mfalme ambaye ni mwingereza .

b) Mfalme wa uingereza .

Katika (37) (a) mfalme ana hadhi ya  $\bar{N}$  wala sio katika (37)( b) ambapo ni  $N^0$ . Hata hivyo, sio dhamira yetu kujadili maswala ya uelewekaji wa kimaana katika vipashio. Yako mambo mengine ambayo sintaksia ya X-bar yanaweza kusababisha upotofu nayo tulipenda kwa muhtasari kuyajadili.

Kama ilivyo katika SMV, kiambajengo ambacho hakijavumishwa nacho kilicho na msambao kama kwa mfano, kiambajengo chenye 'bar mbili' kinawekwa chini ya 'bar mbili' (kama katika SMV, ingepewa hadhi ya kirai). Kwa mfano, sentensi (38) Yohana ampenda Maria.

Wote, Yohana na Maria watawekwa chini ya hadhi ya  $N^0$  (tukichukulia kwa sasa kuwa hii ni kategoria ya 'bar' inayoshahibiana na KN), hivi kwamba (38) itakuwa kama katika mfano (39)



Sababu ya muundo (39) ni sawa na sababu tulizozitoa awali ya kuonyesha msambao, uwezekano wa kutekeleza wajibu kama kisabiki cha umbo mrejeosabiki  $\bar{N}$  kinachohusu utumiaji wa umbo fulani kuwakilisha kitu kilichotajwa awali.

Jambo jingine la kuzingatiwa ni kwamba ingawa sintaksia ya X-bar imeweka kama kanuni yake kwamba kiambajengo kilicho na X au  $X^0$  ni  $\bar{X}$  au  $X^1$ , kile kilicho na  $\bar{X}$  au  $X^1$  ni  $\bar{X}$  au  $X^2$  na vile vile kilicho na  $\bar{X}$  au  $X^2$  ni  $\bar{X}$  au  $X^3$  n.k, hii kamwe haimaanishi kwamba pale tulipo na kiambajengo cha namna moja kila mara kikibebwa katika kiambajengo kingine cha mfano wake, kitakuwa na 'bar' moja zaidi kuliko kinachobeba. Kuzingatia jambo hili bila shaka kutamaanisha

kutupilia mbali uwezekano wa kutokea kwa hali ya uchamko. Miundo ya (15), (17) na (21) inafafanua wazo hili. Kwa kweli uhitaji wa kupata nafasi ya uchamko ndipo ulifanya kanuni  $X^n \rightarrow X^{n-1}$  kuwa  $X^n \rightarrow X^m$  .

Katika sura hii, tuliona upungufu mkubwa wa SMV na namna ambavyo sintaksia ya X-bar ilivyojizatiti kuziba mianya iliyopo ya SMV. Michoro mbalimbali ya miti ilichanganuliwa na tukaona nafasi ya  $\bar{N}$  ambayo ni kiambajengo kipya kilichopendekezwa na waasisi wa X-bar, kiambajengo ambacho hakipo katika SMV. Ingawa sintaksia ya X-bar inaonekana kuwa bora zaidi kuzidi SMV, tuliona walakini zilizopo kama vile kutojitosheleza kwa nadharia hii kuhusu sheria zake ambazo zinarejelea uchamko. Pia, tatizo linatokea kuhusu msambao wa viambajengo ambavyo havijavumishwa kama tulivyoona katika mfano (39). Manufaa zaidi ya sintaksia ya X-bar yaliangaliwa mbali na dai kuwa viambajengo vya kati, kati ya kategoria virai, vinawezekana kwa kuzingatia sintaksia ya X-bar. Tuliona kuwa nadharia hii inatatua tatizo ambapo kipashio fulani kinaweza kueleweka kwa maana zaidi ya moja. Hatukujiingiza kwa undani kuhusu haya kwa vile ingetubidi tuingie kilindini kwa maswala ya kisemantiki ambayo hayakuwa katika upeo wetu, hadi pale tulipolazimika kuyataja ili tutoe ufafanuzi muafaka.

# TANBIHI

1. Kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990) Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) chuo kikuu cha Dar-es-Salaam uk. 46
2. Radford, A (1981) Transformational Syntax. Cambridge University Press, Cambridge uk.79
3. Kielelezo tungo ni mchoro wa matawi au matumizi ya mabano kuwakilisha muundo wa tungo ambapo vifundo mbalimbali vimetajwa
4. Crystal, D (1987) The Cambridge Encyclopaedia of Language Cambridge University Press Cambridge uk.97
5. Kama 4 hapo juu.
6. Kama 2 hapo juu uk. 91
7. Mgullu, R (!990) The Structure of Kiswahili Sentences: A Transformational Generative Approach. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi uk.32
8. Kapinga, M (1983) Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Dar-es-Salaam uk-9
9. Kama 8 hapo juu uk.107
10. Emonds, J. (1976) A Transformational Approach to English Syntax. Academic press, Newyork uk.151
11. Riemsdijk, H na E.Williams (1986) Introduction to the Theory of Grammar The Massachusetts Institute of Technology (MIT) press Massachusetts. uk.41
12. Riemsdijk, H(1978) A Case Study in Syntactic Markedness: The Binding Nature of Prepositional Phrases. The Peter De Ridder Press, Dordrecht uk. 30
13. Kama 12 hapo juu.
14. Tumetumia istilahi Kibainishi katika muktadha tofauti ambapo hapa, tunarejelea dhana ya Kiingereza ya ‘specifier’.

15. Tapo la isimu lililozingatia mbinu kadhaa za uchambuzi kwa lugha pamoja na uelekezi katika kipindi kilichotangulia uchanganuzi wa kisasa wa isimu, hasa katika kipindi cha karne ya 18-19 huko ulaya
16. Colen, A (1983) ' Observations on the syntax of English nominals' katika Tasmowski, L na D. Willems (whr) Problems in Syntax. Plenum press, NewYork uk 86.
17. Kama 2 uk. 97-98
18. Katika sarufi geuzamaumbo zalishi, hii ni sifa ya kisarufi inayoweza sentensi nyingi zisizo na kikomo kutungwa kutokana na kanuni fulani. Kwa Kiingereza, neno uhamko ni 'recursiveness'
19. Tumetafsiri dhana ya Kiingereza ya 'projection' kama uvurumishaji katika Kiswahili. Kwa mitarafu hii, uvurumishaji wa 'X' ni tafsiri ya 'projection of 'X'
20. Baltin, M (1987) ' Degree Complements' Katika Ojeda, A na G. Huck (whr) Syntax and Semantics. Academic press inc. London uk.24

## 5.0

## SURA YA TANO

### 5.0.0

### HITIMISHO

Katika utafiti huu, ilidhihirika wazi kuwa kipashio kinachotangulia vipashio vingine katika KN ni nomino. Hatimaye, nomino hufuatwa na vivumishi ambavyo navyo vinaweza vilevile kutangulia hizo nomino katika miktadha maalum.

Sura ya kwanza ilihusu utangulizi wa kazi hii. Ilieleza utangulizi wa kijumla wa uchanganuzi wa KN cha Kiswahili na kuangaza vipengele mbalimbali vitakavyoshughulikiwa katika uchanganuzi huo.

Sura ya pili ilituangazia mengi kuhusu nomino ya Kiswahili. Tuliona kuwa mizizi ya nomino katika Kiswahili sharti iwe na kiambishiawali kinachoambishwa na ambacho kinafanya neno kuwa na maana kamili na uamilifu wake kukamilika. Pia ilidhihirika wazi katika sura hii kwamba baadhi ya nomino ni nomino zinazotokana na mnyambuliko, huku zikiwa zimenyambuliwa kutoka kwa vitenzi au vivumishi. Nomino hizi zinazotokana na mnyambuliko nazo zinachukua viambishiawali na zinafanana na nomino nyingine.

Katika sura ya tatu, tulichunguza kategoria tofauti za kisintaksia zinazohusiana na KN. Tuliona kuwa hizi zilikuwa kategoria zilizohusika na uvumishaji wa nomino na kwamba vingi vya vivumishi hivi sharti vichukue viambishiawali



sawa na vya nomino vinavyovumisha. Tulihitimisha kwa kusema kuwa hivi vinaweza vikaelezwa na kutofautishwa kwa kutumia aina ya mizizi ambayo viambishiawali vinachukua. Isitoshe, tulipata kwamba, kwa kweli, ni lugha yenyewe ambayo inaweza ikatoa maelezo ya kategoria hizi wakati inapozitumia, kwa sababu neno amilifu huwa halipo kama kategoria leksika kuu.

Vivumishi kama vile 'kila' vilipatikana kufanya kazi tofauti na vivumishi vingine kwa vile 'kila' huwa haifuati nomino inayovumisha, lakini huwa inatangulia. Kivumishi hiki vilevile huwa hakina viambishiawali. Vivumishi vyote vilipatikana kuwa si vya lazima huku nomino pekee ikiwa ndiyo kategoria ya lazima katika KN.

Pia katika sehemu hii, tuliona kuwa vitambulishi vya ukubaliano wa nomino huzalishwa kwenye KN. Vipashio hivi ni kitambulishi cha ngeli au nomino, kitambulishi cha kiima na kitambulishi cha yambwa.

Katika sura ya nne, tuliona kuwa  $\bar{N}$  kwa kweli haimo katika KN cha Kiswahili. Hakika, hatukugundua kategoria yoyote mpya au kategoria nyingine tofauti iliyoko katikati ya  $\bar{N}$  na  $N^0$  (Kategoria kirai na kategoria leksika). Hivyo, katika uchanganuzi wetu, dhana ya X-bar ya uvurumishaji wa  $X^0$  katikati ya  $\bar{N}$  na  $X^0$  haina mashiko yoyote angalau katika uchanganuzi wa KN cha Kiswahili.

Ile kategoria inayoelezwa katika Kiingereza kama  $\bar{N}$  na wanasintaksia wa X-bar

ilipatikana kuwa inafanana na KN cha Kiswahili na hivyo basi, kushahibiana na kategoria  $\bar{N}$  ya X-bar. Ni kweli kwamba kategoria  $\bar{X}$  huenda ikawa tofauti na kategoria  $N^0$  kwa jambo moja, ambalo ni kuwa linabeba zaidi ya neno moja ilhali  $N^0$  ni kategoria leksika. Hata hivyo kategoria nyingine za X-bar ambazo zilishughulikiwa hapa kama vile  $N^0$ ,  $\bar{N}$  na  $\bar{\bar{N}}$  zilipatikana kuwa ni KN cha Kiswahili na zilikuwa sawa kisarufi. Kwa sababu  $N^0$ ,  $\bar{N}$  na  $\bar{\bar{N}}$  zina msambao ulio sawa, Radford (1981:108) anasema:

Uamilifu wa kimsingi wa kategoria ni kupambanua  
msambao wa maneno na virai katika lugha, kwa vile  
elementi hizo zilizo na msambao ulio sawa  
zinagawanywa katika kategoria hiyo hiyo.

(Tafsiri ni yetu)

Hivyo basi, tunapaswa kuvigawanya viambajengo vya kati ya  $N^0$  na  $\bar{\bar{N}}$  kwa kategoria ya KN. Kinachofanyika hapa ni kwamba kiambajengo kimoja cha aina moja kama  $\bar{\bar{N}}$  kinabebwa kwenye kiambajengo kingine cha aina hiyo hiyo (tazama mfano 32) Katika sehemu 4.2. Katika 4.1 tulisema kwamba KN kinaweza kuwa neno (kinapokuwa neno kuu) au kinaweza kuwa kifungu cha maneno kilicho na neno kuu, tunaingiza kategoria  $N^0$  kama KN. Hili linamaanisha kwamba  $N^0$  na KN ni sawa katika uamilifu kama KN kilivyo na  $N^0$  kama kipengele cha nafasi ya KN kwa vile hakivumishwi.

Maelezo haya yanatupeleka katika sehemu yetu ya nadharia tete ambapo tulisema kuwa KN cha Kiswahili kinaweza kuchambuliwa kikamilifu kwa kutumia sintaksia ya X-bar. Tumeona kuwa nadharia tete hii haikuweza kutoshelezwa ipasavyo. Uchambuzi wa KN kwa kutumia nadharia hii haikuwa kamilifu kama ambavyo watetezi wake walivyopendekeza. Dosari zilizoko tayari zimechanganuliwa. Fauka ya haya, nadharia tete yetu nyingine ilikuwa kwamba KN cha Kiswahili kina viambajengo vya kati, kati ya kategoria leksika na kategoria ya virai. Matokeo yetu yalikuwa kwamba ile kategoria inayoelezwa kama  $\bar{N}$  na wanasintaksia wa X-bar kwa kweli ni KN cha Kiswahili na hivyo basi inashahibiana na  $\bar{N}$  ya X-bar.

Sura hii vilevile kwa muhtasari iliweza kutoa sababu nyingine zinayoifanya nadharia ya X-bar kuwa ya manufaa mbali na kwamba ina viambajengo vya kati, kati ya kategoria kirai na kategoria leksika. Tuliona kuwa sintaksia ya X-bar inatatua lile tatizo linalotokea la kimaana, ambapo sentensi au kishazi kimoja kinaweza kuashiria dhana mbalimbali, jambo ambalo SMV halikuweza kamwe kutatua. Tulitoa mifano ili kutoa mwangaza wa kile tulichonua kueleza kuhusiana na swala hili.

## 5.1 MAPENDEKEZO

Kama tulivyosema katika sura ya kwanza kwenye upeo wa utafiti, hatukuweza kushughulikia aina za sentensi zote za Kiswahili. Sisi tulijikita katika sentensi

sahili. Tunapendekeza kwamba utafiti zaidi ufanywe juu ya KN katika sentensi changamano na sentensi ambatano kwa kutumia nadharia ya sintaksia ya X-bar, ili tupate uamilifu wa nadharia hii katika sentensi nyingine mbali na sentensi sahili, huku tukizingatia KN cha Kiswahili.

Kuna umuhimu wa kuangalia muundo wa sentensi ya Kiswahili kwa kutumia baadhi ya nadharia zinazopendekezwa na ambazo hususan zinajaribiwa kwa kutumia lugha zisizo za nasaba moja na Kiswahili. Mfano wa nadharia hizi ni kama vile X-bar. Tunapendekeza kutambuliwe sababu za wanaisimu kuegemea sana nadharia hizi mpya na 'kutupilia mbali' nadharia kama vile SZGM. Utafiti ufanywe kuangalia ni kwa nini nadharia zingine za 'umilikifu na masharti' zina nafasi kubwa katika uchanganuzi wa KN kuliko zingine.

KN cha Kiswahili kinaweza kupigwa msasa ipasavyo ikiwa utafiti utafanywa kuhusu KT cha Kiswahili na uhusiano wao kuangaliwa. Tunapendekeza utafiti ufanywe unaohusu KT cha Kiswahili kwa kutumia nadharia hizi mpya wala sio kuegemea nadharia ya X-bar-kama tulivyofanya sisi. Fauka ya hayo, ugeuzajimaumbo unapaswa kufanyiwa utafiti kwa kuzingatia nadharia ya X-bar wala sio SZGM, katika kipengele cha KN cha Kiswahili.

Ni matumaini yetu kuwa tasnifu hii itakuwa msingi unaofaa na ulio thabiti kwa utafiti zaidi katika kipengele hiki cha sintaksia kwenye nyanja hii ya isimu.

# MAREJELEO

- ADEWOLE, S (1986): 'A Syntactic basis for noun classification in Kiswahili', katika Kiswahili vol.53/1 na 2. TUKI, Dar-es-Salaam.
- AKMAJIAN, A., R. DEMERS na R. HARNISH (1984): Linguistics: An Introduction to language and communication. Massachussets Institute of Technolgy (MIT) Press, Cambridge.
- ALYESHMERNI, M na P. TAUBR (1975): Working with Aspects of Language. Harcourt Brace Jovanovich, Inc. New York.
- ASHTON, E (1947): Swahili Grammar Including Intonation, London.
- BACH, E (1968): 'Nouns and noun phrases' katika Bach, E na R. Harm (whr) Universals in Linguistic Theory. Holt, Rinehart and Winston, Inc. New York.
- BALTIN, M (1987): 'Degree complements' Katika Ojeda, A na G. Huck (whr) Syntax and Semantics. Academic Press, Inc. London.
- BORNSTEIN, D (1977): An Introduction to Transformational Grammar. Winthrop Publishers, Inc. New York.
- BRANDON, F (1976): "Quantification, negation and the semantic isolation of sentence," Katika Moravcsik, E (Mhr) Working Papers on Language Universals Vol.20. Stanford University Press, California.
- CHOMSKY, N (1964): Current Issues in Linguistic Theory, Mouton, The Hague.
- \_\_\_\_\_ (1965): Aspects of the Theory of Syntax. Cambridge, Massachusetts.
- \_\_\_\_\_ (1970): "Remarks on nominalization." Katika Jacobs, R na P. Rosenbaum (whr) Readings in English Transformational Grammar. Ginn and Co. Waltham, London.
- \_\_\_\_\_ (1971): Syntactic Structures. Mouton and Co. Publishers, The Hague.
- \_\_\_\_\_ (1976): Reflections on language pantheon Books, Newyork.

- \_\_\_\_\_ (1977): " Conditions on rules of grammar" Katika Cole, w (mhr) Current Issues in Linguistic Theory. Indiana University press, Bloomington.
- \_\_\_\_\_ ( 1981 a): "Principles and Parameters in Syntactic theory', Katika Horstein, N na D. Lightfoot( whr) Explanation in Linguistics: The Logical Problem of Language Acquisition. Longman, London.
- \_\_\_\_\_ (1981b): Lectures on Government and Binding. Foris, Dordrecht.
- COLEN, A( 1983): "Observations on the Syntax of English nominals," Katika Tasmowski, L na D. Willems(whr) Problems in Syntax. Plenum press, NewYork.
- CRYSTAL, D (1987a): The Cambridge Encyclopaedia of Language. Cambridge University press, Cambridge.
- CULICOVER, P(1976): Syntax. Academic Press, New York.
- CULICOVER,P na A. AKMAJIAN (1977): Formal Syntax. Academic press, New York
- DINNEEN, F(1967): An Introduction to General Linguistics.Holt, Rinehart and Winston Inc. New York.
- DOWNING, B (1978): "Some Universals of relative clause structure', Katika Greenberg, J (mhr) Universals of Human Language. Stanford University Press, California
- FILLMORE, C (1968): ' The case for case' katika Bach, E na Harms, R (whr) Universals in Linguistic Theory. Holt, Rinehart and Winston, New York.
- GADZAR, G (1982): 'Phrase structure grammar' katika Jacobson, P na G. Pullum. (whr) The Nature of Syntactic Representation. Reidel, Boston.

- GREENBERG, J (1963): 'Some Universals of grammar, with particular reference to the order of meaningful elements,' katika Greenberg, J (mhr) Universals of Language. Massachusetts Institute of Technology (MIT) Press, Massachusetts.
- \_\_\_\_\_ (1966): The language of Africa. Indiana University press, Bloomington.
- GUTHRIE, M (1967): The Classification of Bantu Languages. Dawson Pall Mall, London.
- HAIK, I na L. TULLER (1989): Current Approaches to African Linguistics (vol.6.) Foris, Dordrecht.
- HARRIES, L (1965): 'Locative Agreement in Swahili. Swahili Vol 35.
- HARRIS, R (1987): Reading Saussure. Gerald Duckworth and Co. Ltd, London.
- HARTMANN, R na F. STORK (1973): Dictionary of Language and Linguistics Applied Science Publishers Ltd. London.
- HORROCKS, G (1987): Generative Grammar. Longman, London.
- HUDDLESTON, R (1976): An Introduction to English Transformational Grammar. Longman, London.
- JACKENDOFF, R (1972): Semantic Interpretation in Generative Grammar. MIT Press, Massachusetts.
- \_\_\_\_\_ (1977): X̄-Syntax: A study of Phrase structure. MIT press, Massachusetts.
- JACOBSEN, B (1977): Transformational Generative Grammar. North- Holland publishing company, Amsterdam
- JESPERSEN, O (1924): The Philosophy of Grammar. George Allen and Unwin Ltd. London.
- \_\_\_\_\_ (1969): Analytic Syntax. Holt, Rinehart and Winston, Inc. New York.

- JOHNSON, F (1939): A Standard English-Swahili Dictionary. OUP, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1939): Standard Swahili-English dictionary, OUP, Nairobi.
- KAMANGO, D (1980): A Syntactic Analysis of the Ki-Giriama Noun Phrase. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi
- Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990): TUKI, chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981): TUKI, chuo kikuu cha Dar-es-salaam.
- KAPINGA, M (1983): Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. TUKI, Dar-es-Salaam.
- KATZ, J na P. Postal (1964): An Integrated Theory of Linguistic Descriptions. MIT Press, Massachusetts.
- LASNIK, H (1988): Lectures on Binding and Empty categories. MIT Press, Massachusetts.
- LEHMANN, W (1978): Syntactic Typology. The Harvester press, Sussex.
- LIGHTFOOT, D. (1979): Principles of Diachronic Syntax. Cambridge University press, Cambridge.
- LONGOBARDI, G (1985): "Connectedness and island constraints," katika Gueron, J, G. Obenauer na Y. Pollock (whr) Levels of Syntactic Representation 11 Foris, Dordrecht.
- LOGGMAN, A (1965): Swahili Grammar and Syntax. Duquesne University Press, Pittsburgh.
- LYONS, J (1968): Introduction to Theoretical Linguistics. Cambridge University press, Cambridge.
- MANYORA, H (1992): Intra-Sentential Relationships of Logooli NPs: A Government and Binding Approach Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- MATTHEWS, P (1972) Inflectional Morphology. Cambridge University Press, Cambridge.



- \_\_\_\_\_ (1981): Syntax. Cambridge University Press, Cambridge.
- MATU,P (1991): WH-Movement in Kiswahili. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- MAW,J (1969): Sentences in Swahili: A study in their Internal Relationships. The presham press, Surrey, England.
- MBAABU, I (1992): Sarufi ya Kiswahili. Longman, Nairobi
- MEBO, P (1989): A Syntactic Analysis of the Lwisukha NP: A survey into X-Bar Syntax. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- MFAUME, G(1984): Misingi ya isimu na lugha ya Kiswahili. Dar-es-Salaam
- MGULLU, R(1990): The Structure of Kiswahili Sentences: A Transformational Generative Approach. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- MORAVCSIK, E (1978): "Agreement"katika Greenberg, J(mhr) Universals of Human Language. Stanford University Press, California.
- MSANJILA, Y (1985): 'Tofauti za msingi kati ya tungo nomino na tungo vitenzi katika Kiswahili,' katika Mdee, J na E. Mbogo (whr) Mulika na. 17 TUKI, chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.
- MWERI, G (1991): NP Movement in Ki-Giriama. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- MYACHINA, E(1973): The Swahili Language: A Descriptive Grammar. OUP, London.
- OMONDI, L (1982): The Major Syntactic Structures in Dholuo. Dietrich Reimerverlag, Berlin.
- \_\_\_\_\_ (1986): Research Methods in Syntax: Illustrative Description of Dholuo Nominal Group in Scale and Category Theory of Grammar. Dietrich Reimerverlag, Berlin.
- PARTEE, B (1975): Fundamentals of Mathematics for Linguistics. Reidel, Dordrecht.

- PEI, M (1966): Glossary of Linguistic Terminology. Columbia University Press, New York.
- PEREZ, C (1985): Aspects of Complementation in three Bantu Languages. Tasnifu ya PH.D chuo kikuu cha Wisconsin, Madison.
- PERLMUTTER, D (1971): Deep and surface structure constraints in Syntax. Holt, Rinehart and Winston, New York.
- POLOME, E(1967): Swahili Language handbook. Centre for Applied Linguistics. Washington.
- RADFORD, A(1981): Transformational Syntax. Cambridge University Press, Cambridge.
- RANDOLPH, Q ( 1973): A University Grammar of English. Longman Group, London.
- REINHART, T (1976): The Syntactic Domain of Anaphora. MIT press Massachusetts.
- RIEMSDIJK, H (1978): A Case Study in Syntactic Markedness: The Binding Nature of Prepositional Phrases. The Peter De Ridder Press, Dordrecht.
- RIEMSDIJK, H na E. WILLIAMS (1986): Introduction to the Theory of Grammar. MIT Press Massachusetts.
- RODNEY, H (1978): An Introduction to English Transformational Syntax. Longman, London
- ROMAINE, S(1983): 'Syntactic change as category change by reanalysis and diffusion.' katika Davenport, M, E. Hansen na H. Nielsen (whr) Current Topics in English Historical Linguistics. Odense University Press, Odense.
- ROSENBAUM, P na R. JACOBS (1968): English Transformational Grammar. Ginn and Co. Ltd. London.
- SEWANGI, S (1993): The Syntax of Empty category in Kiswahili Simple Sentences: The Government-Binding Approach. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- STOCKWELL, R (1973): The major Syntactic Structures of English. Holt Rinehart and Winston, Inc. New York.

- THANDE, C(1988): PRO-nominalization in Kiswahili: Government and Binding Approach. Tasnifu ya M.A chuo kikuu cha Nairobi.
- VITALE, A (1981): Swahili Syntax. Newyork
- WALL, R (1972): Introduction to Mathematical Linguistics.  
Prentice - Hall New Jersey.
- WELMERS, G(1973): African Language Structure. The University of California press, California.
- WHITELEY, W. (1969): Some Problems of Transitivity in swahili. School of Oriental and African Studies, University of London, London.
- ZAWAWI, S (1971): Kiswahili kwa Kitendo. Harper and Row, New York.